# UREJELEZI KATIKA GAZETI LA *TAIFA LEO:* MTAZAMO WA KIPRAGMATIKI

**KIRUI SIMON KIPKOECH**

**C50/9327/2017**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**JULAI, 2021**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa ili kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine.

.................................................. 26|11|2021..................................................

KIRUI SIMON KIPKOECH TAREHE

C50/9327/2017

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

.................................................. 30|11|2021..................................................

DKT PRISCA JERONO TAREHE

Msimamizi

.................................................. Novemba 29, 2021..................................................

DKT BASILIO MUNGANIA TAREHE

Msimamizi

## TABARUKU

Ninawatabarukia marehemu mamangu, Annah Milgo, babangu, William Milgo, Mke wangu mpendwa, Beatrice Kirui na wanangu Faith Chebet, Adams Kiplangat na Joy Chepchirchir, ndugu zangu Samwel Kirui, Joyce Chepngetich, Mercy Chepkemoi na Robert Kirui.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, ninatoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na mahitaji yote yaliyohitajika katika safari hii ya masomo. Bila Yeye, nisingeweza kufikia kiwango hiki katika masomo yangu.

Pili, ninatoa shukrani za kipekee kwa wasimamizi wangu Dkt. Prisca Jerono na Dkt. Basilio Mungania kwa ushauri wao. Kupitia ushauri wao wa mara kwa mara, kazi hii imekamilika. Asanteni kwa kujitolea kusoma kila neno katika tasnifu hii na kunielekeza. Ushauri wenu umenichochea kuendelea kimasomo hadi kufika kiwango cha juu. Mungu awabariki. Aidha, ninatoa shukrani kwa Prof. John Hamu Habwe kwa kunielekeza wakati nilihitaji ushauri wake katika kazi hii.

Tatu, ninawashukuru wahadhiri wangu waliojitolea kutufunza kozi mbalimbali zilizotuwekea msingi kazi hii. Wahadhiri hawa ni: Prof. Kineene Wamutiso, Prof. Iribe Mwangi, Prof. Rayya Timmamy, Prof. Kyalo Wadi Wamitila, Prof. Tom Olali, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kithaka Wa Mberia, Prof. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga na mwalimu Leo Sanja.

Nne, shukrani ziwaendee wanagenzi wenzangu: Simon Peter Katui, Joseph Kang'ethe, Oliver Ogutu, Yunny Amisi, Agatha Susa, Purity Muthomi, Meshack Kithure, Deon Musau, Benard Mulati na Alex Mwebesa kwa kuhimizana na kushirikiana pamoja kimasomo.

Tano, ninawashukuru wazazi wangu, babangu William Milgo na marehemu mamangu Annah Milgo. Kupitia malezi mema mlionipa, nimeweza kufikia kiwango hiki katika masomo. Mlijinyima mambo mengi ili niweze kuendelea na masomo. Asanteni, Mungu awabariki.

Sita, ninatoa shukrani za dhati kwa mke wangu mpendwa Beatrice Kirui na wanangu Faith Chebet, Adams Kiplangat na Joy Chepchirchir. Mlinipa ruhusa ya kuendeleza masomo na kuniombea kila wakati nilipokuwa chuoni. Asanteni sana.

Mwisho, ninawashukuru walimu wangu wa shule ya msingi na shule ya upili walionihimiza kufanya bidii katika masomo. Walimu hao ni kama vile Bw. Mike Mutai, Bw. Cheboi, Bi. Mkala, Bi. Okello, Bi. Wangio, Bi. Maguke na Bi. Onindo. Mungu awabariki. Aidha, natoa shukrani kwa walimu wenzangu wa Shule ya Upili ya Kyogong kwa kunihimiza kila wakati kuendelea na uandishi wa tasnifu hii.

## IKISIRI

Tasnifu hii ililenga kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* na jinsi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini. Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu: kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo*, kubainisha jinsi urejelezi ulivyotumika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo* na kubainisha iwapo nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Uhusiano zinaweza kutumika kuonyesha umuhimu wa urejelezi katika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo*. Data iliyotumika kufikia malengo haya ya utafiti ilitolewa kutoka *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo*. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) ilitumika katika utafiti huu kwa kuangazia mtazamo wa Halliday (1976). Aidha, nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Wilson (2003) na Wilson na Sperber (2002) ilitumika kama nadharia changizi katika kufafanua jinsi wasomaji wanavyofikia maana tambuzi katika matini. Data ya utafiti huu imechanganuliwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa urejelezi wa kiendofora, urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha umetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Data ya utafiti huu imewasilishwa kwa kutumia maelezo na majedwali kuonyesha jinsi aina mbalimbali za urejelezi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

| | |
|---|---|
| **Mshikamano**: | Sifa ya matini kufasiriwa kama kitu kizima wala sio kama sentensi zilizotengana. |
| **Mshikamano wa kileksia**: | Jinsi maneno yanayohusiana yanachaguliwa kuonyesha uhusiano wa vipashio katika matini. |
| **Mshikamano wa kisarufi:** | Matumizi ya vipashio vya kisarufi kuunganisha sentensi au aya katika matini ili kuonyesha uhusiano wa kimaana. |
| **Urejelezi:** | Ufasiri wa kipashio kimoja kisemantiki kupitia kwa kurejelea kipashio kingine katika matini. |
| **Endofora**: | Aina ya urejelezi unaojikita katika matini. |
| **Eksofora/kisabiki nje**: | Aina ya urejelezi unaomhitaji msomaji kufasiri kitajwa kwa kuzingatia mazingira nje ya matini. |
| **Anafora**: | Kipashio cha kiisimu kinachotumiwa kurejelea kilichotajwa katika tungo. |
| **Katafora**: | Kipashio cha kiisimu kinachotumiwa kurejelea kitakachotajwa katika tungo. |
| **Urejeleo wenza**: | Viambajengo viwili au zaidi vinavyorejelea kitajwa kimoja katika matini. |
| **Eksiplikecha:** | tamko wazi |
| **Implikecha:** | tamko isiyo wazi |
| **Dhana maalum ya kihali**: | Dhana maalum inayopatikana kupitia kwa kuhusisha neno au tamko na muktadha ili kupata maana tofauti kidogo na maana iliyosimbwa na neno au tamko fulani. |
| **Viathiri vya utambuzi:** | Vichocheo au vidokezo vinavyoweza kuelekeza msikilizaji au msomaji kuelewa jambo au kitu kinachosemwa. |
| **Pragmatiki Leksika:** | Tawi la isimu linalofafanua jinsi maana ya dhana inaweza kubadilika kulingana na muktadha |
| **Maana ya Kikamusi:** | Maana ya neno au tamko iliyohifadhiwa/ zilizohifadhiwa akilini mwa msikilizaji au msomaji. |
| **Uhusiano:** | Hali ya msemaji au mwandishi kusema jambo linaloweza kufasiriwa kwa njia rahisi na msikilizaji au mwandishi |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Dkt. | Daktari |
| Prof. | Pofesa |
| PSB | Public Service Board |
| Bw. | Bwana |
| NMK | National Museums of Kenya |
| ODM | Orange Democratic Movement |
| BBI | Building Bridges Initiative |
| DCI | Director of Criminal Investigations |

## YALIYOMO


**UNGAMO ... ii**

**TABARUKU ... iii**

**SHUKRANI ... iv**

**IKISIRI ... v**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU ... vi**

**ORODHA YA VIFUPISHO ... vii**

**MAJEDWALI ... xi**

**SURA YA KWANZA: USULI WA MADA ... 1**

1.1 Utangulizi ... 1

1.2 Tatizo la Utafiti ... 3

1.3 Maswali ya Utafiti ... 4

1.4. Malengo ya Utafiti ... 4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ... 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ... 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii ... 6

1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Sarufi Amilifu ... 7

1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Uhusiano ... 8

1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mshikamano ... 10

1.7.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Urejelezi ... 13

1.8 Msingi wa Kinadharia ... 15

1.8.1 Nadharia ya Sarufi Amilifu ... 15

1.8.1.1 Maana Tambuzi ... 17

1.8.1.2 Maana Husishi ... 20

1.8.1.3 Maana Matini ... 21

1.8.2 Nadharia ya Uhusiano ... 22

1.9 Njia ya Utafiti ... 26

1.9.1 Njia za Kuchanganua Data ... 27

1.9.2 Hitimisho ... 27

**SURA YA PILI: VIPENGELE MUHIMU VYA MSHIKAMANO............................28**
2.1 Utangulizi....................................................................................................28
2.2 Vijenzi vya Mshikamano ..............................................................................28
2.2.1 Mshikamano wa Kileksia ........................................................................ 29
2.2.1.1 Urudiaji wa nomino muhimu.................................................................. 29
2.2.1.2 Matumizi ya Sinonimu ........................................................................... 29
2.1.2.3 Matumizi ya Haiponimu......................................................................... 29
2.2.2 Mshikamano wa Kisarufi ........................................................................ 30
2.2.2.1 Urejelezi................................................................................................. 30
2.2.2.2 Urejelezi wa Kieksofora ........................................................................ 30
2.2.2.3 Urejelezi wa Kiendofora......................................................................... 30
2.2.2.4 Anafora .................................................................................................. 31
2.2.2.5 Katafora ................................................................................................. 31
2.2.3 Urejelezi wa nafsi...................................................................................... 32
2.2.3.1 Viwakilishi Ngeli.................................................................................... 33
2.2.3.2 Vimilikishi.............................................................................................. 34
2.2.4 Urejelezi wa kuashiria/kuonyesha........................................................... 35
2. 2.5 Urejelezi wa kulinganisha ...................................................................... 36
2.2.6 Uunganishaji.............................................................................................. 37
2.2.7 Ubadilishaji ............................................................................................... 39
2.2.7.1 Ubadilishaji wa nomino.......................................................................... 39
2.2.7.2 Ubadilishaji wa vitenzi ........................................................................... 40
2.2.7.3 Ubadilishaji wa vishazi........................................................................... 40
2.2. 8 Udondoshaji ............................................................................................. 41
2.2.9 Hitimisho................................................................................................... 42
**SURA YA TATU: AINA ZA UREJELEZI KATIKA GAZETI LA TAIFA LEO....43**
3.1 Utangulizi....................................................................................................43
3.2 Urejelezi Nafsi .............................................................................................43
3.2.1 Viwakilishi Nafsi Viambata ..................................................................... 43
3.2.2 Viwakilishi Nafsi Huru ............................................................................ 48

3.2.3 Vimilikishi........ 51
3.2.4 Katafora........ 54
3.3 Urejelezi wa Kuashiria........57
3.4 Urejelezi wa Kulinganisha........60
3.5 Ubadilishaji........62
3.6 Udondoshaji........65
3.7 Uunganishaji........67
3.8 Urudiaji wa Nomino Muhimu........70
Hitimisho........72

**SURA YA NNE: MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........74**
4.1 Utangulizi........74
4.2 Muhtasari........74
4.3 Hitimisho........76
4.4 Mapendekezo........77
**MAREJELEO ........79**
**VIAMBATISHO ........84**

## MAJEDWALI

Jedwali la Urejelezi Nafsi………………………. ...........................................................32
Jedwali la vimilikishi Nafsi ..........................................................................................34

# SURA YA KWANZA

# USULI WA MADA

Katika sura hii, tutaweka msingi utafiti wetu kwa kujikita katika sehemu zifuatazo: utangulizi, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia na njia za utafiti.

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unachunguza jinsi urejelezi unavyotumika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo*. Nadharia ya Sarufi Amilifu ambayo husisitiza uamilifu wa maana katika lugha itatumika kama msingi wa utafiti huu. Vilele vile, nadharia ya uhusiano itatumika kama nadharia changizi. Nadharia ya uhusiano itatumika kama nadharia changizi kwa sababu inafafanua jinsi msikilizaji au msomaji anavyofikia maana iliyokusudiwa na msemaji au mwandishi akilini mwake kwa kufuata utaratibu wa utambuzi (Wilson & Sperber, 1995). Nadharia hii itatumika kufidia upungufu wa nadharia ya Sarufi Amilifu wa kutofafanua jinsi msomaji anavyofikia maana tambuzi katika matini.

Kulingana na nadharia ya Sarufi Amilifu, maana tambuzi huhusika na matumizi ya lugha kwa namna ya kipekee kurejelea dhana mbalimbali. Msomaji hufikia maana tambuzi kupitia kwa kuhusisha neno na dhana mbalimbali kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa vile neno moja linaweza kurejelea dhana mbalimbali, kuna haja ya kuwepo na utaratibu unaofuatwa ili kuonyesha jinsi ya kuhusisha neno na dhana mbalimbali ili kufikia maana iliyokusudiwa na msemaji au mwandishi kwa msikilizaji au msomaji. Hata hivyo, nadharia ya Sarufi Amilifu inafafanua wazi jinsi maana matini inaweza kufikiwa na msomaji katika matini ili kufanikisha mawasiliano. Kulingana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Uhusiano haziwezi kutosheleza mahitaji ya utafiti wetu kivyao bali zinaweza kutumika pamoja ili kufanikisha mawasiliano na kufikia malengo ya utafiti huu.

Lugha ni chombo muhimu cha kuwezesha binadamu kuwasiliana. Mawasiliano huhusisha mzungumzaji au mwandishi pamoja na msikilizaji, msomaji au mtazamaji. Katika utafiti huu, tutachunguza matumizi ya aina mbalimbali za urejelezi katika kuleta mshikamano

katika *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Gazeti hili linamilikiwa na kampuni ya *Nation Media Group*.

Ili mawasiliano yafanikiwe, mzungumzaji au mwandishi ni lazima awasilishe ujumbe wake kwa njia inayofasiriwa na msikilizaji, msomaji au mtazamaji wake kwa njia inayofaa. Ili ujumbe uwafikie wasomaji wa gazeti, ni sharti sentensi ziwe na mshikamano. Mshikamano ni njia tofauti ambazo vijenzi vya sentensi ya matini vimeunganishwa. Hii ina maana kuwa maneno tunayoyasikia na kutumia yameunganishwa pamoja ili kuleta maana. Sentensi huundwa na elementi zinazohusiana kimaana ambazo huunganishwa ili kuunda matini. Kwa hivyo, mshikamano ni ile sifa ya matini kufasiriwa kama kitu kizima wala sio sentensi ambazo zimetengana. Sentensi ambazo hazina mshikamano huwatatanisha wasomaji na hivyo kufanya ujumbe usifasiriwe kwa urahisi.

Urejelezi ni ufasiri wa kipashio kimoja kisemantiki kupitia kwa kurejelea kipashio kingine katika matini. Urejelezi humsaidia msomaji kutambua nomino na sehemu inayosisitizwa katika sentensi. Isitoshe, urejelezi unaweza kutumika kuleta taharuki wakati wa kusoma matini. Kuna aina mbili za urejelezi: urejelezi wa kieksofora na urejelezi wa kiendofora. Katika urejelezi wa kieksofora, msomaji anahitajika kufasiri kitajwa kwa kuzingatia mazingira nje ya muktadha wanayoshiriki msomaji na mwandishi. Msomaji hajifungi kwenye muktadha wa neno, kirai, kishazi au sentensi kwenye matini ili kufasiri kitajwa. Urejelezi huu hautaji kitajwa bali unaashiria kuwa maana ya kitajwa inapatikana kwa kurejelea muktadha.

Urejelezi wa kiendofora ni aina ya urejelezi ambao hujikita katika matini na huwa ni za aina mbili: katafora na anafora. Urejelezi wa katafora hurejelea neno, kirai, kishazi au sentensi ambayo itatajwa mbele katika matini. Anafora ni aina ya urejelezi ambayo neno, kirai, kishazi au sentensi hurejelea nyuma kwa neno, kirai, kishazi au sentensi zilizotumika awali katika matini.

Urejelezi wa kianafora unachunguzwa kwa sababu wakati mwingine kuna utata wa kufasiri maana ya urejelezi wa kianafora hasa wakati ambapo kuna viambajengo viwili au zaidi vinavyorejelea kitu kile kile kimoja. Utata wa kianafora hutokea wakati matini ina vitajwa viwili au zaidi katika sentensi hiyo au sentensi iliyotangulia. Kwa mfano, katika sentensi ‘Yeye alisema kuwa yeye ni mkulima’ kuna utata wa kufasiri nomino inayorejelewa.

Kiwakilishi nafsi huru ‘yeye’ huweza kumrejelea mzungumzaji ambaye anajirejelea au mtu mwingine anayezungumziwa ambaye hayuko karibu na mzungumzaji.

Ingawa anafora na katafora hutumika katika matini, katafora haitumiki sana ikilinganishwa na anafora (Halliday na Hasan, 1976). Urejelezi wa kianafora unafaa zaidi katika kuleta mshikamano kwa sababu unaonyesha uhusiano na sehemu ya matini iliyotangulia. Kutokana na maelezo haya, ni bayana kuwa matumizi ya urejelezi wa kianafora huchangia pakubwa katika ufasiri wa maana katika matini.

Wasomaji wanafaa kuelewa jinsi ya kutambua na kufasiri aina mbalimbali za urejelezi zinazochangia kuleta mshikamano katika matini na hivyo kufanya gazeti kueleweka kwa wasomaji. Utafiti huu utaweka wazi jinsi ufasiri wa aina mbalimbali za urejelezi katika gazeti unaweza kuleta utata wa kimaana na utata huo unaweza kutatuliwa kwa kuhusisha vipengele vya kiisimu kama vile pragmatiki, sintaksia na semantiki katika ufasiri wa maana katika matini.

Katika utafiti huu, tutachunguza aina mbalimbali za urejelezi kwa sababu vijenzi hivi ni lazima vihusishwe katika uandishi. Waandishi mbalimbali hutumia vijenzi hivi kwa njia mbalimbali na hivyo kuleta utata. Ili kuondoa utata huu, msomaji anahitajika kuwa na uwezo wa kutambua na kufasiri maana ya urejelezi katika matini anayosoma. Utafiti huu utajikita katika nakala za *Habari za Kaunti* zinazoandikwa kila siku na wasomaji mbalimbali katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Magazeti ni kiungo muhimu cha mawasiliano katika nchi yoyote. Ni muhimu kujua namna urejelezi unavyochangia kufanikisha mawasiliano katika magazeti. Ingawa suala la urejelezi ni kiungo muhimu katika ujenzi wa matini, hadi sasa kuna tafiti chache zinazozamia suala hili hususan katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hili kwa kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* na namna zinavyosaidia kujenga matini na kufanikisha mawasiliano ya kimaana. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) itatumika katika utafiti huu kwa kuangazia mtazamo wa Halliday (1976). Aidha, nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Wilson (2003) na Wilson na Sperber

(2002) itatumika kama nadharia changizi katika kufafanua jinsi wasomaji wanavyofikia maana tambuzi katika matini.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo ya utafiti:

i. Je, aina zipi za urejelezi zinatumiwa katika gazeti la *Taifa Leo?*
ii. Je, urejelezi unatumika vipi katika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo?*
iii. Je, nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Uhusiano zinaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa kutumia urejelezi kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo?*

### 1.4. Malengo ya Utafiti

Utafiti wetu una malengo yafuatayo:

i. Kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo.*
ii. Kubainisha jinsi urejelezi unavyotumika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo.*
iii. Kubainisha iwapo nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Uhusiano zinaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa kutumia urejelezi kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo*.

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu unafanywa kwa sababu urejelezi huchangia katika kuleta mshikamano katika matini. Utafiti huu unakusudia kuonyesha aina mbalimbali za urejelezi na jinsi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini. Ni kweli kuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu mshikamano. Tafiti zilizofanywa na Ogato (2018), Bahaziq (2016), Klimova na Hubackova (2014), Habwe (2012) na Thiga (1997) zilitumia nadharia ya jadi ya mshikamano ya Halliday (1976). Kulingana na utafiti wetu, hakuna utafiti ambao umefanywa unaoonyesha jinsi urejelezi unavyochangia kuleta mshikamano katika matini kwa kutumia nadharia ya kisasa ya Sarufi Amilifu ya Halliday (1985) ambayo inaweka msisitizo katika uamilifu wa maana katika lugha. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) itatumika katika utafiti huu kwa kuangazia mtazamo wa Halliday

(1976). Nadharia ya Sarufi Amilifu itatumiwa katika utafiti huu kwa sababu nadharia hii hufafanua matumizi ya lugha kwa kuzingatia miktadha halisi katika jamii.

Nadharia ya Uhusiano ya Sperber na Wilson (1995,2002, 2004) itatumika katika utafiti huu kama nadharia changizi kwa sababu inaeleza utaratibu wa kuchakata na kufasiri ujumbe katika akili ya kitambuzi ya msikilizaji au msomaji. Nadharia ya Sarufi Amilifu haifafanui jinsi msikilizaji au msomaji hufikia maana tambuzi akilini mwake. Hivyo basi, nadharia hii itatumika kufafanua jinsi msomaji hufikia maana tambuzi katika *Habari za Kaunti*.

Utafiti huu utawawezesha wasomaji kutambua aina mbalimbali za urejelezi zinazochangia kuleta mshikamano. Gazeti la *Taifa Leo* lilichaguliwa kimakusudi kwa sababu gazeti hili huchapishwa katika lugha ya Kiswahili kila siku nchini Kenya. Waandishi mbalimbali wa gazeti la *Taifa Leo* kwa jumla wataweza kunufaika kutokana na ufahamu wa aina mbalimbali za urejelezi kwa sababu wataweza kutumia urejelezi kwa njia inayofaa katika maandishi yao.

Walimu na wanafunzi wa lugha ya Kiswahili pia wataweza kunufaika kutokana na uelewa wa aina mbalimbali za urejelezi zinazochangia katika kuleta mshikamano kwa kuweza kuandika insha ambazo zinaeleweka kwa urahisi kwa wasomaji. Hii ni kwa sababu wakati mwingine kuna mashindano ya uandishi wa insha katika gazeti la *Taifa Leo.*

Wanafunzi wanaodhamiria kufanya kazi za uhariri wa magazeti yanayotumia lugha ya Kiswahili watanufaika kutokana na utafiti huu kwa kuweza kutumia aina mbalimbali za urejelezi kwa njia inayoleta mshikamano. Watafiti wa Isimu katika lugha ya Kiswahili watakaoshughulikia aina za urejelezi katika matini zao watanufaika kutokana na utafiti huu kwa sababu wataweza kutumia utafiti huu kuwa sehemu ya marejeleo ya tafiti zao. Isitoshe, utafiti huu utaleta mchango mkubwa katika kutambua utata katika ufasiri wa aina mbalimbali za urejelezi katika matini.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu utajikita katika kuchunguza urejelezi wa kiendofora, urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha. Aina hizi za urejelezi zitachanganuliwa kimaelezo kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu inayohusishwa na Halliday (1985). Mhimili wa maana matini utatumiwa kutathmini jinsi yale yameandikwa yameshikana pamoja na kuhusiana na kilichoandikwa hapo awali kulingana na muktadha. Mhimili wa maana tambuzi utatumiwa kutathmini jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutumia lugha kueleza mambo yanayotendeka katika ulimwengu halisi na tajriba zao kwa kutumia sentensi au aya zenye mshikamano.

Mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano inayohusishwa na Carson (2002), Wilson na Sperber (2002) na Wilson (2003) itatumika kutathmini jinsi msomaji anavyofikia maana tambuzi katika *Habari za Kaunti*. Kanuni tambuzi itatumiwa kutathmini jinsi msomaji au mwandishi huchagua sifa chache miongoni mwa sifa nyingi ili kurejelea kifaa au dhana kulingana na muktadha wa matini. Mhimili wa kanuni mawasiliano utatumika kutathmini jinsi msomaji huchakata na kufasiri ujumbe kwa kutegemea kiwango cha uhusiano ili kupata maana tambuzi iliyokusudiwa na mwandishi.

Nakala za *Habari za Kaunti* zilizoandikwa kati ya mwezi wa Juni hadi Julai mwaka wa 2020 zitatumika tu katika utafiti. Hata hivyo, utafiti huu hautachunguza urejelezi nje (eksofora) kwa sababu ufasiri wake unategemea muktadha nje ya matini. Urejelezi nje hauunganishi vipashio viwili au zaidi katika sentensi ila humpeleka msomaji nje ya matini ili kuufasiri. Isitoshe, urejelezi huu hauchangii katika kuleta mshikamano katika matini.

Vilevile, utafiti huu utachunguza michango ya matumizi ya viunganishi, udondoshaji, ubadilishaji kiurejelezi katika sentensi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Vipashio hivi vitachunguzwa kwa sababu vinachangia katika kuleta mshikamano katika matini.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii

Katika sehemu hii, tutajikita katika yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya Sarufi Amilifu, nadharia ya Uhusiano, yaliyoandikwa kuhusu mshikamano na yaliyoandikwa kuhusu urejelezi.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Sarufi Amilifu

Wakarindi (2010) anaeleza kuwa lugha huwa na jukumu la kuleta maana. Katika maelezo yake, lugha ina maana tambuzi, maana matini na maana husishi. Maana hizi hubainika katika kishazi. Hii ina maana kuwa kishazi kama ujumbe ina uwiano na maana tambuzi ilhali kishazi kama upokezano ina uwiano na maana husishi. Kishazi kama uwakilishi ina uwiano na maana matini. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu inaeleza kuhusu nadharia ya Sarufi Amilifu na hivyo kutusaidia kuelewa nadharia ambayo tutatumia katika utafiti huu.

Nthenya (2009) anaeleza kuwa kazi ya lugha ni kuleta maana katika matini. Kulingana naye, kila lugha huwa na maana tambuzi, maana husishi na maana matini. Maana tambuzi huhusu yale yanayotendeka katika ulimwengu wa mzungumzaji, maana husishi huhusu jukumu la lugha kuwafanya watu washirikiane pamoja katika mawasiliano. Maana matini huhusu namna ya kupanga mawazo kwa njia iliyo na mshikamano. Utafiti huu utatufaa katika kuelewa nadharia ya Sarufi Amilifu.

Banks (2002) anafafanua kuwa wakati wa kuchunguza matini kwa kutumia nadharia ya Sarufi Amilifu, dhana kama vile mada, uhusiano na mtindo ni muhimu. Katika maelezo yake, dhana hizi zina uwiano na maana tambuzi, maana husishi na maana matini mtawalia. Maelezo haya ni muhimu kwa sababu yatatusaidia kuelewa mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu.

Eggins n.w (2004) wanaeleza kuwa Sarufi Amilifu hufafanua namna watu wanavyotumia lugha kutangamana katika jamii na jinsi lugha inavyopangwa wakati wa mazungumzo ili kuleta maana mbalimbali zinazokusudiwa. Lugha hutumiwa katika jamii kulingana na muktadha. Vilevile, wanaeleza kuwa wazungumzaji wanaposhiriki katika mazungumzo hutumia lugha ili kueleza ulimwengu wanamoishi na tajriba zao za kibinafsi. Isitoshe, wanapanga maneno wanayotumia ili waelewane wanapozungumza. Maelezo wanayoyatoa ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatachangia katika kuelewa mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu.

Halliday na Mathiessen (2004) wanaeleza kuwa lugha ina uamilifu wa kuleta maana kulingana miktadha mbalimbali katika jamii. Kulingana na wao, maana katika lugha

hutambuliwa katika kishazi. Kishazi kinabeba maana tambuzi, maana husishi na maana matini. Maana hizi huingiliana na kuchangiana katika kufanikisha mawasiliano. Maelezo wanayoyatoa ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatachangia katika uelewa wa nadharia ya Sarufi Amilifu.

Butt n.w (1995) wanafafanua kuwa nadharia ya Sarufi Amilifu inashughulikia matumizi ya lugha kulingana na miktadha mbalimbali ya jamii. Washiriki katika mazungumzo huchagua na kupanga maneno wanayotumia ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kulingana na mada, uhusiano na mtindo. Maelezo haya yatatusaidia katika kuelewa mihimili ya nadharia ya Sarufi Amilifu.

Gerot n.w (1995) wanaeleza kuwa Sarufi Amilifu inaeleza jinsi lugha inavyotumiwa kuleta maana mbalimbali kulingana miktadha halisi katika jamii. Nadharia hii huonyesha uhusiano uliopo baina ya muktadha na matini. Vilevile, wao wanaeleza kuwa lugha hutumika kulingana na mada, uhusiano na mtindo. Maelezo haya yatatufaa katika kuelewa maana mbalimbali zinazojitokeza katika matini.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Uhusiano

Atieno, B.A (2018) anafafanua kuwa nadharia ya uhusiano inaweza kutumika katika ufasiri wa lakabu. Kulingana naye, ili msomaji afasiri maana ya lakabu, mazingira ya kiutambuzi wanayoshiriki msemaji na msikilizaji ni muhimu. Vile vile, anaeleza kuwa muktadha humsaidia msomaji kuunda chukulizi kuhusu tamko wazi na tamko isiyo wazi. Ufafanuzi huu utatufaa katika utafiti wetu katika uelewa wa umuhimu wa mazingira ya kiutambuzi katika ufasiri wa maana katika matini.

Gaichu, M.N. (2016) anafafanua kuwa tamko wazi na tamko isiyo wazi inaweza kufasiriwa kwa kutumia mikakati ya upanuaji wa tamko husika. Katika upanuzi wa maana ya tamko, kamusi ya ubongo wa msikilizaji itakuza chukulizi zinazomsaidia kupata maana iliyokusudiwa na msemaji. Chukulizi zilizo na maana zitachukuliwa ilhali chukulizi ambazo hazina maana zitaachwa. Maelezo haya yatatufaa katika utafiti huu katika kuelewa kanuni tambuzi ya nadharia ya Uhusiano ambayo tumetumia katika utafiti huu.

Toews, N. (2016) anafafanua kuwa nadharia ya Uhusiano ni nadharia ya kitambuzi ya mawasiliano ambayo inaweza kutumika kufasiri maana ya eksiplikecha na implikecha.

Isitoshe, anaeleza kuwa ili mawasiliano yafanikiwe, msemaji anafaa kutoa vidokezo vinavyovuta makini ya msikilizaji kwa jambo muhimu linalozungumziwa. Maelezo haya yatatufaa katika kutambua mihimili ya nadharia ya Uhusiano.

Ojode, J.O. (2014) anafafanua kuwa nadharia ya Uhusiano ni muhimu katika kutambua maana iliyokusudiwa na mwimbaji katika nyimbo zake. Kulingana naye, msikilizaji wa nyimbo anaweza kufikia maana zilizokusudiwa na mwimbaji kupitia kwa kutumia vidokezi, tajriba ya msikilizaji na muktadha. Maelezo ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatachangia katika uelewa wa maana ya kauli mbalimbali zilizotumika katika *Habari za Kaunti*.

Koech, S.K. (2013) anaeleza kuwa nadharia ya uhusiano inaweza kutumiwa kueleza maana zinazokusudiwa na msemaji kwa msikilizaji wake. Kulingana naye, maana ya msemaji hufasiriwa kulingana na muktadha. Isitoshe, msemaji anaweza kufasiri maana ya maneno yaliyobanwa na yaliyopanuliwa kimaana kwa kutumia nadharia ya Uhusiano. Maelezo haya yatatufaa katika kubainisha jinsi msomaji anavyoweza kufasiri maana ya maneno yaliyobanwa au yaliyopanuliwa kimaana katika *Habari za Kaunti.*

Aduda, K. (2011) anaeleza kuwa nadharia ya Uhusiano inaweza kutumika kufasiri maana ya tamko. Kwake, mikakati ya ubanaji na upanuzi wa maana hurahisisha ufasiri wa maana iliyokusudiwa na msemaji. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu katika uelewa wa jinsi mikakati ya ubanaji na upanuaji inaweza kutumika kufasiri maana iliyokusudiwa na mwandishi katika *Habari za Kaunti*.

Okeyo (2011) anaeleza kuwa hatua za uzulishaji zinazotokea akilini mwa msikilizaji hufanikisha mawasiliano. Kulingana naye, ili msikilizaji afasiri ujumbe katika tamko wazi au tamko fiche, ni lazima afasiri ujumbe kwa kutumia mikakati ya ukadiriaji, ubanaji na upanuzi. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatachangia katika kutambua mikakati ambayo msomaji anaweza kutumia ili kufikia maana tambuzi katika *Habari za Kaunti*.

Deirdre Wilson na Dan Sperber (2002) wanaeleza kuwa uhusiano ni muhimu katika ufahamu wa binadamu kwa sababu binadamu husikiliza kwa makini tamko ambalo ni muhimu na lina uhusiano. Tamko muhimu huibua matarajio ya msikilizaji husika kupitia

matumizi ya vidokezi. Maelezo haya yatatufaa katika kuelewa jinsi msomaji wa *Habari za Kaunti* hufikia maana tambuzi.

Blutner (1999) anaeleza kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya nadharia ya Pragmatiki leksika na nadharia ya Uhusiano kwa sababu nadharia hizi mbili huchunguza jinsi maana ya kiisimu ya neno hubadilika kutegemea muktadha wa matumizi. Isitoshe, mikakati ya ufasiri wa ujumbe kama vile ubanaji, upanuaji na ukadiriaji hutumika katika nadharia hizi mbili. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa kuchangia uelewa wa mikakati ya ufasiri wa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa *Habari za Kaunti* kwa usahihi.

Halliday (1999) anafafanua kuwa muktadha huweza kubadilisha maana ya neno. Kulingana naye, kuna aina tatu za miktadha: muktadha wa kitamaduni, muktadha wa kihali na muktadha wa kimatini. Muktadha wa kitamaduni na muktadha wa kihali huhusiana na masuala nje ya lugha. Muktadha wa kimatini nao unachunguza vipengele ndani ya lugha. Maelezo haya yatatufaa katika kubainisha jinsi msomaji anavyoweza kutumia muktadha katika nadharia ya Uhusiano kung’amua maana iliyokusudiwa na mwandishi wa *Habari za Kaunti*.

Leech (1983) anaeleza kuwa muktadha ni muhimu kwa sababu inamwezesha msikilizaji kufasiri maana iliyokusudiwa na msemaji. Kulingana naye, muktadha ni ufahamu unaofanana baina ya msemaji na msikilizaji. Ufahamu unaofanana humsaidia msikilizaji afahamu na afasiri tamko kwa njia inayofaa. Maelezo haya ni muhimu katika kuelewa jinsi muktadha huchangia katika ufasiri wa maana katika nadharia ya Uhusiano ambayo tumetumia katika utafiti huu.

Grice (1963) anafafanua kuwa watu wanapozungumza hushirikiana wakiongozwa na utaratibu wa ushirikiano. Bila utaratibu huu basi mazungumzo yanavurugwa. Kulingana naye, utaratibu wa uhusiano una kanuni nne: kanuni ya idadi, ukweli, namna na uhusiano. Maelezo haya yatatufaa katika kuelewa jinsi kiwango cha uhusiano huchangia katika kuchuja vidokezi katika tamko.

### 1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mshikamano

Afzaal n.w. (2019) wanafafanua kuwa mshikamano ni muhimu katika uandishi wa gazeti. Ijapokuwa utafiti huu ulitumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ni muhimu kwetu

kwa kuonyesha jinsi urejelezi unavyoweza kutumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Ogato (2018) anaeleza kuwa tungo zilizo na mshikamano zinaeleweka kwa urahisi. Kwa kuwa tunachunguza jinsi urejelezi unavyotumika kuleta mshikamano, maelezo anayoyatoa ni muhimu katika utafiti huu. Utafiti huu utatusaidia kutambua aina mbalimbali za urejelezi katika *Habari za Kaunti*.  Kazi hii pia ni muhimu kwetu kwa sababu itatusaidia kuelewa nadharia ya Sarufi Amilifu.

Malah n.w (2017) wanaeleza kuwa mshikamano ni muhimu katika kuleta muwala katika matini. Utafiti huu utatufaa kwa kutufafanulia nadharia ya Sarufi Amilifu na dhana ya mshikamano ambayo tunashughulikia katika utafiti huu. Tofauti kati ya utafiti huu na utafiti wetu ni kuwa utafiti huu umejikita katika tahariri ilhali utafiti wetu umejikita katika Habari *za Kaunti*.

Bahaziq (2016) anaeleza kuwa katika uandishi wa tungo, mshikamano ni muhimu. Utafiti huu utatufaa katika kutambua aina mbalimbali za urejelezi zinazotumika katika *Habari za Kaunti*. Isitoshe, utafiti huu utabainisha umuhimu wa kutumia vijenzi vya mshikamano ili kuleta uandishi fanifu.

Okoth (2015) anafafanua kuwa viwakilishi vinavyotumiwa wakati wa kusimulia ngano vinaweza kuleta utata wa kimaana. Katika maelezo yake, msikilizaji wa ngano asipoelewa nomino zinazorejelewa na viwakilishi, hataweza kufuatilia mtiririko wa ngano. Ijapokuwa utafiti huu umetumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu utatufaa kwa kutambua aina mbalimbali za urejelezi zinazochangia kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Klimova na Hubackova (2014) wanafafanua kuwa mshikamano ni muhimu katika uandishi wa matini. Kulingana nao, mshikamano huchangia katika kuleta muwala katika matini. Utafiti huu ulijikita katika ikisiri ilhali utafiti wetu utajikita katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu utatufaa kwa kutambua aina mbalimbali za urejelezi katika *Habari za Kaunti*.

Habwe (2012) anaeleza kuwa mshikamano haujitokezi tu baina ya sentensi bali unaweza kujitokeza katika sentensi moja. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu

yanafafanua dhana ya mshikamano ambayo tunashughulikia. Hata hivyo, utafiti huu ulitumia nadharia ya jadi ya Halliday na Hasan (1976).

Hameed (2008) anafafanua kuwa mshikamano ni muhimu katika uandishi wa gazeti. Kulingana naye, mshikamano huchangia katika kuleta muwala katika matini. Ingawa utafiti huu umetumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ni muhimu kwa sababu unachunguza dhana ya mshikamano ambayo tunashughulikia katika utafiti huu.

Nyarige (2002) anaeleza kuwa mshikamano ni muhimu katika kuleta muwala katika tungo. Utafiti huu, kama utafiti wetu, umetumia nadharia ya Sarufi Amilifu. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika tungo za wanafunzi ilhali utafiti wetu utajikita katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu utatufaa katika kuelewa nadharia ya Sarufi Amilifu.

Habwe (1998) anaeleza kuwa mshikamano huchangia kuleta muwala katika hotuba za wanasiasa. Katika maelezo yake, hotuba zilizo na mshikamano huwavutia wasikilizaji. Ijapokuwa alitumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu utatufaa kwa sababu utachangia katika kuelewa dhana ya mshikamano tunayoshughulikia katika utafiti huu.

Thiga (1997) anaeleza kuwa mshikamano ni muhimu katika kuleta muwala katika tungo za wanafunzi. Kulingana naye, tungo zilizo na mshikamano zinaeleweka kwa urahisi. Utafiti huu ulijikita katika tungo za wanafunzi ilhali utafiti wetu utajikita katika gazeti la *Taifa Leo*. Ingawa alitumia nadharia tofauti na utafiti wetu, maelezo haya ni muhimu kwa sababu yanaeleza dhana ya mshikamano ambayo tunashughulikia katika utafiti huu.

Thompson (1996) anafafanua kuwa mshikamano unaweza kutumiwa kutathmini kama matini ina muwala au inakosa muwala. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatachangia katika kubainisha jinsi urejelezi unavyoweza kutumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Karanja (1993) anaeleza kuwa mshikamano ni muhimu katika ufasiri wa maana katika matini. Utafiti huu ulijikita katika matini za vipindi vya mjadala kwenye runinga ilhali utafiti wetu utajikita katika *Habari za Kaunti.* Utafiti huu utatufaa katika kuelewa dhana ya mshikamano ambayo tunachunguza katika utafiti huu.

Beaugrande na Dressler (1981), Fowler (1991) na Alba-Juenz (2009) wanakubaliana kuwa matini ina sifa bainifu. Mshikamano ni miongoni mwa sifa bainifu za matini. Sifa zingine za matini ni uwazi wa makusudio, muwala, maudhui, ukubalifu, muktadha na mwingiliano wa kimatini. Kulingana nao, sifa hizi huchangia kuonyesha mahusiano ya kimaana katika matini. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yanaeleza maana ya mshikamano.

Halliday na Hasan (1976) wanafafanua kuwa mshikamano ni muhimu katika uelewa wa matini. Wao wanaeleza kuwa ili matini ieleweke kwa wasomaji, ni lazima iwe na mshikamano. Maelezo haya yatatufaa katika utafiti huu kwa sababu yanaeleza dhana ya mshikamano ambayo ni muhimu katika utafiti huu.

### 1.7.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Urejelezi

Sukthanker n.w (2020) wanafafanua aina mbalimbali za urejelezi. Ufafanuzi wao utatupatia mwelekeo muhimu kuhusu namna ya kufasiri maana ya viwakilishi vinavyorejelea nomino moja au zaidi katika matini. Japo utafiti huu umejikita matumizi ya urejelezi katika tafsiri, utafiti huu utatufaa kwa kutambua aina za urejelezi katika *Habari za Kaunti*.

Habarkah (2019) anafafanua kuwa urejelezi huchangia katika kuleta mshikamano katika matini. Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa sababu utatusaidia kutambua aina mbalimbali za urejelezi na anafora katika *Habari za Kaunti*. Tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ulikusanya data zake kutoka kusoma barua.

Khofidoh (2017) anaeleza kuwa urejelezi ni muhimu katika kuleta mshikamano katika matini. Kulingana naye, matini iliyo na mshikamano hueleweka kwa urahisi. Ingawa utafiti huu ulitumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ni muhimu kwetu kwa kuwa unafafanua vipengele tunavyochunguza katika utafiti huu.

Saddimbah (2011) anaeleza kuwa vijenzi mbalimbali vya mshikamano huchangia kuleta muwala katika matini. Ingawa utafiti huu ulitumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu utachangia katika kuonyesha jinsi urejelezi unavyochangia kuleta mshikamano katika matini.

Schubert (2008) anasema kuwa urejelezi wa kianafora ni muhimu katika kutambua kitu au jambo linalorejelewa katika matini. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatasaidia katika kutambua kitajwa kilicho nyuma ya sentensi moja au zaidi kwa kutumia anafora. Maelezo ya Schubert yatasaidia katika kutambua aina mbalimbali za urejelezi katika *Habari za Kaunti.*

Mulila (2005) anafafanua jinsi muwala na mshikamano zinavyotumika uandishi wa riwaya. Katika maelezo yake, mshikamano ni muhimu katika kuleta muwala. Ijapokuwa utafiti huu umetumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ni wa manufaa kwetu kwa sababu utachangia katika kufafanua dhana ya mshikamano.

Sugiharto (2004) anafafanua kuhusu umuhimu kuelewa dhana za urejelezi katika matini. Kulingana naye, uelewa wa dhana hizi zitachangia katika kurahisisha ufunzaji wa dhana hizi. Walimu wa semantiki wanafaa kuelewa dhana hizi ili kuweza kuwafunza wanafunzi wao kwa njia inayofaa. Ingawa utafiti huu unatumia nadharia tofauti na utafiti wetu, utafiti huu utatufaa katika kueleza umuhimu wa kutumia mshikamano katika Habari *za Kaunti*.

Njue (1989) anaeleza kuwa mshikamano ni muhimu katika utambaji wa hadithi. Kwake, mtambaji wa hadithi anafaa kuwa na uwezo kusimulia hadithi kwa njia inayoeleweka kwa urahisi kwa wasikilizaji. Vilevile, anasema kuwa mshikamano humwezesha msikilizaji kufuatilia matukio katika hadithi. Maelezo haya yatatufaa katika kuelewa dhana ya mshikamano tunayoshughulikia katika utafiti huu.

Brown na Yule (1983), Halliday na Hasan (1994), and Lyons (1995) na Mathews (1997) wanaeleza kuhusu umuhimu wa kutumia urejelezi katika matini. Kulingana nao, vitu vinavyopatikana katika ulimwengu vinaweza kuelezwa kwa kutumia urejelezi. Schriffin na wenzake, (2008) wanasema kuwa kitajwa kinaweza kubainishwa katika matini kupitia urejelezi. Yule (1996) anaeleza kuwa kupitia kwa urejelezi msikilizaji au msomaji huweza kubainisha kitu, mtu au jambo katika matini kupitia matumizi ya maumbo ya kiisimu. Eggins (1994) naye anaeleza kuwa msomaji anaweza kutumia urejelezi kufuatilia matendo ya washiriki katika matini. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yatachangia katika kutambua aina mbalimbali za urejelezi na sababu za kutumika katika *Habari za Kaunti.*

### 1.8 Msingi wa Kinadharia

Katika utafiti huu, tutatumia nadharia mbili kuchanganua data. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985,1994,1999), Halliday na Mathiessen (2004) na Matthiessen (2013) itatumika kwa kuangazia mtazamo wa Halliday (1976). Nadharia hii itatumika kutathmini iwapo mhimili wa maana matini unaweza kutumiwa kiurejelezi katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Aidha, Nadharia ya Uhusiano iliyoendelezwa na Carson (2002), Wilson na Sperber (2002) na Wilson (2003), itatumika katika utafiti huu kutathmini iwapo mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano inaweza kutumiwa kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

#### 1.8.1 Nadharia ya Sarufi Amilifu

Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) itatumika katika utafiti huu kuchunguza matumizi ya urejelezi katika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo* kwa kuangazia mtazamo wa Halliday (1976). Dik (1978) ndiye mwasisi wa nadharia hii. Nadharia ya Sarufi Amilifu ilitokana na madai ya nadharia ya Sarufi Zalishi kuwa lugha ni umilisi wa mtu binafsi. Kinyume na nadharia ya Sarufi zalishi, nadharia hii inaeleza kuwa lugha ni mali ya jamii. Lugha inafaa kuchunguzwa kwa kuzingatia miktadha halisi ya kijamii. Kulingana na nadharia hii, msemaji anafaa kuelewa namna watu wanavyotumia lugha katika jamii kulingana na muktadha.

Nadharia hii huchunguza jinsi lugha inavyopangwa ili kuleta maana mbalimbali zinazokusudiwa na msemaji. Maneno yanaweza kupangwa kwa njia mbalimbali ili kuleta maana mbalimbali katika matini. Sarufi Amilifu pia inatupatia vifaa vya kufafanua jinsi lugha inavyotumika katika miktadha tofauti ya maisha halisi na vya kuelewa kwa nini matini iko jinsi ilivyo. Vifaa hivi ni vitengo vitatu vya lugha: semantiki, sintaksia na pragmatiki.

Semantiki huchunguza maana ya maneno katika sentensi ilhali sintaksia huhusika na mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kuzingatia kanuni za kisarufi ili kuleta maana inayokubalika na jamii husika. Pragmatiki inajikita katika umilisi wa mawasiliano. Isitoshe, pragmatiki inachunguza vikwazo vya kijamii wakati wa kutumia lugha, athari za kijamii za matumizi ya lugha na uwezo wa mzungumzaji kufanya uamuzi katika akili yake

kuhusu namna ya kuzungumza. Kwa hivyo, nadharia hii inafafanua jinsi vitengo vya lugha hufanya kazi pamoja kama mfumo mkubwa ili kuunda maana katika matini.

Katika nadharia ya Sarufi Amilifu dhana kama vile mada, utaratibu wa uhusiano na mtindo hutumika. Mambo haya matatu huathiri sajili. Hii inaonyesha kuwa sajili hubadilika kutegemea jinsi mwandishi au msomaji anavyotumia lugha wala sio mwandishi au msomaji anayetumia lugha. Mada ni uwanja unaozungumziwa au unaoandikwa kuhusu. Utaratibu wa uhusiano ni uhusiano baina ya msemaji na msikilizaji au mwandishi na msomaji. Mtindo ni njia ya mawasiliano iliyotumika kama vile lugha iliyoandikwa au mazungumzo. Kwa mfano: Waandishi mbalimbali katika *Habari za Kaunti* hutumia lugha kwa namna mbalimbali wakizungumzia mada mbalimbali, lugha inayoonyesha uhusiano uliopo baina ya mwandishi na msomaji kwa kutumia lugha iliyoandikwa.

Sarufi Amilifu inampa msemaji uwezo wa kufanya uamuzi katika akili yake kuhusu namna ya kuzungumza na kuelewa sababu ya kuzungumza namna anavyozungumza. Msemaji hufanya uamuzi kuhusu mpangilio wa maneno anayoyasema ili kuwasilisha ujumbe anaokusudia kuwasilisha. Ujumbe huo hujitokeza katika sentensi. Kishazi ni kipashio cha kimsingi katika uchanganuzi wa matini za kisarufi katika Sarufi Amilifu. Kishazi kinachukuliwa kama sentensi sahili inayobeba ujumbe kamili. Kishazi kinaelezwa kwa kuzingatia mitazamo mitatu: kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano na kishazi kama uwakilisho.

Kishazi kama ujumbe huhusiana na uamilifu wa kishazi wa kubeba maudhui. Mada inayochaguliwa na msemaji kutanguliza usemi wake katika kishazi ni maudhui. Kimsingi, maudhui hujitokeza mwanzoni mwa kishazi ili kuunganisha ujumbe katika matini. Msemaji anaweza kuchagua kirai nomino, kirai kivumishi au kirai kihusishi kuwa sehemu ya maudhui katika ujumbe. Kwa mfano, katika kishazi, *'Kitabu kile kimeraruka'*, msemaji amechagua kirai nomino kuwa maudhui ya kishazi katika ujumbe. Katika kishazi hiki, kila kipengele kina uamilifu wake kwa mfano, *'Kitabu kile'* ni maudhui ilhali *'kimeraruka'* ni kijalizo.

Kishazi kama upokezano kina maana kuwa kishazi kimepangwa ili kuleta ile hali ya kutagusana baina ya msemaji na msikilizaji. Msemaji humhusisha msikilizaji wake kwa kumtaka kujibu swali au kumpa taarifa fulani. Hivyo basi, kishazi kama upokezano ni ile

hali ya kishazi kuchukua muundo wa swali, amri au taarifa. Kwa mfano, katika kishazi *'Mwanafunzi amesoma riwaya sana',* msikilizaji anatakiwa kuitikia kwa sababu kishazi hiki kina muundo wa taarifa. Msikilizaji anaweza kumjibu msemaji, '*sawa'.* Kila kipengele katika kishazi hiki kina uamilifu wake kwa mfano, mwanafunzi ni kiima, amesoma ni kiarifu, riwaya ni shamirisho na sana ni chagizo.

Kishazi kama uwakilisho huhusiana na kutumia kishazi kujenga picha kwenye akili ya binadamu kati ya mambo yanayoendelea ulimwenguni na katika akili yake. Katika mtazamo huu, kishazi kina mfanyiko (kitu au jambo linaloendelea), wahusika katika mfanyiko huo (anayesababisha mfanyiko huo) na mazingira (mahali au namna) ambamo mfanyiko huo umefanyika. Kishazi kama uwakilisho huwa na vitendo ambavyo ni vya kiakili au halisi. Kwa mfano:

*(1) Mchezaji anacheza.*

*(2) Yeye anahisi njaa.*

Katika mfano (1), kishazi kina kitendo halisi ilhali kishazi cha pili kina kitendo cha kiakili. Kila neno katika vishazi hivi lina uamilifu wake kwa mfano, katika kishazi cha kwanza, mchezaji ni mtendaji na amecheza ni mfanyiko yakinifu (jambo linafanyika kwa mtu fulani). Hapa, kishazi kimetumika kujenga picha ya mambo yanayotendeka katika ulimwengu halisi wa msemaji. Katika mfano (2), anahisi ni mfanyiko wa kiakili na njaa ni mhisiwa. Katika mfano huu, kishazi kimetumika kujenga picha katika akili ya msemaji. Kishazi kama uwakilishi inaelekeza jinsi msemaji anavyopanga maneno ili kuwasilisha ujumbe kwa ufasaha. Kishazi pia kinaelezwa kuwa kinabeba maana tatu:

#### 1.8.1.1 Maana Tambuzi

Maana tambuzi ni uwezo wa mzungumzaji kuelewa mambo kupitia kwa kutumia lugha kueleza mambo yanayotendeka katika ulimwengu wa kawaida na katika fikra zake. Msomaji hufikia maana tambuzi kupitia kwa kuhusisha maana halisi ya neno na dhana mbalimbali kulingana na muktadha wa matumizi. Maana tambuzi huchangia katika kuleta mshikamano katika matini kupitia kwa kuhusisha maana ya kiisimu na maana ya msemaji. Maana ya kiisimu hufasiriwa moja kwa moja katika matini lakini maana ya msemaji ni kile anachomaanisha mwandishi au mzungumzaji wakati anapotamka au anapoandika neno fulani. Msomaji huchagua maana inayohusishwa na dhana inayorejelewa katika matini

kulingana na muktadha wa kimatumizi. Katika mhimili wa maana tambuzi, lugha hutumiwa kwa namna ya kipekee kurejelea dhana mbalimbali.  Isitoshe, maana tambuzi hubeba ujumbe katika matini.

Waandishi mbalimbali wa *Habari za Kaunti* hutumia lugha kwa njia ya kunasibisha yanayotendeka katika ulimwengu wao wa kawaida na yanayotendeka katika kaunti zao. Japo maneno yanayotumiwa ni ya kawaida, huonekana kama maneno yenye maana fiche kwa watu ambao hawaelewi lugha hii. Kwa mfano, viwakilishi vinaweza kutumika badala ya nomino ambayo ilikuwa imetajwa au itakayotajwa katika matini. Msomaji ni lazima afasiri maneno hayo kwa kutegemea muktadha wa mazungumzo. Maana inayobebwa katika sentensi au aya inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti kulingana na muktadha. Kwa hivyo katika maana tambuzi, msomaji anaweza kufahamu maana iliyokusudiwa katika matini kupitia kwa kuhusisha maana halisi ya neno na dhana inayowasilishwa na neno hilo kwa kuzingatia muktadha. Kwa mfano:

> *(1) Wazee kutoka jamii ya Waswahili walikutana jana. Wao walikutana mjini Mombasa kusuluhisha migogoro.*

Katika mfano (1), neno *wazee* linalorejelewa na kiwakilishi nafsi huru *wao* limetumika kwa maana tambuzi. Kulingana na TUKI (2014), neno wazee lina maana nyingi. Kwanza, neno wazee lina maana ya watu walioishi miaka mingi. Pili, wazee ni watu wanaoheshimiwa kwa sababu ya vyeo vyao kazini au mali waliyonayo. Tatu, wazee ni jina la heshima kwa wanaume. Nne, wazee ni wazazi, hasa akina baba. Katika muktadha huu, neno wazee lina maana ya dhana ya watu walioishi miaka mingi wala sio watu wanaoheshimiwa kwa ajili ya vyeo vyao kazini au mali waliyonayo, jina la heshima kwa wanaume au wazazi, hasa kina baba. Msomaji anaweza kufahamu maana inayorejelewa au inayokusudiwa na mwandishi kupitia kwa kuhusisha neno wazee na dhana ya watu walioishi miaka mingi wala sio dhana ya watu wanaoheshimiwa kwa ajili ya vyeo vyao kazini au mali waliyonayo, jina la heshima kwa wanaume au wazazi, hasa kina baba. Kwa hivyo, maana halisi ya neno huweza kuathiriwa na muktadha wa matumizi.

Maana tambuzi husimba tajriba za kitamaduni na humwezesha mzungumzaji kujenga tajriba zake za kibinafsi. Kupitia kwa kuelewa ulimwengu unaomzunguka, mzungumzaji anaweza kueleza tajriba zake kwa kutumia lugha. Maana tambuzi hubeba ujumbe katika lugha na mzungumzaji anaweza kuelewa ulimwengu anamoishi na kuwasilisha tajriba zake binafsi. Hii inatokana na ukweli kuwa watu hawawezi kuzungumzia mambo yasiyokuwa katika ulimwengu. Kwa mfano, waandishi wa gazeti wanaweza kutumia lugha kueleza tajriba zao za kibinafsi katika ulimwengu wanamoishi.

Wasomaji wa gazeti wanaweza kutoa maoni yao kwa kutumia lugha kueleza yanayotendeka katika Kaunti zao na yanayotendeka katika ulimwengu wao wa kawaida. Wasomaji wanapotoa maoni yao, hupitisha ujumbe kwa wasomaji wengine wa gazeti hilo. Kupitia maana tambuzi, mwandishi wa gazeti anaweza kutumia lugha kueleza kuhusu vitu vinavyopatikana katika ulimwengu anamoishi na mambo yanayotendeka katika ulimwengu huo. Ili ujumbe unaowasilishwa na mwandishi ufasiriwe na wasomaji kwa njia inayofaa, sentensi zinafaa ziwe na mshikamano. Kwa mfano:

*(2) Michezo ni muhimu katika maisha ya binadamu. Michezo hufanya viungo vya mwili kuwa imara*.

Katika mfano (2), neno '*michezo*' limerudiwa katika sentensi ya pili ili kuonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana kati ya sentensi ya kwanza na sentensi ya pili. *Michezo* ni

mfano wa nomino iliyotumiwa kwa maana tambuzi. Neno michezo, lina maana ya kunyoosha viungo vya mwili. Msomaji anaweza kufahamu maana inayokusudiwa na mwandishi kupitia kwa kuhusisha neno michezo na dhana ya kunyoosha viungo vya mwili. Ujumbe unaopatikana katika sentensi ya kwanza una uhusiano wa kimaana na ujumbe unaopatikana katika sentensi ya pili. Ujumbe katika sentensi hizi huhusiana na umuhimu wa michezo au zoezi la kunyoosha viungo vya mwili. Katika sentensi hizi, mwandishi wa gazeti ametumia lugha kueleza mambo yanayotendeka katika ulimwengu anamoishi. Kwa hivyo, ujumbe unaofanana katika sentensi hizi umefanya sentensi hizi kuwa na mshikamano. Lugha pia ina maana husishi.

#### 1.8.1.2 Maana Husishi

Maana husishi huhusika na kutumia lugha kuleta utangamano katika jamii. Hii ina maana kuwa lugha hutumiwa kuleta ushirikiano baina ya watu wanaoshiriki katika mazungumzo. Lugha hutumiwa kuwasiliana, kujitambulisha, kujieleza na kutangamana na watu wengine katika jamii. Washiriki katika mazungumzo hulenga kujieleza na kusikilizwa na wenzao. Kwa mfano, mzungumzaji anaweza kuuliza swali, kurai, kuamrisha au kutoa taarifa. Msikilizaji anatarajiwa kujibu swali, kuitikia au kutenda jambo kwa mzungumzaji. Kwa mfano:

*(3) Je, umezuru mji wa Nakuru?*

*(4) Tafadhali nipe kalamu yako.*

*(5) Ingia haraka!*

*(6) Wauguzi wanagoma.*

Katika sentensi (3), mzungumzaji anauliza swali na anatarajia jibu kutoka kwa msikilizaji na katika sentensi ya (4), mzungumzaji anaomba apewe kalamu. Katika sentensi ya (5), mzungumzaji anamwamrisha msikilizaji aingie mahali fulani haraka na katika sentensi ya (6) mzungumzaji anamtolea msikilizaji taarifa kuhusu mgomo wa wauguzi. Katika sentensi hizi, lugha imetumiwa kuleta ushirikiano baina ya watu wanaoshiriki katika mazungumzo. Ili washiriki katika mazungumzo waweze kufuatilia mkondo wa mazungumzo, sentensi wanazotumia lazima ziwe na mshikamano. Mbali na lugha kuwa na maana husishi, lugha pia ina maana matini.

#### 1.8.1.3 Maana Matini

Maana matini ni jinsi yale tunayosema yameshikana pamoja na kuhusiana na kilichosemwa hapo awali na kulingana na muktadha unaotuzunguka. Maana matini huhusika na kanuni za kisarufi zinazotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa njia inayofaa kulingana na vikwazo vya muktadha wa lugha. Mshikamano huibuka kutokana na vijenzi vya lugha vinavyounganisha maana kutoka sentensi moja hadi nyingine. Maana matini humwezesha mzungumzaji kupanga maneno kwa njia ambayo kila kipengele kinachotumiwa kinategemea kipengele kingine ili kuunda matini. Ili kuelewa maana katika sentensi moja, msomaji ni lazima arejelee sentensi nyingine. Kwa mfano:

*(7) Ali alipita mtihani wa kidato cha nne.*

*(8) Yeye ni mwanafunzi mwerevu.*

Maana katika sentensi ya (8) hutegemea sentensi ya (7). Maana ya neno *Yeye* katika sentensi ya (8) inapatikana katika neno *Ali* katika sentensi ya (7). Kwa hivyo neno *yeye* katika sentensi ya (8) ni anafora kwa sababu linamrejelea *Ali* katika sentensi ya (7). Kutokana na maelezo yanayohusiana na mihimili ya maana, inadhihirika kuwa mihimili hii hutegemeana ili mawasiliano yafanikiwe.

Maana matini pia hudhihirika kupitia matumizi ya viunganishi ambavyo huunganisha maana kutoka sentensi au aya moja hadi sentensi au aya nyingine. Viunganishi huchangia katika kuleta uhusiano wa kimaana na uhusiano wa kisarufi katika matini. Kwa mfano:

*(9) Kirui aliandika insha iliyowavutia wanafunzi wengi shuleni. Hata hivyo, insha hiyo ilikuwa fupi sana.*

Katika mfano (9), kiunganishi *hata hivyo* kimetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana kati ya sentensi ya kwanza na sentensi ya pili. Kiunganishi hiki kimetumika kuonyesha hali kinyume katika uhusiano fulani katika mfuatano wa mambo. Ingawa Kirui aliandika insha iliyowavutia wanafunzi wengi, insha hiyo ilikuwa fupi sana.

Kutokana na mitazamo mitatu ya kishazi, inadhihirika kuwa kishazi kama ujumbe una uwiano, mada, maana tambuzi na Pragmatiki. Vilevile, kishazi kama upokezano ina uwiano na uhusiano, maana husishi na Semantiki. Isitoshe, kishazi kama uwakilishi ina uwiano na mtindo, maana matini na sintaksia.

Mihimili ya maana tambuzi na maana matini itatumiwa kuonyesha jinsi urejelezi unavyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti.* Mhimili wa maana tambuzi utatumiwa kutathmini jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutumia lugha kueleza mambo yanayotendeka katika ulimwengu halisi na tajriba zao kwa kutumia sentensi au aya zenye mshikamano. Vilevile, mhimili wa maana matini utatumiwa kutathmini jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutumia urejelezi kuunganisha maana kutoka sentensi au aya moja hadi nyingine ili kuleta mshikamano katika matini.

### 1.8.2 Nadharia ya Uhusiano

Nadharia ya Uhusiano iliyoendelezwa na Carson (2002), Wilson na Sperber (2002) na Wilson (2003), itatumika katika utafiti huu kama nadharia changizi kuchunguza jinsi wasomaji wanavyofikia maana tambuzi katika *Habari za Kaunti*. Nadharia hii iliasisiwa ili kufidia upungufu wa nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) iliyodai kuwa kila maana iliyomfikia msikilizaji ilikuwa imekusudiwa na msemaji. Madai haya si kweli kwa sababu kuna mambo mengi ambayo msemaji hataki kuwasilisha kwa msikilizaji lakini yanawasilishika.

Nadharia hii ina mihimili miwili mikuu: kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano. Katika kanuni tambuzi, msemaji anahitajika kutoa kauli ambazo zinaeleweka kwa msikilizaji kwa urahisi. Msemaji huchochea akili ya msikilizaji kwa kutumia vidokezi vinavyomfanya msikilizaji kuteka makini yake tu katika ujumbe muhimu na kufahamu ujumbe unaolengwa na msemaji kwa urahisi.

Mhimili wa kanuni mawasiliano unahusiana na kutumia lugha yenye usemi mkubwa wa uhusiano katika kila tendo la mawasiliano. Msemaji anafaa kutumia lugha yenye kiwango kikubwa cha uhusiano. Lugha yenye kiwango kikubwa cha uhusiano ni lugha rahisi kwa msikilizaji kuelewa kinachosemwa na msemaji. Katika mhimili huu, msemaji anafaa kutumia lugha inayomfanya msikilizaji kuchukulia kuwa kauli inayotolewa na msemaji ina umuhimu kwake na inafaa kutiliwa maanani ili kupata ujumbe. Mhimili huu huongoza utaratibu wa kuchakata na kufasiri ujumbe kwa kuzingatia kiwango cha uhusiano. Katika mhimili huu, muktadha ambamo kauli imetolewa huchangia katika ufahamu wa maana katika kauli ya msemaji.

Kulingana na Wilson na Sperber (2002), muktadha ni vitu vyote vilivyo akilini mwa msikilizaji vinavyomsaidia kuelewa au kutafuta viathiri vya utambuzi. Muktadha hujumuisha mambo yote yanayozunguka tamko kama vile: lugha, mazingira, muda na utamaduni. Msikilizaji au msomaji atafasiri maana iliyokusudiwa na msemaji au mwandishi kwa kutumia uhusiano na muktadha.

Kulingana na nadharia hii, msemaji fulani anapotaka kuzungumza na msikilizaji fulani huwa na lengo la kuwasilisha na suala la kuwasilisha. Ili mawasiliano yafanikiwe, msemaji atapima kama jambo atakalosema litakuwa na uhusiano mkubwa na msikilizaji wake. Msemaji anaamua kutumia usemi ambao una uhusiano mkubwa (usemi utakaoeleweka kwa urahisi kwa msikilizaji) kwa sababu mfasiri (msikilizaji) atapata viathiri vya utambuzi kwa haraka. Kama viathiri ni vingi, msikilizaji ataipata maana iliyokusudiwa na msemaji na ikiwa viathiri si vingi, atatupilia mbali ile maana.

Nadharia hii inaeleza kuwa mawasiliano inaweza kutathminiwa kwa kuzingatia athari za kifahamu na athari za jitihada. Usemi utakuwa na usemi mkubwa wa uhusiano wakati ambapo una athari za kiwango cha juu za ufahamu na jitihada za mchakato kuwa katika kiwango cha chini. Hii ina maana kuwa akili ya msikilizaji itapata uhusiano wa usemi kwa urahisi na ataufasiri kwa gharama ya chini.

Wakati wa mazungumzo, msemaji anaweza kusema mambo kwa kutumia eksiplikecha au implikecha. Nadharia ya Uhusiano inaeleza aina mbili za matamko: tamko wazi na tamko fiche. Tamko wazi ni hali ya tamko kutokuwa na maana nyingi ilhali tamko fiche ni hali ya tamko kuwa na utata. Msikilizaji anafaa kufasiri matamko hayo yote.

Katika ufasiri wa tamko wazi au tamko fiche, ujumbe unaweza kufasiriwa kwa kuzingatia mikakati hii: mkakati wa upanuaji, ubanaji na ukadiriaji. Katika mkakati wa upanuaji, maana ya neno hupanuka kwani neno linamaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanisha na kuweza kuongezea maana nyingine. Msomaji anaweza kufasiri maana ya neno kupitia upanuzi wa neno hilo ili kukuza chukulizi zinazofaa kwa dhana ya neno hilo. Kwa mfano:

*Maria ni sungura*.

Ili msomaji apate maana ya sungura, atapanua neno hili akilini mwake ili kuzua chukulizi zifuatazo ya dhana ya sungura:

(i) mjanja
(ii) manyoya
(iii) miguu mine
(iv) masikio marefu
(v) mnyama

Chukulizi hizi zote zinarejelea sungura kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya msomaji na mwandishi. Neno sungura limetumika kwa maana tambuzi kwa sababu linafafanua neno Maria. Chukulizi zilizokuzwa katika matini huchunguzwa kupitia dhana maalum ya kihali (Wilson na Sperber, 2004). Dhana maalum ya kihali huchukuliwa kama kituo cha kufikia sifa mbalimbali za kiensaiklopedia zinazochochewa kwa kuhusisha tamko au neno na muktadha ili msomaji au msikilizaji aweze kufasiri tamko au neno lililotolewa. Shroeder (2005:5) akinukuliwa na Matifari (2016:10) anaeleza kuwa muktadha ni kama kikamusi cha ulimwengu kilicho katika akili ya mzungumzaji na msikilizaji. Kikamusi hicho hujumuisha ufahamu walionao washiriki katika mazungumzo akilini mwao wakati wanapozungumza. Kutokana na maelezo hayo, inadhihirika kuwa muktadha ni muhimu katika ufasiri wa ujumbe.

Msomaji atachagua chukulizi (i) kwa sababu inaleta maana kwa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kwa msomaji kulingana na muktadha wa tamko na ina uhusiano wa kiwango cha juu. Chukulizi (ii) hadi (v) zitaachwa kwa sababu hazileti maana kulingana na muktadha wa tamko na hazina uhusiano wa kiwango cha juu.  Maana ya neno sungura kupitia kwa dhana maalum ya kihali ni mjanja wala sio mnyama, manyoya, miguu minne au masikio marefu. Katika muktadha huu, neno sungura litapata maana mpya ya '*mjanja*'. Neno sungura limetumika kijazanda kumaanisha kuwa Maria, ambaye ni binadamu, ana tabia fulani za sungura (ujanja). Hitimisho hili hufikiwa wakati chukulizi iliyochanganuliwa katika muktadha wa akili inalinganishwa na chukulizi zilizo katika akili ili kuzaa ujumbe mpya.

Ubanaji ni mkakati ambao dhana huchukua vipengele vinavyohusiana na dhana husika. Katika mkakati huu, msikilizaji au msomaji hufasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno. Kwa mfano:

Mwanafunzi yuko darasani.

Katika tamko hii, neno darasani linabeba maana kuu kwa sababu linafafanua mwanafunzi. Ili kupata maana ya darasani, msikilizaji atahitajika kufasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno darasani. Kutokana na ufasiri huu, msikilizaji au msomaji atakuwa na chukulizi zifuatazo katika akili yake:

(i) chumba
(ii) kuna wanafunzi
(iii) kuna mafunzo
(iv) kuna mwalimu au walimu
(v) kuna vitabu

Hii ni kwa sababu ubongoni mwa msikilizaji au msomaji anajua kuwa darasa ni chumba chenye wanafunzi, mafunzo, mwalimu au walimu, vitabu.

Ukadiriaji ni mkakati ambapo msikilizaji anajijazia akilini mwake ili kuelewa maana ya tamko. Muktadha wa kiutambuzi hufanya kazi katika akili ya msikilizaji. Kwa mfano:

*Juma atakuja Jumamosi na kuondoka Jumapili.*

Katika tamko hili, ni lazima kwa msikilizaji kujua kuwa Jumamosi inakuja kabla ya Jumapili. Msikilizaji atajijazia akilini mwake kuwa siku ya Jumamosi inakuja kabla ya Jumamosi.

Isitoshe, katika nadharia hii, matamko yote yanafaa kufasiriwa kwa kufuata utaratibu fulani. Kwa mfano: Iwapo kuna wazungumzaji wawili ambao wanazungumza kwa mfano, Kirui (msemaji) na Katui (msikilizaji), utaratibu huu wa ufasiri utafuatwa:

(i) Kirui ana jambo.
(ii) Kirui anachagua jinsi ya kusema ili Katui apate viathiri (vidokezi) vya utambuzi.
(iii) Kirui atachukulia kuwa usemi wake unafikia kiwango cha juu cha uhusiano.
(iv) Baada ya Kirui kusema jambo, Katui atafasiri kwa kutumia uhusiano wa viathiri vya utambuzi na muktadha wa mazungumzo yao.

(v) Iwapo vichocheo ni vingi, Katui ataipata maana iliyokusudiwa na Kirui. Iwapo vichocheo ni chache, Katui hatapata maana iliyokusudiwa na Kirui.

Imedhihirika kuwa msikilizaji au msomaji hukisia makusudio ya msemaji au mwandishi kwa kutumia urejelezi fulani alio nao katika mazingira tambuzi yake kwa kurejelea vidokezi au chukulizi, muktadha na kiwango cha uhusiano ili kupata ujumbe uliokusudiwa. Kutokana na maelezo kuhusu nadharia hizi mbili, imedhihirika kuwa nadharia ya Sarufi Amilifu haifafanui utaratibu wa kufikia maana tambuzi. Nadharia ya Uhusiano inaweza kutumiwa kuziba pengo hili kwa kuwa inafafanua utaratibu unaofuatwa na msomaji ili kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi kupitia kwa kurejelea muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano.

Vipengele vitakavyochanganuliwa katika nadharia ya Sarufi Amilifu ni: vitengo vya kiisimu vinavyoshirikiana kuunda maana katika matini: semantiki, pragmantiki na sintaksia, mambo yanayoathiri sajili: mada, utaratibu wa uhusiano na mtindo, mitazamo mitatu ya kishazi: kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano na kishazi kama uwakilisho. Vile vile, tutachanganua maana zinazobebwa na kishazi: maana tambuzi, maana husishi na maana matini. Isitoshe, tutachunguza uhusiano uliopo baina ya vipengele hivi katika kujenga matini na kufanikisha mawasiliano.

Katika nadharia ya Uhusiano, tutachanganua vipengele kama vile: mhimili wa kanuni tambuzi, mhimili wa kanuni mawasiliano, mikakati ya kufasiri ujumbe: upanuaji, ubanaji na ukadiriaji. Pia, tutachanganua utaratibu wa kufasiri matamko kwa kurejelea muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano. Isitoshe, tutachanganua jinsi ya kutathmini mawasiliano kwa kutumia athari za ufahamu na athari za jitihada za mchakato.

**1.9 Njia ya Utafiti**

Utafiti huu ni utafiti stahilifu kwa sababu data tutakayopata si za takwimu. Tutasoma tafiti zilizofanywa na wasomi wengine waliotangulia zinazohusiana na mada yetu ya utafiti. Tutatumia kazi za mtandao kupata habari zaidi kuhusu nadharia yetu ya utafiti. Isitoshe, tutasoma vitabu mbalimbali vya wataalamu mbalimbali walioandika kuhusu urejelezi. Gazeti la *Taifa Leo* litanunuliwa kila siku kwa muda wa miezi miwili. *Habari za Kaunti* za mwezi wa Juni, 2020 hadi Julai mwaka wa 2020 zitasomwa ili kupata data ya utafiti wetu.

Data ya kimsingi itakusanywa moja kwa moja kutoka kwa waandishi mbalimbali wa *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo*. Nakala 61 za *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo* zitakusanywa kwa muda wa miezi miwili. Miezi hii miwili itatupa *Habari za Kaunti* zinazoandikwa na waandishi mbalimbali. *Habari za Kaunti* zinachunguzwa kwa sababu habari hizi huandikwa kila siku na waandishi mbalimbali nchini Kenya kwa hivyo tutapata sampuli kubwa ya kutumika katika utafiti huu. Mtafiti atasoma nakala zote 61 kisha kuteua kimakusudi nakala 30 zilizotumia aina mbalimbali za urejelezi kwa sababu nakala hizi huandikwa na waandishi mbalimbali wanaotumia mbinu tofauti za uandishi.

### 1.9.1 Njia za Kuchanganua Data

Baada ya kukusanya data, aina mbalimbali za urejelezi zitagawanywa katika vikundi vitatu: urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha kulingana na vikundi vilivyofafanuliwa na Halliday na Hasan (1976). Vigezo vitakavyoonyesha kuwepo kwa mshikamano katika *Habari za Kaunti* ni matumizi ya viwakilishi na vivumishi kutambua ni wakati gani kauli au sentensi katika matini zinarejelea mtu mwingine au wakati gani zinajirejelea, urudiaji wa maneno, udondoshaji, uunganishaji na ubadilishaji. Mhimili wa maana matini wa Sarufi Amilifu utatumiwa kubainisha jinsi urejelezi ulivyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano itatumika kuchanganua data ili kubainisha jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutoa ujumbe ulio na mshikamano kwa wasomaji wao kupitia urejelezi wa muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano. Vigezo vitakavyoonyesha kuwa msomaji amepata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi ni kurejelea chukulizi zilizo akilini mwake na kuchagua chukulizi zilizo na maana kulingana na muktadha wa tamko na kiwango cha juu cha uhusiano. Data ya utafiti huu itawasilishwa kwa kutumia maelezo na majedwali kuonyesha jinsi aina mbalimbali za urejelezi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini.

### 1.9.2 Hitimisho

Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia, njia za utafiti na muhtasari wa sura.

# SURA YA PILI

# VIPENGELE MUHIMU VYA MSHIKAMANO

## 2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tumeweka msingi utafiti wetu. Katika sura ya pili, tutajadili vipengele muhimu vinavyotumiwa kiurejelezi kuleta mshikamano katika matini. Vipengele vitakavyofafanuliwa katika sehemu hii ni urudiaji wa nomino muhimu, matumizi ya sinonimu na haiponimu, urejelezi wa kiendofora (katafora na anafora), urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha. Vilevile, tutafafanua jinsi uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji zinavyotumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika matini.

## 2.2 Vijenzi vya Mshikamano

Halliday na Hassan (1976) wanaeleza kuwa mshikamano unahusiana na uhusiano wa kisemantiki au uhusiano wa maana zinazopatikana katika matini. Bila kuwepo uhusiano wa kisemantiki, sentensi au matamko yataonekana kuwa hayana uhusiano na hivyo huweza kutotambuliwa kama matini. Mshikamano ni sifa ya matini kufasiriwa kama kitu kimoja bali sio kama sentensi zilizotengana. Sentensi huunganishwa katika matini kupitia matumizi ya vipashio vya kiisimu ili kuonyesha uhusiano wa kimaana katika sentensi hizo. Jambo muhimu katika mshikamano ni uhusiano unaojitokeza wakati wa ufasiri wa maana ya kipashio kimoja katika sentensi moja unategemea sentensi nyingine. Kipengele kimoja katika sentensi kimeshikana na vipengele vingine vya sentensi zinazotangulia au zinazofuata ili kuleta maana. Kwa mfano:

*(10) Maimuna anasoma katika Chuo Kikuu cha Nairobi.*

*(11) Yeye anasomea kazi ya ualimu.*

Sentensi ya (11) inategemea sentensi (10) ili kufasiri maana. Maana ya ‘*yeye’* katika sentensi (11) hueleweka kupitia kurejelea ‘*Maimuna’* katika sentensi ya (10). Uhusiano kati ya sentensi (10) na sentensi (11) unadhihirisha kuwa kuna mshikamano kwa sababu ufasiri wa maana ya kipashio kimoja katika sentensi unategemea sentensi nyingine. Kuna aina mbili za mshikamano: mshikamano wa kileksia na mshikamano wa kisarufi.

### 2.2.1 Mshikamano wa Kileksia

Mshikamano wa kileksia unahusu jinsi maneno yanayohusiana kimaana yanachaguliwa kutumika ili kuunganisha sentensi katika matini. Kuna aina mbili za mshikamano wa kileksia katika matini: urudiaji wa nomino muhimu na matumizi ya maneno yanayohusiana.

#### 2.2.1.1 Urudiaji wa nomino muhimu

Urudiaji ni matumizi ya neno au maneno fulani zaidi ya mara moja katika matini. Urudiaji hutambulika kupitia maneno yaliyotumiwa katika matini. Uamilifu wa urudiaji ni kuonyesha kuwa sehemu ya matini inahusiana na sehemu nyingine kimaana na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(12) Aziza ni mwanafunzi mwenye bidii. Aziza hurauka mapema kusoma.*

Katika mfano (12), neno '*Aziza'* limetumiwa katika sentensi ya kwanza na kurudiwa katika sentensi ya pili. Urudiaji huu unaonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana kati ya sentensi hizi mbili. Uhusiano wa kimaana kati ya sentensi au aya huleta mshikamano wa kileksia katika matini. Vile vile, matumizi ya sinonimu au haiponimu huleta mshikamano wa kileksia.

#### 2.2.1.2 Matumizi ya Sinonimu

Sinonimu ni miundo tofauti ya maneno iliyo na maana sawa. Kwa mfano:

*(13) Oloo anasomea shule ya upili ya Nakuru. Watu wengi wamesomea skuli hiyo.*

Maneno '*shule*' na '*skuli*' katika mfano (13) ni visawe vya dhana moja. Neno '*shule*' na '*skuli*' ni sinonimu. Maneno haya yametumiwa ili kupunguza urudiaji wa neno moja katika matini na kuleta mshikamano katika sentensi.

#### 2.1.2.3 Matumizi ya Haiponimu

Haiponimu ni matumizi ya maneno ambayo maana ya neno moja huwa sehemu ya maana ya neno lingine. Kwa mfano:

*(14) Mnyama alimfukuza mwindaji. Simba huyo alikimbia kwa kasi sana.*

Katika mfano (14), neno '*mnyama*' lina uhusiano wa kihaiponimu na neno '*simba*'. Neno '*simba*' lina maana ndogo (haiponimu) na hupatikana ndani ya neno kuu '*mnyama*'. Neno '*simba*' limetumiwa ili kusaidia kueleweka kwa neno '*mnyama*' na kuonyesha uhusiano

wa kimaana baina ya sentensi. Mbali na matumizi ya mshikamano wa kileksia, mshikamano wa kisarufi unaweza kutumika katika matini.

### 2.2.2 Mshikamano wa Kisarufi

Mshikamano wa kisarufi unahusu matumizi ya vipashio vya kisarufi kuunganisha sentensi katika matini ili kuonyesha uhusiano wa kimaana. Mshikamano wa kisarufi unajumuisha matumizi ya urejelezi, ubadilishaji, uunganishaji na udondoshaji.

#### 2.2.2.1 Urejelezi

Urejelezi ni ufasiri wa kipashio kimoja kisemantiki kupitia kwa kurejelea kipashio kingine katika matini. Urejelezi ni uhusiano wa kimaana. Hii ina maana kuwa ili kuelewa maana katika sentensi au aya moja, ni lazima kwa msomaji kurejelea sentensi iliyotangulia au iliyo mbele katika matini. Urejelezi umegawika katika sehemu mbili kutegemea uamilifu wao katika matini: urejelezi wa kieksofora na urejelezi wa kiendofora.

#### 2.2.2.2 Urejelezi wa Kieksofora

Urejelezi wa kiksofora hutokea pale ambapo ufasiri wa kitajwa hutegemea nje ya muktadha. Msomaji hajifungi katika matini ili kifasiri maana ya kitajwa inayorejelewa. Hiii ina maana kuwa kitajwa kinachorejelewa hakipatikani katika matini ila msomaji atahitajika kufasiri kitajwa hicho nje ya muktadha. Kwa mfano:

*(15) Hiyo ilikuvutia sana*

Katika mfano (15) msemaji anaweza kuwa alikuwa amesema ‘nilikuwa nimesoma riwaya’ au wazungumzaji wanazungumzia aina ya nguo iliyomvutia mmoja wao. Kwa hivyo, katika urejelezi wa kieksofora msemaji na msikilizaji wanachukuliwa kuwa wanaelewa jambo wanalozungumzia nje ya muktadha. Kwa vile urejelezi huu haujifungi katika matini wakati wa kufasiriwa, urejelezi huu hachangii katika kuleta mshikamano katika matini.

#### 2.2.2.3 Urejelezi wa Kiendofora

Urejelezi wa kiendofora ni aina ya urejelezi ambao ufasiri wa maana ya kipashio unajikita katika matini. Mtu au kitu kinachorejelewa kinaweza kutambulika katika matini. Urejelezi huu huchangia katika kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(16) Momanyi na Okello ni marafiki. Wao hutembeleana mara kwa mara.*

Neno '*wao'* katika sentensi ya pili linawarejelea '*Momanyi na Okello'* katika sentensi ya kwanza. Ili kuelewa maana ya '*wao*' katika sentensi ya pili, msomaji atalazimika kurejelea maneno '*Momanyi*' na '*Okello*' katika sentensi ya pili. Kwa hivyo, katika urejelezi wa kiendofora, ili msomaji aelewe sehemu moja ya matini ni lazima aelewe sehemu ya matini iliyotangulia. Kuna aina mbili za urejelezi wa kiendofora: anafora na katafora.

#### 2.2.2.4 Anafora

Anafora ni kipashio cha kiisimu kinachotumiwa kurejelea neno au kitu kilichokuwa kimetajwa katika matini. Neno linatumiwa kurejelea mtu au kitu kilichokuwa kimetajwa awali katika matini. Kwa mfano:

*(17) Kibet ni mchezaji hodari. Yeye huchezea timu ya taifa.*

Neno '*yeye'* linarejelea neno '*Kibet'* lililokuwa limetajwa awali katika sentensi kwa hivyo, ni anafora. Ili kuelewa maana ya '*yeye*' katika sentensi ya pili, msomaji atalazimika kurejelea neno '*Kibet*' katika sentensi ya kwanza. Urejelezi huu ni tofauti na urejelezi wa katafora ambao unategemea neno lililo mbele ya matini ili kufasiriwa.

#### 2.2.2.5 Katafora

Katafora matumizi ya kipashio cha kiisimu kuonyesha neno litakalotajwa katika matini. Katafora ni aina ya urejelezi ambayo hutegemea neno lililo mbele ya matini ili kufasiriwa. Kwa mfano:

*(18) Yeye alikuwa mkulima stadi sana. Juma alishinda tuzo la mkulima bora miaka kumi iliyopita.*

Ili kufasiri maana ya neno *yeye*, msomaji analazimika kusoma hadi mwisho wa sentensi ya pili. Neno '*yeye'* linalojitokeza katika sentensi ya kwanza huashiria neno '*Juma'* ambalo liko katika sentensi ya pili. '*Yeye'* katika sentensi ya kwanza ni katafora kwa sababu linategemea neno '*Juma'* katika sentensi ya pili ili kufasiriwa.

Brown na Yule (1983), Halliday na Hasan (1994), Lyons (1995) na Mathews (1997) wanaeleza kuwa urejelezi hurejelea uhusiano kati ya vipashio vya lugha na vipashio visivyo vya vya kiisimu (ulimwengu). Hii ina maana kuwa urejelezi ni uhusiano baina ya ishara za kiisimu na kile kinachowakilisha katika ulimwengu au ulimwengu wa diskosi au katika matukio fulani ya tamko. Hii inatokana na ukweli kwamba watu hawawezi kurejelea kitu au jambo lisilokuwako katika ulimwengu halisi. Kwa hivyo, urejelezi unajihusisha na

uhusiano uliopo baina ya faridi za kiisimu, maneno, sentensi na ulimwengu halisi usiokuwa wa kiisimu. Kwa mfano:

*(19) Walimu wanaenda shuleni. Wao wanafundisha Hesabati.*

Kiwakilishi nafsi huru '*wao*' katika sentensi ya pili hurejelea nomino '*walimu*' katika sentensi ya kwanza. Kiwakilishi nafsi kiambata 'w*a*' katika neno '*wanafundisha'* katika sentensi ya pili kinarejelea nomino '*walimu*' katika sentensi ya kwanza. Huu ni urejelezi wa kianafora. '*wao*' na 'w*a*' ni vipashio vya kiisimu vinavyorejelea nomino '*walimu*' inayopatikana katika ulimwengu wa diskosi na ulimwengu halisi. Kwa hivyo, urejelezi unaonyesha uhusiano wa kimaana katika sentensi. Mbali na matumizi ya urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi pia huweza kutumika kuleta mshikamano katika matini.

### 2.2.3 Urejelezi wa nafsi

Urejelezi nafsi ni watu wanaoshiriki katika mazungumzo fulani. Urejelezi nafsi hudhihirika kupitia matumizi ya viwakilishi na vimilikishi. Urejelezi huu hutambulisha mzungumzaji (nafsi ya kwanza), mzungumziwa (nafsi ya pili) na mtu mwingine anayezungumziwa (nafsi ya tatu). Jedwali lifuatalo linaonyesha nafsi tatu katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la Urejelezi Nafsi**

| Nafsi | Viwakilishi nafsi huru | | Viwakilishi nafsi viambata | |
|---|---|---|---|---|
| | Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
| I | mimi | sisi | ni | tu |
| II | wewe | nyinyi | u | m |
| III | yeye | wao | a | wa |

Jedwali lifuatalo linaonyesha matumizi ya vimilikishi kulingana na nafsi.

| Nafsi | Vimilikishi | |
|---|---|---|
| | Umoja | Wingi |
| I | -angu | -etu |
| II | -ako | -enu |
| III | -ake | -ao |

Viwakilishi nafsi huwakilisha nomino katika nafsi ya kwanza, ya pili, na ya tatu ilhali vimilikishi huonyesha umilikaji katika sentensi. Viwakilishi hivi huonyesha kitu kinamilikiwa na nani. Halliday na Hasan (1976) wanaeleza kuwa nafsi ya kwanza na nafsi ya pili huwa urejelezi wa kianafora zinapotumika katika usemi halisi. Nafsi ya tatu, inaweza kutumika kurejelea kitu au mtu mwingine ambaye hayuko katika muktadha huo. Kwa mfano:

*(20) Babu alisema, "Mimi nilienda sokoni jana.*

*(21) Waziri aliwaambia wanafunzi, "Nyinyi mtapita mtihani.*

*(22) Yeye alizuru mji wa Nairobi.*

Katika sentensi ya (20) kiwakilishi cha nafsi ya kwanza '*mimi*' kimetumika kianafora kurejelea '*babu'*. '*Babu*' anajirejelea katika sentensi ya (20). Kiwakilishi cha nafsi ya tatu '*nyinyi*' kimetumiwa kuonyesha urejelezi wa kianafora kurejelea '*wanafunzi*' wanaozungumziwa katika sentensi ya (21). Katika sentensi ya (22), kiwakilishi cha nafsi ya tatu '*yeye*' kimetumika kieksofora kurejelea mtu mwingine ambaye hayuko katika muktadha huo. Viwakilishi vimilikishi na vivumishi vimilikishi vinaweza kutumiwa kianafora katika sentensi. Kwa mfano:

*(23) Langu lilivunjwa jana jioni na wezi.*

*(24) Duka langu lilivunjwa jana na wezi.*

Kiwakilishi kimilikishi langu kimetumika kianafora katika sentensi (23) kwa sababu ufasiri wa maana ya kiwakilishi kimilikishi langu unategemea nomino iliyotajwa awali katika matini. Katika mfano (24), kivumishi kimilikishi langu kinarejelea nomino duka lililotajwa awali katika sentensi. Viwakilishi ngeli pia vinaweza kutumika kuleta mshikamano katika matini.

#### 2.2.3.1 Viwakilishi Ngeli

Viwakilishi ngeli ni viambishi maalum vinavyotumika kutambulisha ngeli za nomino mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Viambishi hivi hutambulisha ngeli za nomino katika umoja na wingi. Kwa hivyo, viwakilishi ngeli huonyesha nomino inayozungumziwa iko katika ngeli ipi. Viwakilishi ngeli huweza kutumika kianafora kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(25) Wakulima kutoka Kaunti ya Nairobi wanaomba serikali iwatengenezee barabara.*

*(26) Wakizungumza katika Ukumbi wa KICC, walisema kuwa barabara hiyo ni muhimu sana.*

Katika mfano (25), kiwakilishi ngeli *WA*- katika neno *wakizungumza* kinawarejelea wakulima ambao walikuwa wametajwa katika mfano (26). Ufasiri wa maana ya kiwakilishi ngeli *WA*- katika neno *wakizungumza* katika mfano (26) unategemea nomino *wakulima* iliyokuwa imetajwa katika mfano (25). Vile vile, viwakilishi vimilikishi vinaweza kutumika kuleta mshikamano na muwala katika matini.

### 2.2.3.2 Vimilikishi

Vimilikishi huonyesha nomino inayomilikiwa katika sentensi. Vimilikishi vina msingi wake katika mizizi ya nafsi. Jedwali lifuatalo linaonyesha vimilikishi nafsi:

**Jedwali la vimilikishi Nafsi**

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| I | mimi ( - angu) | sisi (-etu) |
| II | wewe (-ako) | nyinyi ( - enu) |
| III | yeye (-ake) | wao ( -ao) |

Vimilikishi –angu, -etu, -ako, - enu, -ake na –ao hutumika kutegemea ngeli ya nomino inayomilikiwa katika sentensi. Kwa hivyo, viambishi vinavyoambatanishwa kwenye mizizi ya kumiliki hutegemea ngeli ya nomino husika. Kwa mfano:

*(27) Wanafunzi wengi wamepita mtihani. Wako wanaongoza.*

Katika mfano (27), kiwakilishi kimilikishi *wako* katika sentensi ya pili kimetumika kianafora kuwarejelea wanafunzi ambao walikuwa wametajwa katika sentensi ya kwanza. Ili kufasiri maana ya kiwakilishi kimilikishi *wako* katika sentensi ya pili, msomaji atalazimika kurejelea nomino wanafunzi iliyokuwa imetajwa katika sentensi ya kwanza. Aidha, vivumishi vimilikishi huweza kutumika kianafora ili kuleta mshikamano katika matini.

Vivumishi ni maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi cha nomino katika matini. Tofauti kati ya vivumishi na viwakilishi ni kuwa kiwakilishi na nomino haziwezi kutumika katika sentensi moja ilhali vivumishi huweza kutokea katika sentensi

moja pamoja na nomino. Vivumishi vimilikishi na vivumishi viashiria vinaweza kutumika kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini.

Vivumishi vimilikishi vinaonyesha kitu kinachomilikiwa na mtu. Vivumishi vimilikishi huambatanishwa na viambishi mbalimbali mwanzoni kutegemea ngeli ya nomino inayomilikiwa. Kuna mizizi sita ya vivumishi vimilikishi katika lugha ya Kiswahili:

| Nafsi | Vivumishi vimilikishi | |
|---|---|---|
| | Umoja | Wingi |
| I | -angu | -etu |
| II | -ako | -enu |
| III | -ake | -ao |

Vivumishi vimilikishi vinaweza kutumika kianafora ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(28) Maria amechaguliwa kama mwandishi bora mwaka huu.*

*(29) Maandishi yake yanazungumzia masuala ibuka katika jamii.*

Katika mfano huu, kivumishi kimilikishi *yake* katika sentensi (29) kimetumika kumrejelea Maria ambaye alikuwa ametajwa katika sentensi (28). Kivumishi kimilikishi *yake* kimetumika kuleta mshikamano katika matini. Ili msomaji afasiri maana ya kivumishi kimilikishi *yake* katika sentensi (29), itambidi arejelee nomino *Maria* katika sentensi (28). Mbali na urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria unaweza kutumiwa pia kianafora kuleta mshikamano katika matini.

**2.2.4 Urejelezi wa kuashiria/kuonyesha**

Urejelezi wa kuashiria huonyesha umbali wa kitajwa kinachorejelewa kwa mtazamo wa msemaji. Vivumishi viashiria hufanya kazi ya kuonyesha kama kitu au mtu yuko karibu, mbali kidogo (wastani) au mbali sana. Mzizi {h-} hutumika kuashiria vitu vilivyo karibu ilhali mzizi {-le} hutumika kuashiria vitu vilivyo mbali. Viambishi vinavyoambatanishwa na mizizi hiyo hutegemea ngeli ya nomino husika katika sentensi. Vivumishi viashiria vinaweza kurejelea watu, mahali au vitu kianafora katika matini. Kwa mfano:

*(30) Waziri wa Elimu aliwahimiza wanafunzi kufanya bidii masomoni. Waziri huyo alikuwa akizungumza mjini Bomet.*

Katika mfano (30) Kivumishi kiashiria *huyo* katika sentensi ya pili kinamrejelea nomino *Waziri wa Elimu* iliyokuwa imetajwa awali. Ufasiri wa maana ya *Waziri huyo* katika sentensi ya pili unategemea *Waziri wa Elimu* katika sentensi ya kwanza. Kwa hivyo, vivumishi viashiria vinaweza kutumika kuleta mshikamano katika matini.

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa vionyeshi vinaweza kufanya kazi ya vivumishi na viwakilishi. Kimsingi katika Kiswahili vionyeshi vinapotokea kabla ya nomino hufanya kazi ya vibainishi. Matumizi ya viashiria hutegemea ngeli husika.

Matei (2008:38) anaeleza kuwa viwakilishi vionyeshi husimama mahali pa nomino kwa kuashiria. Viwakilishi vionyeshi husaidia kuonyesha nafasi (umbali/ukaribu) ya watu/vitu kutoka kwa msemaji. Kwa mfano:

(31) *Hili ni la mwanafunzi.*

(32) *Hicho ni cha mtalii*.

(33) *Wale wanacheza uwanjani*.

Katika sentensi (31), Kiwakilishi kionyeshi '*hili*' kinaonyesha nomino iliyo karibu na msemaji. Kiwakilishi '*hicho*' katika sentensi (32) kinaonyesha nomino iliyo mbali kidogo na msemaji. Katika sentensi ya (33) kiwakilishi kionyeshi '*wale*' kinaonyesha nomino iliyo mbali sana na msemaji. Viashiria '*hili*','*hicho*' na '*wale*' vinarejelea nomino karibu, karibu kidogo na mbali sana kutoka kwa msemaji.

### 2. 2.5 Urejelezi wa kulinganisha

Urejelezi wa kulinganisha huonyesha hali ya kufanana au kutofanana kwa vitu viwili au zaidi. Halliday na Hasan (1976) wanaeleza kuwa ili vitu viwili vilinganishwe, ni lazima pawe na kitu kingine kinacholinganishwa nacho. Urejelezi wa kulinganisha unaweza kuwa nje ya matini (urejelezi wa eksofora) au ndani ya matini (urejelezi wa endofora). Ikiwa ulinganishi huu ni wa endofora, unaweza kuwa urejelezi wa kianafora au urejelezi wa katafora. Maneno kama vile kuliko, zaidi, -ingine na kama hutumiwa kuonyesha urejelezi wa kulinganisha. Kwa mfano:

(34) *Sikuku ni mrefu kuliko Simiyu.*

Katika sentensi hii, '*Simiyu'* analinganishwa na '*Sikuku*'. Ulinganishi huu unajitokeza katika muktadha wa sentensi. Huu ni urejelezi wa kianafora.

### 2.2.6 Uunganishaji

Uunganishaji ni matumizi ya viunganishi ili kuonyesha uhusiano wa kimaana baina ya sentensi. Urefu wowote wa matini unatokana na kuunganishwa kwa vipengele mbalimbali kama vile: kuunganishwa kwa maneno na maneno mengine na kuunganishwa kwa maneno na alama za uakifishaji. Viunganishi huunganisha sentensi katika matini na kuonyesha uhusiano baina ya sentensi.

Halliday na Hasan (1976) wanaeleza kuwa viunganishi hutumika kuunganisha sentensi kimaana. Habwe na Karanja (2004), pia wanaeleza kuwa viunganishi hutumika kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Kulingana nao, kuna viunganishi kama vile: viunganishi viongezi, viunganishi vya kuonyesha sababu, viunganishi vya kuonyesha kinyume, viunganishi vya kuonyesha chaguo, viunganishi vya kuonyesha masharti na viunganishi vitegemezi.

Viunganishi viongezi huonyesha hali ya kuongezeka katika idadi, kwa mfano: *na, aidha, isitoshe, tena, mbali na, zaidi ya* na *pia*. Viunganishi hivi huongeza taarifa katika sentensi. Kwa mfano:

*(35) Kamau anasoma na Ouma anacheza uwanjani.*

Katika sentensi ya (35), idadi ya vitendo vya kamau vimeongezeka: kusoma na kucheza. Kamau pamoja na Ouma wanatenda vitendo tofauti: kusoma na kucheza.

Viunganishi visababishi ni viunganishi vinavyoonyesha hali ya kusababisha. Viunganishi hivi huonyesha kuwa jambo moja limesababisha jingine. Kwa mfano: *kwa hivyo, kisha, basi, halafu, kwa vile, mintaarafu (kutokana na)* na *kwa sababu*. Kwa mfano:

*(36) Rukia alichelewa kufika shuleni kwa sababu hakuamka mapema.*

Kiunganishi '*kwa sababu'* kinaunganisha mambo mawili yanayohusika katika sentensi hii. Kutoamka mapema kwa Rukia kulisababisha kuchelewa kwake kufika shuleni.

*(37) Mama alipika chakula halafu akaondoka kwenda sokoni*.

Kiunganishi '*halafu'* kimetumiwa kuonyesha mfuatano wa matukio kiwakati katika sentensi. Mama alipika chakula na baada ya kupika chakula aliondoka kwenda sokoni.

Kiunganishi hiki husaidia msomaji kufuatilia mfuatano wa matukio kiwakati katika sentensi.

Viunganishi vya kuonyesha kunyume vinatumika katika sentensi kuonyesha hali kinyume katika uhusiano fulani katika mfuatano wa mambo. Kwa mfano: *ila, lakini, isipokuwa, ijapokuwa, bali, hata hivyo, licha ya, ilhali* na kadhalika. Kwa mfano:

*(38) Yusufu aliamka mapema ila hakufika shuleni mapema*.

(39) *Lui alishauriwa lakini hakuzingatia ushauri huo*.

Katika sentensi ya (38), Yusufu alikuwa akitarajiwa kufika shuleni mapema kwa sababu alikuwa ameamka mapema lakini alichelewa kufika shuleni hata baada ya kuamka mapema. Kiunganishi '*ila*' kinaunganisha sentensi mbili pamoja na kuonyesha uhusiano wa kimaana baina ya sentensi hizi.

Katika sentensi ya (39), Kiunganishi '*lakini'* kimetumiwa hapa kuonyesha kuwa Lui alifanya kinyume cha kile alichotarajiwa kufanya: alitarajiwa kuzingatia ushauri lakini hakufanya hivyo.

Viunganishi vya kuonyesha chaguo hutumika kuchagua baina mambo au vitu viwili au zaidi. Kwa mfano: *ama, au, wala* na *aidha*. Kwa mfano:

*(40) Yeye hali sima wala wali.*

*(41) Watalii watawasili Jumanne au Alhamisi*.

Katika sentensi (40), kiunganishi '*wala*' kimetumiwa kuonyesha hali ya kutoteua baina ya vitu wiwili: '*sima'* na *'wali'*. Viunganishi vya kuonyesha chaguo (viteuzi) hutumiwa kuonyesha hali ya kuchagua baina ya tendo au kitu kimoja na kingine. Katika sentensi (41), hakuna kitu kilichochaguliwa. Katika sentensi ya (39), kitendo cha kuwasili kitatendeka siku moja tu; Jumanne au Alhamisi.

Viunganishi vya kuonyesha masharti hutumiwa kuunganisha sentensi na nyingine. Kwa mfano: *kama, ikiwa, iwapo,* na *endapo*. Kwa mfano:

*(42) Musa atapita mtihani iwapo atasoma kwa bidii.*

*(43) Ali atachaguliwa kuwa mbunge kama ataomba kura.*

Katika sentensi (42), kiunganishi '*iwapo'* kinaunganisha sentensi *'Musa atapita mtihani*'na *'atasoma kwa bidii'* ilhali kiunganishi '*kama'* katika sentensi (43) kinaunganisha sentensi *'Ali atachaguliwa kuwa mbunge*' na *'ataomba kura'*. Katika sentensi hizi, kitendo cha pili kinategemea kitendo cha kwanza ili kueleweka. Huu ni urejelezi wa kianafora.

Viunganishi vitegemezi hutumika kuunganisha vishazi tegemezi na vishazi huru katika sentensi. Kwa mfano: *baada ya, kwa vile, -po, ingawa* na *kwa sababu.* Kwa mfano:

*(44) Kimani alituzwa kwa sababu alifanya vyema katika mtihani.*

(45) *Momanyi aliadhibiwa kwa vile hakumaliza zoezi darasani.*

Katika sentensi (44) na (45), viunganishi vitegemezi "*kwa sababu'* na '*kwa vile'* vinaunganisha vishazi tegemezi na vishazi huru. Sentensi (44) imeundwa kwa vishazi viwili: kishazi huru na kishazi tegemezi. *'Kimani alituzwa*' ni kishazi huru ilhali '*kwa sababu alifanya vyema*' ni kishazi tegemezi. Sentensi (45) vilevile ina kishazi huru na kishazi tegemezi. '*Momanyi aliadhibiwa*' ni kishazi huru ilhali '*kwa vile hakumaliza zoezi darasani*' ni kishazi tegemezi. Mbali na matumizi ya viunganishi, ubadilishaji pia ni kijenzi muhimu cha mshikamano katika matini.

### 2.2.7 Ubadilishaji

Ubadilishaji ni hali ya neno au kirai kuchukua nafasi ya neno au kirai kingine katika sentensi. Ubadilishaji unahusu uhusiano baina ya vipashio vya kiisimu. Ubadilishaji unachunguzwa kwa sababu ufasiri wa maana ya maneno ambayo nafasi yao yamechukuliwa na maneno mengine katika matini humhitaji msomaji kurejelea maneno yaliyotajwa katika sentensi zilizotangulia. Halliday na Hasan (1976) wanaeleza kuwa aina tatu za ubadilishaji:

#### 2.2.7.1 Ubadilishaji wa nomino

Ubadilishaji wa nomino ni hali ambapo nafasi ya nomino au kiwakilishi katika sentensi huchukuliwa na vyeo na majina ya vitu vilivyokuwa vimetajwa badala ya nomino. Ubadilishaji wa nomino huweza kutokea katika matini kupitia matumizi ya vyeo, viwakilishi, majina ya watu au vitu ambavyo vilikuwa vimetajwa hapo awali katika sentensi badala ya nomino iliyokuwa imetajwa. Ubadilishaji huu ni wa kianafora kwa sababu vyeo, viwakilishi, majina ya watu na vitu vilivyokuwa vimetajwa hapo awali hutumika katika sentensi badala ya nomino yenyewe. Kwa mfano:

*(46) Njuguna alipochaguliwa na wananchi alifanya kazi bidii. Mbunge huyo alipendwa sana.*

*(47) Walimu wanafanya kazi muhimu sana. Wao wanastahili kupongezwa.*

Katika sentensi (46) nomino '*mbunge'* imetumiwa kurejelea nomino '*Njuguna'* ambayo ilikuwa imetajwa hapo awali katika sentensi. Katika sentensi (47), kiwakilishi '*wao*' kimetumiwa badala ya nomino '*walimu*'. Ili kuelewa maana ya kiwakilishi '*wao*', msomaji atalazimika kurejelea nomino '*walimu*'. Huu ni urejelezi wa kianafora. Hapa, nafasi ya nomino imechukuliwa na kiwakilishi. Ubadilishaji wa vitenzi huchangia kuleta mshikamano katika matini.

### 2.2.7.2 Ubadilishaji wa vitenzi

Ubadilishaji wa vitenzi hutokea wakati ambapo vitenzi huchukua nafasi ya virai vitenzi vilivyotajwa awali katika sentensi. Wakati mwingine maneno *'hivyo'* au *'kama'* hutumika. Ubadilishaji huu hutumika kianafora kwa sababu vitenzi hurejelea vitenzi au virai vitenzi vilivyotajwa hapo awali katika sentensi. Ubadilishaji wa vitenzi huondoa urudiaji na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

(48) *Mwalimu alimwambia mwanafunzi asome. Mwanafunzi alifanya hivyo.*

Katika sentensi hii kirai kitenzi '*alifanya hivyo'* hurejelea kitenzi '*kusoma'* kilichotajwa hapo awali katika sentensi. Vilevile, ubadilishaji wa vishazi unaweza kutumiwa kuleta mshikamano katika matini.

### 2.2.7.3 Ubadilishaji wa vishazi

Ubadilishaji wa vishazi hutokea wakati ambapo nafasi ya kishazi kizima inachukuliwa na neno lingine linalorejelea kishazi hicho. Neno kama vile '*hivyo'* huweza kutumika ili kuepuka na urudiaji wa kishazi hicho. Kwa mfano:

*(49) Maimuna alipomwona rafiki yake, alibubujikwa na machozi ya furaha. Rafiki yake akafanya hivyo pia*.

Katika sentensi hii, nafasi ya kishazi '*alibubujikwa na machozi ya furaha*' kinachukuliwa na kishazi '*akafanya hivyo'.* Kishazi *'akafanya hivyo'* linarejelea kishazi *'alibubujikwa na machozi ya furaha'* kilichotajwa awali katika sentensi. Huu ni urejelezi wa kianafora. Mbali na kutumia ubadilishaji, udondoshaji pia huweza kutumiwa kiurejelezi kuleta mshikamano katika matini.

**2.2. 8 Udondoshaji**

Udondoshaji unahusu kuacha baadhi ya maneno katika sentensi ili kupunguza urudiaji. Nafasi iliyoachwa katika sentensi baada ya kudondoa neno au kishazi inaweza kujazwa kwa kurejelea vipashio katika sentensi iliyotangulia ili kupata neno lililofaa kuchukua nafasi hiyo. Katika udondoshaji, maneno yanaachwa wakati kirai ni lazima lirudiwe. Udondoshaji unaonyesha uhusiano wa kisarufi kati ya maneno, virai au vishazi katika matini. Udondoshaji ni […] kitu au jambo ambalo limeachwa bila kusema. Jambo ambalo limeeleweka linatumika kwa njia fulani bila kutamka au kusema (Halliday na Hasan 1976:142). Kwa mfano:

*(50) Mumo alienda dukani akanunua kalamu, kitabu na gazeti.*

Katika sentensi hii, kitenzi *'akanunua'* kimedondolewa badala ya kuandika sentensi *'Maria alienda dukani akanunua kalamu, akanunua kitabu na akanunua gazeti.'* Udondoshaji unaojitokeza hapa ni udondoshaji wa vitenzi. Ili kuelewa kitendo kilichofanyika kwa nomino kitabu na gazeti, itambidi msomaji kurejelea kitendo kilichofanyika kwa nomino kalamu (kitendo cha kununuliwa). Kitenzi *'akanunua'* kinaonyesha urejelezi wa kianafora katika sentensi.

(51) *Watalii wanne walizuru mji wa Nairobi na wakaondoka mapema.*

Katika sentensi hii, nomino *'watalii'* imedondolewa ili kuepuka urudiaji badala ya kuandika sentensi,*'watalii wanne walizuru mji wa Nairobi na watali wakaondoka mapema.'* Ili kuelewa maana ya '*wa',* katika *'wakaondoka',* msomaji atabidi kurejelea nomino '*watalii'* iliyotajwa hapo awali. Huu ni urejelezi wa kianafora. Aina ya udondoshaji unaojitokeza hapa ni udondoshaji wa nomino.

(52) *Kuna mtu aliyechukua kitabu changu bila idhini. Laiti ningemjua ningemnunulia chake.*

Katika sentensi hii, kishazi *'mtu aliyechukua kitabu changu'* kimedondolewa ili kuepuka urudiaji. Iwapo kishazi hiki kingerudiwa, sentensi hii ingekuwa:

*(53) Kuna mtu aliyechukua kitabu changu bila idhini. Laiti ningemjua mtu aliyechukua kitabu changu ningemnunulia kitabu chake.* Huu ni udondoshaji wa vishazi.

Katika udondoshaji, kuna uhusiano baina ya neno linalotumika kurejelea neno lililodondolewa na neno lililodondolewa. Uhusiano huu ni wa kianafora.

### 2.2.9 Hitimisho

Katika sura ya pili, tumefafanua vipengele muhimu vinavyotumika kiurejelezi ili kuleta mashikamano katika matini. Vipengele hivi ni kama vile: urudiaji wa nomino muhimu, matumizi ya sinonimu, matumizi ya haiponimu, urejelezi wa kieksofora, urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha. Aidha, tumefafanua vipashio vinavyoweza kutumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika matini. Vipashio hivi ni kama vile: uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji. Vijenzi hivi vya mshikamano huungana ili kujenga matini na kufanikisha mawasiliano wa kimaana.

# SURA YA TATU

# AINA ZA UREJELEZI KATIKA GAZETI LA *TAIFA LEO*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili, tumeshughulikia vipengele muhimu vinavyochangia kuleta mshikamano katika matini kama vile: urudiaji wa nomino muhimu, matumizi ya sinonimu, matumizi ya haiponimu, urejelezi, anafora, katafora, uunganishaji, ubadilishaji, udondoshaji, urudiaji na matumizi ya viwakilishi. Katika sura ya tatu tutabainisha aina za urejelezi zilizotumika katika *Habari za Kaunti* na sababu za kutumika katika matini. Vilevile, tutabainisha jinsi nadharia ya Sarufi Amilifu imetumiwa kuonyesha umuhimu wa kutumia urejelezi kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo*. Isitoshe, tutabainisha jinsi msomaji atakavyotumia nadharia ya Uhusiano ili kufikia maana tambuzi. Halliday na Hasan (1976) wanafafanua kuwa kuna aina tatu za urejelezi:

## 3.2 Urejelezi Nafsi

Urejelezi nafsi ni watu wanaoshiriki katika mazungumzo. Urejelezi huu hubainika kupitia matumizi ya vimilikishi na viwakilishi. Viwakilishi ni viambishi au maneno yanayotumika badala ya nomino. Vimilikishi kama vile: -angu, -etu, -ako, -enu, -ake na –ao vinaweza kutumika kuonyesha urejelezi nafsi. Viwakilishi nafsi ni vya aina mbili: viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsi viambata.

Tofauti kati ya viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsi viambata ni kuwa viwakilishi nafsi huru havihitaji kuongezewa viambishi vyovyote ili kukamilika kimaana ilhali viwakilishi nafsi viambata hutokea kama viambishi mwanzoni mwa vitenzi. Viwakilishi nafsi huru ni kama vile: mimi, sisi, wewe, nyinyi, yeye na wao ilhali viambishi nafsi viambata ni kama vile: ni-, tu-, m-, a- na wa-. Isitoshe, viwakilishi nafsi viambata huwakilisha nafsi huru.

### 3.2.1 Viwakilishi Nafsi Viambata

Urejelezi nafsi ulitumika katika *Habari za Kaunti* kupitia matumizi ya viwakilishi nafsi viambata. Viwakilishi nafsi viambata hutokea kama viambishi. Aidha, viwakilishi nafsi viambata hujitokeza mwanzoni mwa vitenzi. Viwakilishi nafsi viambata huchangia katika kujenga matini na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

(54) *Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha, ameonya kuwa afisa yeyote ya umma atakayehusishwa na ufisadi atasimamishwa kazi.*

*Akizungumza wakati wa kuapisha maafisa sita wapya wa Bodi ya Kuajiri wafanyakazi Kaunti ya Lamu (PSB), Bw. Twaha aliwasisitizia haja ya kuzingatia maadili, uwazi na uwajibikaji wakati watakapokuwa wakitekeleza majukumu yao.*

*Alionya kwamba serikali yake haitamruhusu yeyote atakayejihusisha au kupatikana na kesi za ufisadi kuendelea kuhudumu katika bodi hiyo.*

*"Ninawapongeza nyote kwa kufaulu kuchaguliwa. Langu ni kuwaomba kuzingatia maadili na kutekeleza majukumu yenu kwa uwazi na uwajibikaji. Ukijihusisha na ufisadi wa aina yoyote hutakuwa na budi ila kutemwa nje. Wakazi wa Lamu wanawategemea nyinyi ili kuleta sura mpya katika utekelezaji wa majukumu yenu," akasema Bwana Twaha.*

*…*

*Waliapishwa katika hafla maalum iliyoandaliwa kwenye makao makuu ya Kaunti ya Lamu mjini Mokowe iliyohudhuriwa pia na Naibu Gavana Abdulhakim Aboud… (Matini 4).*

Katika mfano (54), kiwakilishi nafsi kiambata *a*- katika neno *akizungumza* kimetumiwa kumrejelea Gavana wa Kaunti ya Lamu, *Bw. Fahim Twaha* ambaye alikuwa ametajwa katika aya ya kwanza. Bw. Twaha alikuwa akizungumza wakati wa kuapishwa kwa maafisa sita waliofaulu kuchaguliwa kuhudumu katika Bodi ya Kuajiri Wafanyakazi Kaunti ya Lamu (PSB). Kiwakilishi nafsi kiambata *a*- kimetumika kumrejelea kianafora *Gavana Twaha* na kuleta mshikamano katika matini. Ili msomaji afasiri maana ya kiwakilishi kiambata *a*- katika neno *akizungumza*, itambidi arejelee nomino *Gavana Twaha* iliyokuwa imetajwa katika matini.

Kiwakilishi nafsi kiambata *ni*- katika neno *ninawapongeza* kimetumika na mzungumzaji kujirejelea. Kiwakilishi nafsi kiambata *ni*- kinamrejelea mzungumzaji katika nafsi ya kwanza umoja. Mzungumzaji ni Gavana wa Kaunti ya Lamu ambaye alikuwa ametajwa katika aya zilizotangulia katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika kuonyesha kuwa mzungumzaji katika aya hii ni yule yule ambaye amejitokeza katika aya iliyotangulia.

Kiwakilishi nafsi kiambata *u*- katika neno *ukijihusisha* kimetumiwa kiurejelezi kurejelea kila afisa aliyeajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu. Kiwakilishi

nafsi kiambata *u-* kinamrejelea mzungumzaji katika nafsi ya pili, umoja. Kila afisa miongoni mwa maafisa sita waliofaulu kuajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu alikuwa akirejelewa. Maafisa sita hawa walikuwa wametajwa katika aya zilizotangulia. Urejelezi wa kianafora umetumika kubainisha maafisa wanaorejelewa na kuleta mshikamano katika matini.

Kiwakilishi nafsi kiambata *m-* katika neno *mtafaulu* kimetumika kuwarejelea maafisa sita waliofaulu kuajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu. Kiwakilishi nafsi kiambata *m-* kinawarejelea wazungumziwa katika nafsi ya pili, wingi. Maafisa hawa walikuwa wametajwa awali katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana na kuleta mshikamano katika matini. Mbali na matumizi ya viwakilishi nafsi viambata kianafora kuleta mshikamano, viwakilishi ngeli pia vimetumika kiurejelezi kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti.*

Viwakilishi ngeli hutambulika kupitia matumizi ya viambishi ngeli. Viambishi ngeli ni herufi moja au mbili ambazo zinatumiwa kuonyesha ngeli ya nomino inayorejelewa katika matini. Kiambishi *a-* katika maneno *akiongea* na *alionya* kinarejelea nomino *Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha* ambayo ilikuwa imetajwa katika matini. Nomino inayorejelewa iko katika ngeli ya A-WA umoja kwa mujibu wa uainisho wa ngeli kwa kutumia viambishi vya upatanisho. Viambishi vya upatanisho vinavyowekwa mwanzoni mwa vitenzi hurejelea nomino katika sentensi au aya iliyotangulia au inayofuata. Ili msomaji afasiri nomino inayorejelewa na kiambishi ngeli *A-*, atalazimika kurejelea nomino inayopatikana katika ngeli ya A-WA katika aya ya kwanza.

Kiwakilishi ngeli *WA-* katika neno *waliapishwa* kinarejelea nomino *maafisa* ambayo ilikuwa imetajwa katika matini. Nomino *maafisa* inapatikana katika ngeli ya A-WA, wingi. Ufasiri wa maana ya kiambishi *wa-* katika neno *waliapishwa* unategemea nomino *maafisa* ambayo ilikuwa imetajwa katika sehemu ya matini iliyotangulia. Kwa hivyo, viwakilishi ngeli huchangia kuleta mshikamano katika matini.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kuelezea mambo yanayotendeka katika Kaunti ya Lamu. Kiwakilishi nafsi kiambata *a*- katika neno *akizungumza* na *ni*- katika neno *ninawapongeza* vinarejelea nomino Gavana wa Kaunti ya Lamu iliyokuwa imetajwa. Ili msomaji afasiri maana ya neno Gavana, itambidi apanue maana ya neno Gavana kupitia dhana maalum ya kihali. Kupitia kwa upanuzi huu, chukulizi zifuatazo zitakuzwa kuhusu dhana ya Gavana:

(i) mkuu wa jimbo
(ii) mtu anayeheshimiwa
(iii) mtu mwenye mamlaka
(iv) msimamizi wa Benki Kuu katika nchi fulani
(v) mwakilishi wa mfalme au malkia katika koloni

Chukulizi hizi zote zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea Gavana kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Hata hivyo, chukulizi chache huweza kuchaguliwa na msomaji kurejelea Gavana. Msomaji atachagua chukulizi (i) hadi (iii) kwa sababu zina uhusiano wa hali ya juu kwa matini hii na zinaleta maana kwa ujumbe unaokusudiwa na mwandishi kwa msomaji. Chukulizi (iv) na (v) zitaachwa kwa sababu hazileti maana kulingana na muktadha wa tamko na hazina kiwango cha juu cha uhusiano. Chukulizi zilizokuzwa zinaweza kuchunguzwa kupitia dhana maalum ya kihali. Katika muktadha huu, dhana maalum ya kihali ya Gavana ni mkuu wa jimbo, anayeheshimiwa na mwenye mamlaka wala sio mwakilishi wa mfalme au malkia katika koloni au msimamizi wa Benki katika nchi fulani.

Kiwakilishi nafsi kiambata *u*- katika neno *ukijihusisha* kinamrejelea dhana ya *kila afisa* aliyeajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu. Ili msomaji afasiri maana kiwakilishi nafsi kiambata *u*- katika kitenzi *ukijihusisha*, ni lazima arejelee nomino *maafisa sita* iliyokuwa imetajwa.

Vile vile, Kiwakilishi ngeli *WA*- katika neno *waliapishwa* kinawarejelea *maafisa* sita ambao walikuwa wakiapishwa ili kuhudumu katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu. Nomino maafisa inapatikana katika ngeli ya A-WA, wingi. Kwa hivyo, kiwakilishi ngeli *WA*- kinaleta dhana ya nafsi ya tatu, wingi. Ili msomaji afahamu nomino

na kiwakilishi nafsi Ngeli *WA*- inayorejelewa katika nafsi ya tatu, itambidi arejelee nomino *maafisa* iliyokuwa imetajwa awali.

Mhimili wa maana matini umetumiwa na mwandishi kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Ufasiri wa ujumbe katika aya moja unategemea sentensi au aya zilizotangulia. Kwa mfano, ufasiri wa ujumbe katika aya tatu na ya pili unategemea aya ya kwanza. Ufasiri wa maana ya viwakilishi nafsi viambata *(a-, ni-, u-, m-* na *wa-)* na viwakilishi ngeli (*A-* na *WA-)* unategemea nomino *Fahim Twaha* na *maafisa sita* zilizotajwa awali katika matini.

(55) *Serikali imejitetea kuhusu ubomoaji wa vibanda katika ufuo wa Jomo Kenyatta almaarufukama Pirates, Kaunti ya Mombasa.*

*Kwenye mahojiano na Taifa Leo, Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Makavazi ya Kenya (NMK) eneo la Pwani, Bw. Athman Hussein alisema wanashirikiana na serikali ya kaunti pamoja na Wizara ya Utalii ili kuupa ufuo huo sura mpya, ifikie hadhi ya kimataifa.*

*…*

*"Tumekuwa na mipango hii tangu tupewe mamlaka ya kusimamia ufuo huo. Eneo lenyewe limekuwako na vibanda vingi vibovu na hata hali ya usalama haijakuwa ya kuridhisha na tunataka kubadilisha haya yote', akasema Bw. Hussein … (Matini 5).*

Katika mfano (55), kiwakilishi nafsi kiambata *tu*- katika neno *tumekuwa* kinarejelea Mamlaka ya Makavazi ya Kenya na serikali ya Kaunti ya Mombasa ambazo zilikuwa zimetajwa katika aya ya pili katika matini. Naibu mkurugenzi wa Mamlaka ya Makavazi ya Kenya eneo la Pwani, Bw. Hussein anarejelea kianafora Mamlaka ya Makavazi ya Kenya na serikali ya Kaunti ya Mombasa iliyotajwa katika aya iliyotangulia. Kiwakilishi nafsi kiambata *tu*- kimetumika kuleta mshikamano katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi pia umetumika kueleza shughuli ya ubomoaji inayoendelea katika Kaunti ya Mombasa. Neno ubomoaji ndilo linabeba maana kuu katika matini hii. Msomaji atahitajika kushughulikia dhana ubomoaji kupitia upanuaji ili apate chukulizi

zinazofaa na ambazo zinaweza kuleta maana iliyokusudiwa na mwandishi. Dhana ya ubomoaji itaweza kuwa na chukulizi zifuatazo:

(i) kuvunja kitu kilichokuwa kimejengwa

(ii) kuharibu kitu

(iii) kuvuruga mpangilio fulani

Katika muktadha huu, chukulizi hizi zote zinarejelea dhana ya ubomoaji kwa jumla. Msomaji atateua chukulizi chache ambazo zinaweza kurejelea dhana ubomoaji kulingana na muktadha wa tamko na kiwango cha uhusiano. Hivyo basi, atateua chukulizi (i) na (ii) kurejelea dhana ubomoaji kwa sababu zinaleta maana na zina kiwango kikubwa cha uhusiano na kuacha chukulizi (iii) ambayo haina kiwango kikubwa cha uhusiano. Maana inayopatikana hapa ni ubomoaji unaorejelewa kupitia chukulizi (i) na (ii) ni kuvunja kitu kilichokuwa kimejengwa au kuharibu kitu. Vitu vinavyorejelewa katika muktadha huu ni vibanda.

Mhimili wa maana matini umetumiwa kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Kwa mfano, ili kufasiri maana ya kiwakilishi nafsi kiambata *tu-* katika neno *tumekuwa* unategemea nomino *Mamlaka ya Makavazi ya Kenya* na *Serikali ya Kaunti ya Mombasa* ambazo zilikuwa zimetajwa katika sehemu ya matini iliyotangulia.

### 3.2.2 Viwakilishi Nafsi Huru

Viwakilishi nafsi huru hujisimamia ili kuleta maana katika matini. Viwakilishi nafsi huru haviongezwi viambishi vyovyote ili kukamilika kimaana. Maneno kama vile mimi, sisi, wewe, nyinyi, yeye na wao ni viwakilishi nafsi huru. Viwakilishi nafsi huru vimetumika katika *Habari za Kaunti* kurejelea wazungumzaji na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(56) Wazee kutoka jamii ya Wakamba wamezidisha juhudi za kutaka Kiongozi wa Chama cha Wiper, Bw. Kalonzo Musyoka amrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022.*

*…*

*"Inatuhitaji sisi sote kukomesha siasa zisizokuwa na maana na kuelekeza nguvu zetu kumuunga Rais," alisema Bw. Kilonzo aliyesoma taarifa ya wazee hao… (Matini 6).*

Kiwakilishi nafsi huru *sisi* katika mfano (56) kimetumika na Bw. Kilonzo kuwarejelea kianafora *wazee kutoka jamii ya Wakamba* ambao walikuwa wameungana kuunga mkono nia ya Bw. Kalonzo Musyoka kumrithi Rais Uhuru Kenyatta baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2022. Kiwakilishi nafsi huru *sisi* kinaonyesha kuwa nomino inayozungumziwa ni ya nafsi ya kwanza, wingi. Ili kufasiri maana ya kiwakilishi nafsi huru *sisi*, msomaji atalazimika kurejelea neno *wazee* lililokuwa limetajwa katika aya ya kwanza. Kiwakilishi nafsi huru *sisi* kimetumika kianafora ili kuleta uhusiano wa kimaana na kuleta mshikamano katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa kuelezea mambo ya urithi wa urais yanayojadiliwa na Wazee kutoka jamii ya Wakamba. Msomaji anaweza kufasiri maana ya neno wazee kwa kutumia mhimili wa kanuni tambuzi na mhimili wa kanuni mawasiliano. Neno hili limetumiwa na mwandishi kwa njia isiyo wazi kwa hivyo linaweza kufasiriwa na msomaji kwa kutumia kamusi ya ubongo. Itamlazimu msomaji apanue maana ya neno wazee kupitia kwa dhana maalum ya kihali. Kutokana na upanuzi huo, chukulizi zifuatazo zitakuzwa zinazohusiana na dhana ya wazee:

(i) watu
(ii) walioishi miaka mingi
(iii) watu wanaoheshimiwa
(iv) wanaume
(v) wazazi wa kiume, hasa kina baba

Chukulizi zote zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea wazee kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Msomaji huteua tu chukulizi ambazo zinafaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Hivyo basi, msomaji atachagua chukulizi (i) hadi (ii) kwa sababu zinaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na zina uhusiano wa kiwango cha juu na kuacha chukulizi (iv) na (v) kwa sababu hazina uhusiano wa kiwango cha juu. Maana maalum itakayopatikana ya wazee ni watu walioishi miaka mingi wanaoheshimiwa wala sio wanaume au wazazi wa kiume hasa kina baba.

Isitoshe, neno wamezidisha limetumika kwa maana tambuzi. Ili msomaji afahamu maana ya neno hili, atatumia mkakati wa ukadiriaji. Neno wamezidisha linaweza kuwasilisha maana yake halisi yaani zidisha au hali iliyo karibu na kuzidisha.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana matini kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Kwa mfano, ufasiri wa maana ya kiwakilishi nafsi huru *sisi* unategemea neno *wazee* kutoka jamii ya Wakamba ambao walikuwa wakihimizwa kukomesha siasa zisizokuwa na maana na kuelekeza nguvu zao kumuunga Rais Uhuru Kenyatta.

*(57)* *Zaidi ya shule 1,000 za kibinafsi nchini huenda zikakosa kufunguliwa mwaka ujao, chama cha shule za kibinafsi nchini (KPSA), kimesema.*

*…*

*Wakizungumza na wanahabari katika afisi za shirika la Haki Africa, mwenyekiti wa shule za kibinafsi mjini Mombasa, Bw. Omar Mboli alisema si sawa watu wa sekta zingine kufadhiliwa na serikali huku wao wakitelekezwa.*

*"Tunasikitika kuona serikali imetoa ufadhili wa wasanii, wadau wa sekta ya hoteli, makahaba na kadhalika, ilhali sisi hatujatambulika licha ya kutoa huduma muhimu nchini", akasema … (Matini 25).*

Bw. Omar Mboli amewarejelea kianafora *wawakilishi wa shule za kibinafsi* katika Kaunti ya Mombasa kupitia matumizi ya kiwakilishi nafsi huru *sisi* katika mfano (57). Mhimili wa maana matini umetumiwa na mwandishi kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Ili kufasiri maana ya kiwakilishi nafsi huru *sisi*, msomaji atalazimika kurejelea neno *wawakilishi wa shule za kibinafsi* lililokuwa limetajwa awali katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika kubainisha wazungumzaji wanaorejelewa katika matini.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kueleza kuwa zaidi ya shule 1,000 za kibinafsi nchini huenda zikakosa kufunguliwa mwaka ujao. Neno shule limetumika na mwandishi kwa namna iliyo wazi kwa hivyo, maana yake imebanwa. Maana ya neno lililobanwa hufasiriwa moja kwa moja. Msomaji atafasiri maana iliyosimbwa katika neno shule moja kwa moja. Kutokana na ufasiri huu, msomaji atakuwa na maana zifuatazo katika akili yake:

(i) mahali kuna madarasa
(ii) kuna wanafunzi
(iii) kuna mwalimu au walimu
(iv) kuna vitabu

Mwandishi amebana maana ya neno shule ili kuleta maana ya mahali kuna madarasa, wanafunzi, walimu na vitabu. Msomaji atajijazia akilini ili kuelewa anayosema mwandishi.

### 3.2.3 Vimilikishi

Vimilikishi ni maneno yanayoeleza nomino inayomilikiwa na mtu. Vimilikishi huonyesha kitu au jambo linalomilikiwa na mtu. Vimilikishi hutumiwa kutegemea nafsi kwa mfano:

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| Nafsi ya kwanza | -angu | -etu |
| Nafsi ya pili | -ako | -enu |
| Nafsi ya tatu | -ake | -ao |

Viwakilishi vimilikishi vimetumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Viwakilishi vimilikishi hutumia mizizi ya vimilikishi nafsi kuonyesha nomino inayomilikiwa. Wakati wa kutumia viwakilishi vimilikishi, nomino inayomilikiwa haitajwi. Mizizi ya viwakilishi vimilikishi huchukua kiambishi cha ngeli. Viwakilishi vimilishi vimetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuonyesha uhusiano wa kimaana na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

(58) *Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha, ameonya kuwa afisa yeyote ya umma atakayehusishwa na ufisadi atasimamishwa kazi.*

*…*

*… Langu ni kuwaomba kuzingatia maadili na kutekeleza majukumu yenu kwauwazi na uwajibikaji. Ukijihusisha na ufisadi wa aina yoyote hutakuwa na budi ila kutemwa nje …*

*(Matini 4).*

Kiwakilishi kimilikishi *langu* katika mfano (58), kimetumika kianafora na mzungumzaji kujirejelea. Gavana Twaha alikuwa akitoa ombi lake kwa maafisa sita waliofaulu kuchaguliwa kuhudumu katika Bodi ya Kuajiri Wafanyakazi Kaunti ya Lamu (PSB) kuzingatia maadili na kutekeleza majukumu yao kwa uwazi na uwajibikaji. Ufasiri wa maana ya kiwakilishi kimilikishi *langu* unategemea nomino *Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha.*

Mhimili wa maana matini umetumika kuleta mshikamano katika matini. Ili msomaji afasiri maana ya kiwakilishi kimilikishi *langu,* atambidi arejele nomino *Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha* iliyokuwa imetajwa katika aya iliyotangulia.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza kuhusu ufisadi unaoendelezwa na maafisa wanaofanya kazi katika Kaunti ya Lamu. Mwandishi ametumia neno ufisadi kwa njia iliyo wazi. Ili msomaji kupata maana ya ufisadi, itambidi kutumia mkakati wa kubana. Msomaji ataweza kupata maana ya ufisadi kwa kufasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno ufisadi. Msomaji atapata kuwa neno ufisadi lina maana ya kila aina ya uovu.

*(59)* *Familia saba katika kijiji cha Kisii mjini Thika, Kaunti ya Kiambu, wamefungiwa nyumba zao baada ya landilodi kudai hawajalipa kwa miezi miwili.*

*Kulingana na wapangaji hao, mwenye nyumba alifika hapo Jumanne asubuhi kwa fujo na kulazimisha kila mpangaji kuondoka ili afunge nyumba yake.*

*Licha ya wapangaji hao kumsihi awahurumie, hawakuwa na budi kwani alikuwa ameandamana na watu waliolazimisha wapangaji kuondoka au mali zao zitupwe nje … (Matini 3).*

Kivumishi kimilikishi *zao* kimetumiwa katika mfano (59) kurejelea kianafora nyumba za familia saba katika kijiji cha Kisii mjini Thika zilizofungwa na landilodi. Nyumba ya landilodi pia imerejelewa kianafora kupitia kivumishi kimilikishi *yake*. Isitoshe, mali za wapangaji zimerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi kimilikishi *zao*.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kueleza kuhusu wapangaji waliofungiwa nyumba zao katika kijiji cha Kisii mjini Thika, Kaunti ya Kiambu. Neno wapangaji ndilo linabeba maana kuu, kwa sababu limerudiwa katika matini. Mwandishi ametumia neno wapangaji kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji apate maana iliyokusudiwa maana ya neno hili, itambidi apanue kupitia kwa dhana maalum ya kihali. Upanuzi huu utakuza chukulizi zifuatazo ya dhana ya wapangaji:

(i) watu wanaokaa kwa nyumba au chumba na kulipa kodi

(ii) watu wanaoweka vitu au mambo kwa kufuata utaratibu fulani.

Chukilizi hizi zote zinarejelea wapangaji lakini chukulizi moja inayoleta maana kulingana na muktadha wa tamko na ina kiwango cha juu cha uhusiano kitachaguliwa na msomaji. Chukulizi (i) itachaguliwa kwa sababu ina uhusiano wa kiwango cha juu ilhali chukulizi

(ii) itaachwa kwa sababu haina kiwango cha juu cha uhusiano. Msomaji atapata maana ya wapangaji inayorejelewa kulingana na muktadha wa tamko kuwa ni watu wanaokaa kwa nyumba na kulipa kodi wala sio watu wanaoweka vitu au mambo kwa kufuata utaratibu fulani.

Mhimili wa maana matini umetumiwa na mwandishi kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano, ufasiri wa maana ya vivumishi vimilikishi *zao* na *yake* unategemea maneno *nyumba* na *mali* ambayo yalikuwa yametajwa awali katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika ili kuondoa urudiaji na kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini.

*(60)* *Wapenzi wa Kiswahili wamepata pigo baada ya mshairi mkongwe Abdalla Mwasimba kuaga dunia hapo jana akiwa na umri wa miaka 83.*

*…*

*Mtindo wake wa kughani ulivutia wengi, akiwemo mshairi Nuhu Zubeir Bakari almaarufu Al-Ustadh Pasua.*

*"Nimepoteza mwalimu aliyeniachia kikoba cha ughani wa mashairi. Alinichochea kuanza kuichangia mashairi magazetini nikiwa mwanafunzi wa darasa la sita. Ilikuwa tija kumsikiliza akighani tungo zangu redioni na imekuwa fahari kufanya naye kazi katika shirika moja", akasema Bakari.*

*Mashairi yake, Faida ya Pombe Nini, Mzungu Kutuita Bwana na Kuwa Hirizi yaliwapa vijana changamoto za kuachana na ulevi na kujitahidi kazini bila ya kutegemea mitishamba.*

*Kutokana na weledi wake katika ushairi, Mwasimba alitunukiwa tuzo kadhaa na kituo cha Kiswahili cha WASTA kinachomilikiwa na Guru Ustadh Wallah Bin Wallah mjini Ngong.*

*Mwanahabari wa Radio Maisha, Hassan Kauleni mwana wa Ali, alisema: "Kwake Mola ndiko tutokako na kwake ndiko turejeako. Kila nafsi itaonja mauti. Lala salama mzee wetu."*

*(Matini 30).*

Mshairi mkongwe marehemu Abdalla Mwasimba amerejelewa kianafora katika mifano (60) kupitia matumizi ya vivumishi vimilikishi *wake*, *yake* na *wetu*. Vivumishi vimilikishi *wake*, *yake* na *wetu* vimetumika kiurejelezi kurejelea mtindo wa Marehemu Abdalla

Mwasimba wa kutunga mashairi, mashairi aliyoyaghani, weledi wake wa kutunga mashairi na mauti yake.

Kivumishi kimilikishi *zangu* kimetumiwa na mzungumzaji kujirejelea. Mzungumzaji ni mshairi Nuhu Zubeir Bakari ambaye alichochewa na marehemu Abdalla Mwasimba kuchangia mashairi magazetini akiwa darasa la sita. Ilikuwa ni fahari kwa Zubeir Bakari kumsikiliza Marehemu Mwasimba Abdalla akighani tungo zake redioni.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kuelezea kuaga dunia kwa mshairi mkongwe Abdalla Mwasimba ambaye amerejelewa katika matini. Mwandishi ametumia neno kuaga kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji apate maana ya neno kuaga, atambidi kupanua neno hili kupitia dhana maalum ya kihali ili kukuza chukulizi zifuatazo ya dhana ya kuaga:

(i) kufariki

(ii) kwaheri

Chukulizi hizi zinarejelea neno kuaga kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Ili kupata maana ya neno kuaga, msomaji atateua tu chukulizi ambazo zinafaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Chukulizi (i) itachaguliwa na msomaji kwa sababu inaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na ina kiwango kikubwa cha uhusiano ilhali chukulizi (ii) itaachwa kwa sababu haileti maaana kulingana na muktadha wa tamko na haina kiwango kikubwa cha uhusiano. Maana ya neno kuaga kupitia kwa dhana maalum ya kihali ni kufariki wala sio kwaheri.

Mhimili wa maana matini umetumiwa kuonyesha kuwa ufasiri wa sehemu moja ya matini unategemea sehemu ya matini iliyotangulia. Ili msomaji afasiri maana ya vivumishi vimilikishi *wake*, *yake* na *wetu*, atalazimika kumrejelea *marehemu Abdalla Mwasimba* aliyekuwa ametajwa katika aya ya kwanza. Aidha, ufasiri wa maana ya kivumishi kimilikishi *zangu* unategemea nomino *Zubeir Bakari* iliyokuwa imetajwa awali. Urejelezi wa kianafora umetumika ili kuondoa urudiaji na kuleta mshikamano katika matini.

### 3.2.4 Katafora

Katafora matumizi ya kipashio cha kiisimu kuonyesha neno litakalotajwa katika matini. Katafora imetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

(61) *Wazee kutoka jamii ya Wakamba wamezidisha juhudi za kutaka Kiongozi wa Chama cha Wiper, Bw. Kalonzo Musyoka amrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022.*

…

*Akiongea na wanahabari wakiwa Mwala, mwenyekiti wa baraza la wazee wa koo za jamii ya Wakamba Boniface Kilonzo alihimiza jamii hiyo kuendelea kuunga mkono azma ya Bw. Kalonzo akisema nafasi yake ya kuongoza nchi imekaribia (Matini 6).*

*Bw. Boniface Kilonzo* (61) amerejelewa kupitia kiwakilishi nafsi kiambata *a*- ambacho kinatokea katika neno *akiongea* mwanzoni mwa aya. Urejelezi unaojitokeza hapa ni urejelezi wa katafora kwa sababu kiwakilishi nafsi kiambata *a*- kimetumika kurejelea nomino *Bw. Boniface Kilonzo* itakayotajwa katika matini. Urejelezi wa katafora umetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kuelezea juhudi za wazee kutoka jamii ya Wakamba za kuunga mkono azma ya Bw. Kalonzo Musyoka za kumrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022. Mwandishi ametumia neno jamii kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji aweze kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi, itambidi apanue maana ya neno jamii kutumia kikamusi cha utambuzi. Katika kikamusi hicho, chukulizi zifuatazo zitakuzwa katika akili ya msomaji:

(i) watu wenye asili moja

(ii) mkusanyiko wa watu au vitu

Chukulizi zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea neno jamii kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Msomaji atachagua tu chukulizi zinazofaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Hivyo, msomaji atachagua chukulizi (i) kwa sababu ina kiwango cha juu cha uhusiano na inaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na kuacha chukulizi (ii) kwa sababu haina kiwango cha juu cha uhusiano na haileti maana. Msomaji ataweza kufahamu maana ya jamii kulingana na muktadha na kifaa cha uhusiano kuwa ina maana watu wenye asili moja wala sio mkusanyiko wa watu au vitu.

Vile vile, mhimili wa maana matini umetumiwa kuonyesha uhusiano wa kimaana katika sentensi. Ili kufasiri maana ya kiwakilishi kiambata *a*- katika neno *akiongea*, msomaji atalazimika kurejelea nomino *Bwana Kilonzo* inayojitokeza katika sentensi hiyo.

(62) *Wawekezaji katika sekta ya utalii kaunti ya Nakuru sasa wanataka kujua jinsi jinsi watakavyonufaika na Sh 3 billioni zilizotengwa na serikali kuifufua sekta hiyo. Mwenyekiti wa muungano wa watalii katika kaunti hiyo, Bw. David Mwangi na mwenyekiti wa muungano wa waelekezaji watalii John Mwangi walisema sekta hiyo ni miongoni mwa sekta zilizoathiriwa vibaya na ugonjwa wa corona.*

*…*

*Akiongea kwa niaba ya waelekezi wa watalii, Bw. John Mwangi naye alisisitiza kwamba kuna haja ya serikali kuwaeleza jinsi wataweza kupata fedha zilizotengwa na serikali kwa ajili ya sekta hiyo … (Matini 11).*

Katika mfano *(62), Bw. John Mwangi* amerejelewa kupitia kiwakilishi nafsi kiambata *a-* katika neno *akiongea* mwanzoni mwa aya. Urejelezi unaojitokeza hapa ni urejelezi wa katafora kwa sababu kiwakilishi nafsi kiambata *a-* kimetumika kurejelea nomino *Bw. John Mwangi* itakayotajwa katika matini. Urejelezi wa katafora umetumika kuleta mshikamano katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza mambo yanayotendeka katika sekta ya utalii katika Kaunti ya Nakuru. Neno utalii limetumiwa na mwandishi kwa njia isiyo wazi kwa hivyo huhitaji mchakato wa akili ili kutafuta uhusiano na kupata ujumbe wa mwandishi. Ili msomaji aweze kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi, itambidi apanue maana ya neno utalii ili kukuza chukulizi zifuatazo katika kamusi ya ubongo wake:

(i) kuenda nchi ya kigeni kwa lengo la kuona

(ii) kuenda mahali fulani kama vile mbuga za wanyama kujistarehesha

(iii) kusoma yale yaliyofundishwa au kudurusu

Chukulizi zote zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea maana ya utalii kwa jumla. Ili kupata maana ya neno utalii, msomaji atachagua chukulizi zilizo na maana kulingana na muktadha wa tamko. Chukulizi (i) na (ii) zitachaguliwa na msomaji kwa sababu zinaleta maana kwa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kupitia kwa tamko husika na zina kiwango cha juu cha uhusiano. Chukulizi (iii) itataachwa kwa sababu haileti maana na haina kiwango cha juu cha uhusiano. Hivyo basi, msomaji anaweza kuelewa kulingana na muktadha na kifaa cha uhusiano kuwa neno utalii lina maana ya kuenda nchi ya kigeni kwa lengo la kuona au kuenda mahali fulani kama vile mbuga za wanyama ili kujistarehesha wala sio kusoma yale yaliyofundishwa au kudurusu.

Mhimili wa maana matini umetumiwa kuonyesha uhusiano wa kimaana katika sentensi. Kwa mfano, ufasiri wa maana ya kiwakilishi nafsi kiambata *a-* katika neno *akiongea* unategemea nomino Bw. John Mwangi inayojitokeza katika sentensi hiyo.

### 3.3 Urejelezi wa Kuashiria

Urejelezi wa kuashiria huonyesha mahali ambapo mtu, jambo au kitu kipo kwa mkabala wa mzungumzaji. Urejelezi wa kuashiria umetumika na waandishi wa *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(63) Watu wawili wenye akili taahira wanashughulikiwa na shirika moja la kutoa msaada baada ya kubainika kuambukizwa maradhi ya virusi vya Corona katika mtaa wa Majengo, Mombasa.*

*Wawili hao ni miongoni mwa wagonjwa wengine 15 wenye akili punguani waliochukuliwa kutoka maeneo mbalimbali kutoka kaunti hiyo mwezi iliyopita katika kaunti hiyo mwezi uliopita.*

*Akizungumza na Taifa Leo, Mwenyekiti wa shirika la Women Empowerment Network ambaye amekuwa akishughulikia na kupigania haki za wagonjwa wa akili katika kaunti hiyo, alisema walipokea matokeo hayo baada ya kaunti kuwapima watu hao 15 …*

*(Matini 2).*

Watu wawili wenye akili timamu ambao walikuwa wameambukizwa virusi vya Corona katika mtaa wa Majengo, Mombasa wamerejelewa kianafora katika mfano (63) kupitia matumizi ya kivumishi kiashiria *hao*. Vilevile, watu 15 kutoka maeneo mbalimbali kutoka Kaunti ya Mombasa waliopimwa kuchunguzwa kama walikuwa na virusi vya Corona wamerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi kiashiria *hao*. Kaunti ya Mombasa imerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi cha kuashiria *hiyo*.

Matokeo ya uchunguzi wa watu 15 wenye akili taahira kutoka maeneo mbalimbali kutoka Kaunti ya Mombasa ili kubainisha kama walikuwa wameambukizwa maradhi ya virusi vya Corona yamerejelewa kupitia matumizi ya kivumishi kiashiria *hayo*. Watu wawili wenye akili taahira kutoka mtaa wa Majengo, Mombasa walipatikana kuwa walikuwa wameambukizwa virusi vya Corona. Watu hao wawili wenye akili taahira

wanashughulikiwa na shirika moja la kutoa msaada baada ya kubainika kuambukizwa maradhi ya virusi vya Corona.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa kuelezea mambo yanayotendeka katika Kaunti ya Mombasa. Neno taahira limetumika kwa maana tambuzi. Neno hili ndilo linalobeba maana kuu kwa sababu linabeba mada ya matini hii. Mwandishi ametumia neno taahira kwa njia isiyo wazi. Ili kufikia maana ya neno taahira, itambidi msomaji kupanua maana neno taahira kwa kutumia kamusi ya ubongo wake ili kukuza chukulizi zifuatazo ya dhana taahira:

(i) kuchelewa

(ii) mtu asiyekuwa na akili razini

Chukulizi hizi mbili zilizoorodheshwa zinarejelea neno taahira kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya msemaji na msikilizaji. Msomaji atachagua tu chukulizi zinazofaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko na kiwango cha uhusiano. Chukulizi (ii) itachaguliwa ilhali chukulizi (i) itaachwa. Chukulizi (ii) inaleta maana na ina kiwango cha juu cha uhusiano ilhali chukulizi (i) itaaachwa kwa sababu haina maana na haina kiwango cha juu cha uhusiano. Msomaji ataweza kuelewa kulingana na muktadha na kifaa cha uhusiano kuwa taahira ina maana ya mtu asiyekuwa na akili razini wala sio kuchelewa. Mhimili wa maana matini umetumiwa kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano, kivumishi *hao* katika aya ya pili kinawarejelea *watu wawili wenye akili taahira* waliokuwa wametajwa katika aya ya kwanza. Ili kuelewa maana ya kivumishi *hao*, *hiyo* na *hayo* itambidi msomaji arejelee *watu wawili wenye akili taahira*, *Kaunti ya Mombasa* na *matokeo* ya wagonjwa 15 wenye akili punguani waliochukuliwa waliokuwa wametajwa awali katika matini.

*(64) Wazee wa Kaya katika Kaunti Ndogo ya Rabai, Kaunti ya Kilifi, wamelalamikia uharibifu wa msitu wa Kaya Bomu unaotekelezwa na watu wanaochoma makaa. Wakizungumza na wanahabari katika eneo la Rabai wakiongozwa na Bw. Kwasho Koba, walisema tangu serikali ilipopiga marufuku wazee kuingia katika misitu kufutia mlipuko wa virusi vya corona, baadhi ya wakazi wa sehemu hiyo wameanza kuharibu msitu huo.*

*Wazee hao wanataka Idara ya Misitu nchini kuangalia kati ya kusaidia kuhifadhi msitu huo kwani wanahofia iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa dhidi kuulinda huenda ukamalizwa kabisa.*

*Kwa upande wake, Bw. Shitanda ameitaka Idara ya Polisi katika kaunti hiyo kuimarisha usalama hadi katika maeneo ya mashinani ili kuzima wahalifu wanaotekeleza mauaji ya wazee eneo hilo… (Matini 9).*

Msitu wa Kaya Bomu umerejelewa kianafora kupitia kivumishi cha kuashiria *huo* katika mfano (64). Msitu huo ulikuwa umeharibiwa na watu wanaochoma makaa. Sehemu ya Rabai pia imerejelewa kianafora kupitia kiwakilishi cha kuashiria *hiyo*. Vilevile, wazee wa Kaya wamerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kiwakilishi cha kuashiria *hao*. Kaunti ya Kilifi imerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi kiashiria *hiyo*. Msitu wa Kaya Bomu unapatikana katika Kaunti ya Kilifi. Eneo la Kilifi limerejelewa kupitia kivumishi cha kuashiria *hilo*.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa na mwandishi kuelezea uharibifu wa msitu wa Kaya Bomu unaotekelezwa na watu wanaochoma makaa katika Kaunti Ndogo ya Rabai, Kaunti ya Kilifi. Mwandishi ametumia neno msitu kwa njia iliyo wazi kwa hivyo maana yake imebanwa. Ili msomaji apate maana msitu, atalazimika kufasiri maana iliyosimbwa katika neno msitu moja kwa moja kutumia kamusi ya ubongo wake. Msomaji ataweza kung'amua kuwa msitu unaorejelewa katika matini ni mahali pana miti mingi, nyasi na vichaka.

Isitoshe, mhimili wa maana matini umetumiwa kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Kwa mfano, vivumishi viashiria *huo, hiyo, hao,* na *hilo* vimetumika kurejelea nomino *msitu wa Kaya Bomu, sehemu ya Rabai, wazee wa Kaya, Kaunti ya Kilifi* na *eneo la Kilifi* zilizokuwa zimetajwa katika aya zilizotangulia. Urejelezi wa kianafora umetumika ili kuonyesha mahali, jambo au watu wanaozungumziwa katika matini. Isitoshe, vivumishi vya kushiria *huo, hiyo, hao* na *hilo* vimetumika kianafora ili kuleta mshikamano katika matini.

### 3.4 Urejelezi wa Kulinganisha

Urejelezi wa kulinganisha hutumiwa kuonyesha hali ya kufanana au kutofanana kwa vitu viwili au zaidi. Urejelezi huu, ukilinganishwa na urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria haujatumika sana katika *Habari za Kaunti*. Kwa mfano:

*(65)* *Viongozi watatu wa chama cha ODM wamekanusha madai kuwa mageuzi ya kikatiba yanayotarajiwa kutekelezwa chini ya ripoti ya Mpango wa Maridhiano (BBI), yanalenga kubuni nafasi za kisiasa kwa viongozi wanaoshindwa kwenye uchaguzi.*

*Watatu hao ni Kiongozi wa Wachache kwenye Seneti, Seneta James Orengo, Seneta Moses Kajwang' (Homa bay) na mbunge Otiende Amollo (Rarieda).*

*…*

*"Viongozi wanaoendesha kampeni za kuipinga ripoti wanapaswa kukoma. Tunataka Kenya kuwa na amani hata baada ya uchaguzi. Hili linaweza tu kufanikishwa kupitia mageuzi ya kikatiba yaliyojumuishwa kwenye ripoti. Mpango huo ni kama gari la moshi ambalo haliwezi kusimamishwa na yeyote," akasema Bw. Kajwang … (Matini 23).*

Katika mfano (65), mpango wa BBI unalinganishwa na gari la moshi kama inavyodhihirika katika sentensi '*Mpango wa BBI ni kama gari la moshi ambalo haliwezi kusimamishwa na yeyote…*' Msemaji anamaanisha kuwa mpango wa BBI hauwezi kusimamishwa na mtu yeyote kwa sababu ulikuwa umeanza. Urejelezi wa kulinganisha haujatumika sana katika *Habari za Kaunti* kwa sababu hauchangii katika kuleta mshikamano katika matini ukilinganishwa na urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza mambo yanayohusiana na Mpango wa Maridhiano. Mpango huu umelinganishwa na gari la moshi. Neno gari la moshi limetumika kwa maana tambuzi. Neno gari la moshi linabeba maana kuu kwa sababu linafafanua Mpango wa Maridhiano. Neno hili limetumika kwa njia iliyo wazi. Msomaji atafasiri maana ya neno gari la moshi kwa kutumia mkakati wa kubana. Katika mkakati huu, msomaji atafasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno gari la moshi. Msomaji atakuwa na sifa zifuatazo zinazorejelea dhana ya gari la moshi akilini mwake:

(i) gari refu

(ii) linatumia reli

(iii) linaendeshwa kwa kasi

(iv) linasimama tu katika vituo fulani

(v) linatoa moshi

Sifa hizi zote zinarejelea gari la moshi kwa jumla. Msomaji atachukua sifa zote zilizoorodheshwa hapo juu kurejelea dhana ya gari la moshi. Maana ya kihali inayopatikana kutokana na muktadha wa tamko ni kuwa Mpango wa Maridhiano, kama gari la moshi linaloendeshwa kwa kutumia reli kwa kasi na kutoa moshi, haliwezi kusimamishwa na mtu yeyote bali litasimama tu katika kituo fulani au mwishoni mwa safari.

*(66) Kundi la wataalamu kutoka eneo la Magharibi nchini wanaounga handisheki mkono wameanza vikao vya kuhamazisha wakazi kuhusu Mpango wa Maridhiano wa BBI, kabla ya kuchapishwa rasmi kwa nakala ya mwisho.*

*…*

*Zoezi hilo lililofanya na kundi hili la wataalamu ni sawa na mchakato ambao ulifanywa na Gavana wa Kakamega, Wycliffe Oparanya na Waziri wa Ugatuzi, Eugine Wamalwa mwezi uliopita, na kusababisha mzozo wa kisiasa katika eneo hilo, ambalo lina wapiga kura wengi … (Matini 18).*

Mkutano uliofanywa na kundi la wataalamu kutoka eneo la Magharibi nchini wanaounga mkono maridhiano umelinganisha (kupitia matumizi ya neno *sawa na*) na mchakato ambao ulifanywa na Gavana wa Kakamega, Wycliffe Oparanya na Waziri wa Ugatuzi, Eugine Wamalwa mwezi uliopita, na kusababisha mzozo wa kisiasa katika eneo hilo.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza kuhusu maridhiano. Neno maridhiano limetumika na mwandishi kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji aweze kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi, itambidi kufasiri maana ya neno maridhiano kwa kutumia mkakati wa upanuzi ili kukuza chukulizi zifuatazo ya dhana ya maridhiano:

(i) maafikiano baina ya watu kutoka jamii mbalimbali katika nchi

(ii) maafikiano baina ya mataifa mbalimbali

Chukulizi hizi zinarejelea maana ya maridhiano kwa jumla. Ili msomaji apate maana iliyokusudiwa na mwandishi, atambidi kuchunguza chukulizi zilizokuzwa kupitia kwa dhana maalum ya kihali. Msomaji atachagua chukulizi (i) kwa sababu inaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na kiwango cha uhusiano. Chukulizi (ii) itaachwa kwa sababu haileti maana kulingana na muktadha wa tamko na haina kiwango cha juu cha uhusiano. Maana ya neno maridhiano itakayopatikana ni maafikiano baina ya watu kutoka jamii mbalimbali nchini Kenya wala sio maafikiano baina ya mataifa mbalimbali.

### 3.5 Ubadilishaji

Ubadilishaji ni hali ya neno kuchukua nafasi ya neno lingine katika matini. Ubadilishaji hutumika na msemaji wakati hataki kurudia neno fulani katika matini. Neno linalochukua nafasi ya neno lingine lina maana sawa na neno hilo. Katika ubadilishaji, ufasiri wa maana ya maneno ambayo nafasi yao yamechukuliwa na maneno mengine katika matini humhitaji msomaji kurejelea maneno yaliyotajwa katika sehemu ya matini iliyotangulia. Ubadilishaji umetumika katika *Habari za Kaunti*. Kwa mfano:

*(67) Rais Uhuru Kenyatta amepuuzilia mbali madai kuwa anapania kutumia mabadiliko ya Katiba kuendelea kusalia mamlakani baada ya 2002.*

*…*

*Kiongozi wa taifa alisema lengo la Mpango wa Maridhiano (BBI), na mageuzi yanayopendekezwa kwayo, ni kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo havikabiliwi na baadhi ya changamoto zinazokumba kizazi cha sasa (Matini 10).*

Nomino *kiongozi wa taifa* imechukua nafasi ya nomino *Rais Uhuru Kenyatta* iliyokuwa imetajwa katika matini katika mfano (67). Huu ni urejelezi wa kianafora. Ubadilishaji wa nomino umetumika katika matini kupitia matumizi ya cheo (kiongozi wa taifa) kumrejelea Rais Uhuru Kenyatta ambaye alikuwa ametajwa hapo awali katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika na mwandishi kueleza kuhusu Mpango wa Maridhiano unaoelezwa na Rais Uhuru Kenyatta ambaye ni kiongozi wa taifa la Kenya. Neno rais limetumika na mwandishi kwa njia isiyo wazi. Neno hili lina maana zaidi ya moja. Ili msomaji aweze kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi, itambidi kupanua maana leksika ya neno rais hadi kwa maana zinazokuzwa na muktadha ambamo neno hili limetumika. Kutokana na upanuzi huo, chukulizi zifuatazo zitakuzwa ya dhana ya rais:

(i) kiongozi wa nchi ambayo ni jamhuri

(ii) kiongozi ambaye amechaguliwa kusimamia kampuni, chama au shirika.

Chukulizi hizi zinarejelea maana ya rais kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya msomaji na mwandishi. Ili kupata maana ya neno rais, msomaji atachagua tu chukulizi zinazofaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Msomaji atachagua chukulizi (i) na kuacha chukulizi (ii) kwa sababu chukulizi (i) ina maana katika usemi husika ilhali chukulizi (ii) haina maana katika usemi husika. Msomaji anaweza kuelewa kulingana na muktadha na kiwango cha uhusiano kuwa neno rais lina maana ya kiongozi wa nchi ambayo ni jamhuri wala sio kiongozi ambaye amechaguliwa kusimamia kampuni, chama au shirika.

Vilevile, mwandishi ametumia mhimili wa maana matini kuonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana baina ya aya moja na aya nyingine. Ufasiri wa maana ya nomino *kiongozi wa taifa* unategemea nomino *Rais Uhuru Kenyatta* ambayo ilikuwa imetajwa awali. Urejelezi wa kianafora umetumika ili kuleta mshikamano katika matini.

*(68) Serikali ya Kaunti ya Kwale, inashirikiana na afisi ya Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI), kupambana na ongezeko la visa vya kaunti hiyo.*

*Gavana Salim Mvurya alisema utawala wake utasaidia DCI kuwanasa wahusika katika uovu huo ili waadhibiwe kwa mujibu wa sheria.*

…

> *Mkuu huyo wa Kaunti alisema hayo wakati ambapo zaidi ya familia 2,000 zinazoishi katika mpango wa makazi kwa jina "Sheep and Goats Settlement Scheme" kaunti ndogo ya Matuga, zinakabiliwa na tishio la kufurushwa baada yawatu wenye ushawishi kunyakua sehemu kubwa ya ardhi hiyo (Matini 27).*

Kirai nomino *Mkuu huyo wa Kaunti* imechukua nafasi ya nomino *Gavana Salim Mvurya* ambayo ilikuwa imetajwa katika matini katika mfano (68). Huu ni urejelezi wa kianafora. Ili kufasiri maana ya *Mkuu huyo wa Kaunti,* msomaji atalazimika kurejelea nomino *Gavana Salim Mvurya* iliyokuwa imetajwa katika aya ya pili. Ubadilishaji wa nomino umetumika katika matini kupitia matumizi ya cheo (*Mkuu huyo wa Kaunti*) kumrejelea *Gavana Salim Mvurya* ambaye alikuwa ametajwa katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika kuleta mshikamano katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa na mwandishi kueleza mambo yanayotendeka katika Kaunti ya Lamu. Neno Gavana limetumika kwa maana tambuzi. Neno hili linabeba maana kuu kwa sababu ndilo linalorejelewa katika matini. Ili msomaji afasiri maana ya Gavana, itambidi apanue neno hili ili kupata chukulizi zifuatazo ya dhana ya Gavana zinazokuzwa na neno hili:

(i) mkuu wa jimbo au gatuzi
(ii) kiongozi mkuu wa Benki Kuu ya nchi fulani
(iii) mwakilishi wa mfalme au malkia katika koloni

Chukulizi hizi zinarejelea maana ya gavana kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya msomaji na mwandishi. Ili kupata maana ya neno gavana, msomaji atachagua chukulizi zilizo na maana kulingana na muktadha wa tamko. Chukulizi (i) zitachaguliwa na msomaji ilhali chukulizi (ii) na (iii) zitaachwa kwa sababu hazileti maana kulingana na muktadha na kiwango cha uhusiano. Msomaji anaweza kuelewa kulingana na dhana maalum ya kihali kuwa neno gavana linalorejelewa katika matini lina maana ya kiongozi wa jimbo wala sio mwakilishi wa mfalme au malkia katika koloni au kiongozi mkuu wa Benki Kuu ya nchi fulani.

Mhimili wa maana matini umetumiwa na mwandishi ili kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Ufasiri wa maana ya *Mkuu huyo wa Kaunti* unategemea *Gavana Salim Mvurya* ambaye alikuwa ametajwa katika matini. Nomino *Gavana Salim Mvurya*

imebadilishwa na nomino *Mkuu huyo wa Kaunti*. Ubadilishaji unaojitokeza hapa ni ubadilishaji wa nomino. Kwa hivyo, ubadilishaji umetumika kianafora ili kuleta mshikamano na kuondoa urudiaji katika matini.

### 3.6 Udondoshaji

Udondoshaji unahusu kuacha baadhi ya maneno katika sentensi ili kupunguza urudiaji. Neno linaloachwa linachukuliwa kuwa linaeleweka kwa wasomaji kwa sababu lilikuwa limetajwa katika matini. Kwa hivyo, udondoshaji ni aina ya urejelezi wa kianafora. Kwa mfano:

(69) *Familia saba katika kijiji cha Kisii mjini Thika, Kaunti ya Kiambu, wamefungiwa nyumba zao baada ya landilodi kudai hawajalipa kwa miezi miwili.*

…

*Licha ya wapangaji hao kumsihi awahurumie, hawakuwa na budi kwani alikuwa ameandamana na watu waliolazimisha wapangaji kuondoka au mali zao zitupwe nje … (Matini 3).*

Katika mfano (69), neno landilodi limedondolewa ili kuondoa urudiaji. Aya hii ingekuwa: *Licha ya wapangaji hao kumsihi landilodi awahurumie, hawakuwa na budi kwani alikuwa na watu waliolazimisha wapangaji kuondoka au mali zao zitupwe.*

Nomino *landilodi* imedondolewa kwa sababu ilikuwa imetajwa katika matini. Nafasi iliyoachwa katika sentensi baada ya kudondoa nomino *landilodi* inaweza kujazwa kwa kurejelea vipashio katika sentensi iliyotangulia ili kupata neno linalofaa kuchukua nafasi hiyo. Neno litakalojaza nafasi iliyoachwa litakuwa ni nomino *landilodi* ambayo ilikuwa imetajwa awali katika matini. Udondoshaji unaojitokeza hapa ni udondoshaji wa nomino. Kwa hivyo, udondoshaji umetumiwa kianafora ili kuleta mshikamano katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika na mwandishi kueleza jinsi wapangaji walivyolazimishwa kuondoka katika kijiji cha Kisii mjini Thika, Kaunti ya Kiambu. Neno wapangaji limetumika kwa maana tambuzi. Mwandishi ametumia neno wapangaji kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji kufikia maana ya neno wapangaji, itambidi kufasiri kwa kutumia kamusi ya ubongo. Katika kamusi ya ubongo wa msomaji, chukulizi zifuatazo zitakuzwa za dhana ya wapangaji:

(i) watu wanaoishi nyumba isiyo yao na wanalipa kodi

(ii) watu wanaoweka mambo au vitu kwa utaratibu fulani

Maana hizi zinarejelea maana ya wapangaji kwa jumla. Ili kufahamu maana ya neno wapangaji, msomaji atachagua tu chukulizi ambazo zinafaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Msomaji anaweza kuelewa kulingana na dhana maalum ya kihali kuwa neno wapangaji lina maana ya watu wanaoishi nyumba isiyo yao wala sio watu wanaopanga vitu au mambo kwa utaratibu fulani. Mihimili ya kanuni fahamu na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano zimetumika na mwandishi kudokeza kauli muhimu za kumvutia msomaji ili kufahamu ujumbe uliokusudiwa na mwandishi haraka.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana matini kupitia matumizi ya udondoshaji kuonyesha kuwa ufasiri wa maana ya neno lililodondolewa (landilodi) unategemea neno lililokuwa limetajwa katika matini (landilodi). Udondoshaji umetumika kianafora ili kuondoa urudiaji na kuleta mshikamano katika matini.

*(70) Rais Uhuru Kenyatta amepuuzilia mbali madai kuwa anapania kutumia mabadiliko ya kikatiba kuendelea kusalia mamlakani baada ya 2022.*

*…*

*"Inasikitisha kuwa kuna watu wanaofasiri mageuzi ya Katiba kupitia kura ya maamuzi kuashiria kuwa ni njama ya kuongeza muhula wangu uongozini kama rais. Na wengine pia wamedai eti ninataka kuwa Waziri Mkuu. Madai haya hayana ukweli wowote," Rais Kenyatta akasema alhamisi jioni … (Matini 10).*

Katika mfano (70), neno *watu* limedondolewa kwa sababu neno hili lilikuwa limetajwa awali katika matini. Sentensi hii ingekuwa:

*Inasikitisha kuwa kuna watu wanaofasiri mageuzi ya katiba kupitia kura ya maamuzi kuashiria kuwa ni njama ya kuongeza muhula wangu uongozini kama rais. Na watu wengine pia wamedai eti ninataka kuwa Waziri Mkuu.*

Neno watu limedondolewa katika sentensi ya pili ili kuondoa urudiaji. Isitoshe, ili msomaji afahamu wanaozungumziwa katika sentensi hii, itamlazimu kurejelea sentensi iliyotangulia katika matini. Udondoshaji unaojitokeza hapa udondoshaji wa nomino.

Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza mambo yanayohusiana na mabadiliko ya katiba nchini Kenya. Neno katiba limetumika kwa maana tambuzi. Mwandishi ametumia neno katiba kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji kufikia maana ya neno katiba, itambidi kutumia mchakato wa akili ili kutafuta uhusiano na kupata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Msomaji atalazimika kupanua maana ya neno katiba ili kukuza chukulizi zifuatazo ya dhana ya katiba:

(i) kanuni zinazowezesha serikali, chama au shirika iendeshe shughuli zake

(ii) kawaida anayofuata mtu wakati anapofanya jambo fulani

Chukulizi hizi zinarejelea maana ya katiba kwa jumla. Ili kufikia maana ya neno katiba, msomaji atachagua chukulizi ambayo inafaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Hivyo basi, chukulizi (i) itachaguliwa kwa sababu inaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na ina kiwango cha juu cha uhusiano ilhali chukulizi (ii) haitachaguliwa kwa sababu haileti maana kulingana na muktadha wa tamko na haina uhusiano wa kiwango cha juu. Msomaji anaweza kuelewa kulingana na dhana maalum ya kihali kuwa neno katiba lina maana ya kanuni zinazowezesha serikali kuendesha shughuli zake wala sio kawaida anayofuata mtu wakati anapofanya jambo fulani.

Mhimili wa maana matini umetumika kupitia matumizi ya udondoshaji. Ufasiri wa maana ya neno lililodondolewa *(watu)* unategemea neno *watu* lillokuwa limetajwa katika sentensi. Udondoshaji umetumiwa ili kuondoa urudiaji katika matini. Mbali na matumizi ya udondoshaji kuleta mshikamano katika matini, uunganishaji unaweza kutumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika matini.

### 3.7 Uunganishaji

Uunganishaji ni matumizi ya neno, fungu la maneno au viambishi kuunganisha na kuonyesha uhusiano baina ya sentensi mbili au zaidi (Matei 2008). Viunganishi vimetumika katika *Habari za Kaunti* kianafora ili kuleta mshikamano na muwala katika matini. Kwa mfano:

*(71) Kiongozi wa Narc –Kenya, Bi. Martha Karua amekosoa vikali pendekezo la Rais Uhuru Kenyatta, kwamba Kenya inahitaji mabadiliko ya kikatiba ili kukabili ghasia za kikabila ambazo hutokea kila baada ya uchaguzi mkuu nchini.*

*Kwenye hotuba yake mnamo Jumatatu, wakati wa sherehe za Sikukuu ya Madaraka, Rais Kenyatta alisema kuwa mabadiliko ya kikatiba ndio njia pekee ya kuondoa taharuki za kisiasa ambazo hukumba chaguzi hizo.*

*Hata hivyo, Bi. Karua amekosoa pendekezo hilo, akishikilia kuwa ingawa hapingi marekebisho hayo, kile Wakenya wengi wanataka kuona ni utekelezaji ufaao wa katiba ya sasa …*

*(Matini 1).*

Kiunganishi *hata hivyo* katika mfano (71) kimetumika kuonyesha hoja iliyo kinyume na hoja iliyokuwa imetajwa katika aya iliyotangulia. Bi. Karua alikuwa anakosoa pendekezo la utekelezaji wa katiba lililokuwa limetolewa na Rais Uhuru Kenyatta katika aya iliyotangulia. Huu ni urejelezi wa kianafora. Kiunganishi *ingawa* kimetumika kuunganisha sentensi na kuonyesha kinyume cha kilichotajwa awali na kile kinachotajwa hivi sasa katika matini. Kwa hivyo, viunganishi *hata hivyo* na *ingawa* vimetumika kuleta mshikamano katika matini.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kueleza kuhusu mabadiliko ya kikatiba nchini Kenya. Mwandishi ametumia neno mabadiliko kwa njia iliyo wazi kwa hivyo maana yake imebanwa. Ili msomaji apate maana mabadiliko, atafasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno mabadiliko. Kupitia ubanaji, msomaji atapata kuwa neno mabadiliko lina maana ya hali inayokuwako baada ya kutokea mageuzi fulani.

Mhimili ya maana matini umetumiwa kuonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana baina ya aya katika matini. Viunganishi *hata hivyo* na *ingawa* vimetumiwa kuunganisha sentensi na aya zinazoonyesha kinyume cha kilichotajwa awali na kile kinachotajwa katika matini. Viunganishi hivi huunganisha sentensi au aya na kuleta mshikamano katika matini.

*(72)* *Watu wanane kutoka familia moja wanaodaiwa kusafiri mjini Isiolo kutoka mtaa wa Eastleigh, jijini Nairobi, wamesukumwa karantini kwa lazima.*

*Wanane hao ambao walikuwa wakisafiria gari aina ya Land Cruiser walilokuwa wamekodisha, walinaswa na polisi wanaosimamia kizuizi cha barabara katika Uwanja wa Ndege wa Isiolo.*

*Vile vile, walikuwa wamebeba mizigo. Polisi waliwaweka kwenye karantini mara moja kwa kukosa stakabadhi zifaazo za usafiri… (Matini 12).*

Katika mfano (72) kiunganishi *vile vile* kimetumika kuunganisha hoja katika aya moja na nyingine na kuleta mshikamano katika matini. Kiunganishi *vile vile* kimetumiwa kuongeza habari zaidi katika habari ambazo zilikuwa zimetolewa katika aya zilizotangulia. Watu wanane kutoka familia moja walionaswa na polisi wanaosimamia kizuizi cha barabara katika uwanja wa ndege wa Isiolo pia walikuwa wamebeba mizigo katika gari lao aina ya Land Cruiser.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kueleza kuhusu watu wanane kutoka familia mmoja waliokuwa wakisafiri kutoka Kaunti ya Nairobi hadi Kaunti ya Isiolo. Neno familia limetumika kwa maana tambuzi. Neno hili limetumika na mwandishi kwa njia isiyo wazi. Msomaji atahitajika kutumia mchakato wa kiakili wa kupanua maana ya neno hili ili kukuza chukulizi zifuatazo za dhana ya familia:

(i) watu wenye uhusiano wa kinasaba

(ii) baba na mama

(iii) baba, mama na wana

(iv) mama na wana

(v) mama, baba, wana, nyanya na babu

Chukulizi hizi zote zinarejelea maana ya familia kwa jumla. Ili kufikia maana ya neno familia, msomaji atateua chukulizi zinazofaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Chukulizi (i) itachaguliwa kwa sababu inaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na ina uhusiano wa kiwango cha juu. Chukulizi (ii) hadi (v) zitaachwa kwa sababu hazileti maana kulingana na muktadha wa tamko na haina uhusiano wa kiwango cha juu. Maana itakayopatikana kutokana na dhana maalum ya kihali ni kuwa familia ni watu wenye uhusiano wa kinasaba wala sio baba na mama, baba, mama na mwana, mama na wana, au mama, baba, wana, nyanya na babu.

Mhimili wa maana matini umetumika kuonyesha jinsi aya zilivyounganishwa ili kuleta uhusiano wa kimaana. Kiunganishi *vile vile* kimetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana kati ya aya ya pili na aya ya tatu na kuongeza habari zaidi ambazo zilikuwa zimetolewa katika aya zilizotangulia. Mbali na watu wanane kutoka familia mmoja waliokuwa wametajwa katika aya ya kwanza kusafiria gari aina ya Land Cruiser, vile vile walikuwa wamebeba mizigo katika gari hilo.

### 3.8 Urudiaji wa Nomino Muhimu

Urudiaji ni matumizi ya neno zaidi ya mara moja katika matini. Urudiaji hutambulika kupitia maneno yaliyotumiwa katika matini. Urudiaji wa nomino muhimu umetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*(73) Wakuzaji kahawa kutoka Kaunti za Embu na Meru wametoa wito kwa Wizara ya Kilimo kufanya ukaguzi wa vitabu vya uhasibu katika vyama vya ushirika kama njia ya kutokomeza ufisadi uliokithiri katika sekta hiyo.*

*Wakulima hao wanadai kwamba baadhi ya maafisa wa vyama hivyo hushirikiana na wauzaji wa kahawa kuwafilisi pesa zao.*

*Aidha wakulima hao wamependekeza vyama vya ushirika ambavyo haviwezi kujisimamia kiuchumi, vuinganishwe ili kuwaepushia wakulima gharama ya kuviendesha.*

*…*

*"Wengi wa maafisa hawajapokea mafunzo ilhali wao ndio husimamia pesa za wakulima. Hawana ofisi na sioni haja ya wao kuendelea kuwabebesha wakulima mizigo ya kugharamia shughuli zao," akasema Bw. Ireri.*

*Kinachomtia hofu zaidi Bw. Ireri ni kwamba maafisa hao hukopa fedha kutoka benki bila kuwashauri wakulima (Matini 21).*

Nomino *wakulima* imerudiwa katika mfano (73) ili kuonyesha kuwa aya zenye uhusiano wa kimaana. Urudiaji wa nomino unachangia kuleta mshikamano kwa sababu unaonyesha nomino inayozungumziwa katika matini. Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kueleza kuhusu ukuzaji wa kahawa katika Kaunti za Embu na Meru. Neno kahawa limetumika kwa maana tambuzi. Neno hili lina maana nyingi. Ili msomaji afasiri maana ya kahawa, itambidi atumie mkakati wa upanuaji. Kupitia upanuzi huu, kamusi ya ubongo wa msomaji itakuza chukulizi zifuatazo ya dhana ya kahawa:

(i) tunda au mbegu ya mbuni

(ii) unga wa mbegu za buni zilizokaangwa

(iii) kinywaji kinachotengenezwa kwa unga wa buni na maji

Chukulizi hizi zote zinarejelea maana ya kahawa kwa jumla. Ili kupata maana ya neno kahawa, msomaji atachagua tu chukulizi ambazo zinafaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano. Hivyo, msomaji atachagua

chukulizi (i) kwa sababu inaleta maana iliyokusudiwa na mwandishi kwa msomaji kulingana na muktadha wa tamko na ina uhusiano wa hali ya juu. Chukulizi (ii) na (iii) zitaachwa kwa sababu hazileti maana kulingana na muktadha wa tamko na hazina uhusiano wa kiwango cha juu. Msomaji ataweza kupata maana kuwa kahawa inayorejelewa ni tunda au mbegu ya mbuni wala sio unga wa mbegu za buni zilizokaangwa au kinywaji kinachotengenezwa kwa unga wa buni na maji.

Mhimili wa maana matini umetumiwa kuleta uhusiano wa kimaana katika matini. Kwa mfano, nomino *wakulima* imerudiwa ili kuonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana katika matini. Urudiaji wa neno wakulima utawahakikishia wasomaji kuwa wanafuata maendeleo ya matini.

*(74)* *Waziri msaidizi wa Utumishi wa Umma, Vijana na Jinsia, Bi. Rachael Shebesh amelaumu jamii ya Abagusii kwa kukosa kuripoti visa vya ukeketaji.*

*...*

*Kulingana na Bi. Shebesh, wazazi wengi maeneo hayo wamekuwa wakiendesha ukeketaji kisiri wakati shule zimefungwa kwa ushirikiano na madaktari wanaomiliki kliniki za kibinafsi au hata madaktari wanaohudumu katika hospitali za serikali ambao huitwa nyumbani waliko watoto kwa lengo la kujipatia hela.*

*Bi. Shebesh alipuzilia mbali mbali dhana miongoni mwa jamii ya Abagusii kwamba, mtoto wa kike asipokeketwa, atageuka kiruka njia atakapoolewa eti atakuwa na hamu ya kufanya ngono isiyoweza kudhibitiwa kwa urahisi… (Matini 15).*

Nomino *Bi. Shebesh* imerudiwa katika mfano (74) ili kuleta mshikamano katika matini kwa sababu inaonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana katika matini. Isitoshe, urudiaji wa nomino hii unasaidia msomaji kufuatilia matukio kutoka aya moja hadi nyingine. *Bi shebesh* alikuwa amezuru Kaunti za Nyamira na Kisii ambazo zimekuwa zikiendesha ukeketaji. *Bi. Shebesh* alipuzilia mbali dhana miongoni mwa jamii ya Abagusii kuwa mtoto wa kike asipokeketwa atageuka kiruka njia.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa na mwandishi kueleza kuhusu ukeketaji wa watoto wa kike uliokithiri katika Kaunti za Nyamira na Kisii. Neno ukeketaji limetumika kwa maana tambuzi. Mwandishi ametumia neno ukeketaji kwa njia iliyo wazi kwa hivyo maana yake imebanwa. Ili msomaji apate maana ukeketaji, atalazimika kufasiri maana iliyosimbwa katika neno ukeketaji moja kwa moja. Msomaji atafasiri ubongoni mwake kuwa ukeketaji unaorejewa kupitia kivumishi kiashiria *huo* katika matini ni tendo la kutahiri mwanamke.

Mhimili wa maana matini umetumiwa na mwandishi kupitia matumizi ya urudiaji wa nomino *Bi. Shebesh*. Urudiaji wa nomino *Bi. Shebesh* unaonyesha kuwa kuna uhusiano wa kimaana katika matini. Pia urudiaji wa nomino *Bi. Shebesh* umetumika kubainisha mzungumzaji anayerejelewa katika matini.

**Hitimisho**

Katika sura ya tatu, tumebainisha aina mbalimbali za urejelezi na namna zinavyochangia kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha umetumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Vile vile, tumebainisha kuwa mbali na matumizi ya urejelezi wa kiendofora, urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kuashiria kuleta mshikamano katika matini, vipashio kama vile urudiaji wa nomino muhimu, uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji vimetumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Aidha, tumebainisha kuwa mhimili wa maana matini wa nadharia ya Sarufi Amilifu inaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa kutumia urejelezi katika kuleta mshikamano katika matini. Kwa vile nadharia ya Sarufi Amilifu haifafanui mchakato wa kufikia maana tambuzi, mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya Nadharia ya Uhusiano imetumika kuziba pengo hili.

Mhimili wa kanuni tambuzi umetumika kutathmini jinsi wasomaji wanavyotumia akili tambuzi kufasiri ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kwa kurejelea muktadha wa tamko husika na kiwango cha uhusiano. Mhimili wa kanuni mawasiliano umetumika kutathmini ufaafu wa ujumbe unaopitishwa na mwandishi kwa msomaji. Imedhihirika kuwa tamko lolote linalotolewa na msemaji linafaa kukuza matarajio fulani kwa msikilizaji kuwa tamko hilo lina umuhimu kwao na linafaa kutiliwa maanani ili kupata ujumbe unaolengwa na msemaji. Michakato ya kufasiri maana iliyokusudiwa na msemaji hukoma wakati ambapo msikilizaji anapata au anakosa uhusiano wa tamko wa msemaji.

Imedhihirika pia kuwa matumizi ya matamko kwa njia wazi huwa na uhusiano bora zaidi kuliko matumizi ya matamko kwa njia isiyo wazi. Matamko yanayotolewa kwa njia isiyo wazi huwa na gharama kubwa ya mchakato na kiwango cha chini cha uhusiano ilhali matamko yaliyotolewa kwa njia iliyo wazi huwa na gharama ndogo ya mchakato na kiwango cha juu cha uhusiano.

Isitoshe, mhimili wa maana matini umetumiwa kutathmini jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* wametumia urejelezi kuunganisha maana kutoka sentensi au aya moja hadi nyingine ili kuleta mshikamano katika matini. Urejelezi, uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji ni vipengele vya mshikamano ambavyo vimetumiwa na waandishi mbalimbali wa *Habari za Kaunti*.

# SURA YA NNE

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikusudia kubainisha aina za urejelezi katika *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo* na kubainisha iwapo nadharia ya Sarufi Amilifu inaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa urejelezi katika kuleta mshikamano. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) imetumika katika utafiti huu kwa kuangazia mtazamo wa Halliday (1976). Isitoshe, utafiti huu ulikusudia kubainisha iwapo nadharia ya Uhusiano inayohusishwa na Carson (2002), Wilson na Sperber (2002) na Wilson (2003) inaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa urejelezi katika kuleta mshikamano katika matini.

Utafiti huu umebainisha kuwa urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha umetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano. Vilevile, imebainika kuwa vijenzi vya mshikamano kama vile urudiaji, uunganishaji, udondoshaji na ubadilishaji vimetumika kiurejelezi katika matini ili kuleta mshikamano. Utafiti huu pia umebainisha kuwa mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano zimetumika na waandishi kudokeza kauli muhimu za kumvutia wasomaji ili kufahamu ujumbe uliokusudiwa na mwandishi haraka.

## 4.2 Muhtasari

Utafiti huu umechunguza na kubainisha aina za urejelezi zilizotumika katika *Habari za Kaunti*. Pia utafiti huu umebainisha namna aina mbalimbali za urejelezi zilizotumika kuleta mshikamano katika *Habari za kaunti*. Isitoshe, utafiti huu umebainisha kuwa nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Uhusiano zinaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa kutumia urejelezi kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Katika sura ya kwanza, tumeweka msingi utafiti wetu kwa kueleza usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti. Sura ya pili ilifafanua vipengele muhimu vinavyochangia kuleta mshikamano katika matini. Vipengele vilivyofafanuliwa ni vijenzi vya mshikamano wa kileksia na mshikamano ya kisarufi.

Vijenzi vya mshikamano vya kileksia vilivyofafanuliwa ni matumizi ya sinonimu, matumizi ya haiponimu na urudiaji wa nomino muhimu. Urejelezi, uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji ni vijenzi vya mshikamano vya kisarufi vilivyofafanuliwa. Aidha, urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi wa kieksofora, urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha vimefafanuliwa. Katika ufafanuzi huu, imebainika kuwa vipashio kama vile uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji huweza kutumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika matini. Isitoshe, ilibainika kuwa urejelezi wa kieksofora hauchangii katika kuleta mshikamano katika matini kwa sababu ufasiri wake haujikiti katika matini.

Katika sura ya tatu, tumeonyesha jinsi aina mbalimbali za urejelezi zilivyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora) umejadiliwa kwa kina na kwa kufanya hivi, imebainika kuwa urejelezi wa kiendofora unachangia katika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Urejelezi nafsi hubainika katika matini kupitia matumizi ya viwakilishi nafsi huru, viwakilishi nafsi viambata, viwakilishi ngeli, viwakilishi vimilikishi na vivumishi vimilikishi.

Vile vile, tumefafanua jinsi urejelezi wa kuashiria ulivyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Katika ufafanuzi huu, imebainika kuwa vivumishi viashiria vimetumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika matini. Imebainika kuwa vivumishi viashiria hufanya kazi ya kuonyesha kama kitu au mtu yuko karibu, mbali kidogo (wastani) au mbali sana. Mzizi {h-} hutumika kuashiria vitu vilivyo karibu ilhali mzizi {-le} hutumika kuashiria vitu vilivyo mbali. Viambishi vinavyoambatanishwa na mizizi hiyo hutegemea ngeli ya nomino husika katika sentensi.

Aidha, tumebainisha jinsi urejelezi wa kulinganisha ulivyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Hata hivyo, utafiti huu umeonyesha kuwa urejelezi wa kulinganisha haujatumika sana kuleta mshikamano katika matini ikilinganishwa na urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria. Urejelezi wa kulinganisha umedhihirika kupitia matumizi ya maneno ya kulinganisha kama vile *sawa na* pamoja na *kama*.

Mhimili wa maana matini wa nadharia ya Sarufi Amilifu umebainisha kuwa urejelezi unaweza kutumika kuleta mshikamano katika matini. Imebainika kuwa mhimili wa maana tambuzi haufafanui utaratibu wa kufuatwa katika ufasiri wa ujumbe katika matini. Ili

kuziba pengo hili, mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano zimetumika kuchanganua data katika utafiti huu. Mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano imebainisha kuwa urejelezi wa kiakili unaweza kutumika kuleta mshikamano kupitia urejelezi wa muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano.

### 4.3 Hitimisho

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo.* Utafiti huu umeonyesha kwamba urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria umetumika. Urejelezi wa kulinganisha haukutumika sana. Aidha, vijenzi vya mshikamano kama vile urudiaji wa nomino muhimu, uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji vimetumika kiurejelezi katika matini.

Madhumuni yetu ya pili yalikuwa ni kubainisha jinsi urejelezi unavyotumika kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo.* Ilibainika kuwa urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria na kulinganisha umetumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Vile vile, vijenzi vya mshikamano kama vile urudiaji wa nomino muhimu, uunganishaji, ubadilishaji na udondoshaji vimetumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Madhumuni ya tatu yalikuwa ni kubainisha iwapo nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Uhusiano zinaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa kutumia urejelezi kuleta mshikamano katika gazeti la *Taifa Leo*. Mhimili wa maana matini wa nadharia ya Sarufi Amilifu umebainisha kuwa matini zilizoandikwa na waandishi mbalimbali zimeshikana pamoja na kuhusiana kulingana na muktadha kupitia matumizi ya urejelezi. Waandishi mbalimbali wametumia mhimili wa maana matini kujenga matini na kufanikisha mawasiliano ya kimaana. Vipengele kama vile viunganishi, urejelezi, udondoshaji na ubadilishaji vimetumika pamoja ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Viunganishi kama vile viunganishi viongezi, viunganishi vya kuonyesha sababu, viunganishi vya kuonyesha kinyume, viunganishi vya kuonyesha chaguo, viunganishi vya kuonyesha masharti na viunganishi vitegemezi vimetumika kuleta mshikamano katika matini.

Utafiti huu umeonyesha kuwa nadharia ya Sarufi Amilifu haifafanui utaratibu wa kufikia maana tambuzi. Ili kufidia upungufu huu, mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano imetumika katika utafiti huu. Mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano imetumika na waandishi mbalimbali kudokeza kauli muhimu za kuwavutia wasomaji ili kufahamu ujumbe uliokusudiwa na mwandishi haraka. Ili msomaji afasiri maana iliyokusudiwa na mwandishi, inambidi kurejelea chukulizi zinazokuzwa akilini mwake kupitia dhana maalum ya kihali. Chukulizi zilizo na maana kwa ujumbe unaokusudiwa na mwandishi kwa msomaji na zilizo na uhusiano wa hali juu zitachaguliwa ilhali chukulizi ambazo hazileti maana kwa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kwa msomaji na zilizo na uhusiano wa kiwango cha chini zitapuuzwa. Kutokana na maelezo haya, inadhihirika kuwa msomaji hutumia urejelezi fulani alionao akilini mwake ili kupata ujumbe wenye mshikamano.

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa urejelezi ni kiungo muhimu katika kujenga matini na kufanikisha mawasiliano ya kimaana. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) na Nadharia ya Uhusiano ya Wilson na Sperber (2002) na Wilson (2003) zinaweza kutumika kufasiri maana ya aina mbalimbali za urejelezi zinazochangia kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti* kwa kuangazia mtazamo wa Halliday (1976).

## 4.4 Mapendekezo

Utafiti wetu umejikita katika kuchunguza namna urejelezi ulivyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo*. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu yafuatayo:

Kwanza, utafiti unaweza kufanywa kuhusu matumizi ya urejelezi kuleta mshikamano katika *Tahariri* katika gazeti la *Taifa Leo*. Vilevile, utafiti huu umejikita katika mihimili miwili ya Sarufi Amilifu: Maana tambuzi na maana matini. Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kwa kutumia mhimili wa maana husishi.

Pili, tunapendekeza pia utafiti wa kina ufanywe ili kutathmini ufaafu wa mhimili wa maana tambuzi katika kutathmini waandishi mbalimbali wa riwaya, hadithi fupi au tamthilia ili

kubainisha jinsi maana iliyokusudiwa na mwandishi inavyoweza kufasiriwa kwa kutumia mhimili huu. Kwa kufanya hivi, utafiti huu utabainisha kama waandishi mbalimbali hutumia mhimili huu katika matini zao kujenga matini na kufanikisha mawasiliano.

## MAREJELEO


Aduda, K. (2011). A Relevance Theoritic Analysis of Dholuo Neologisms. M.A. Thesis. University of Nairobi: Unpublished.

Atieno, B.O. (2018). Pragmatics of Dholuo Panegyrics. M.A. Thesis. Maseno University: Unpublished.

Afzaal, M. Hu, K. Chishti, I.M & Imran, M. (2019). A Study of Pakistan English Newspaper Texts: An Application of Halliday and Hasan's Model of Cohesion: A Discourse Analysis. *International Journal of English Linguistics*; *Vol.9*, No.5.doi:10.5539/ijel. v9n5p78

Alba-Juez, L. (2009). *Perspectives on Discourse Analysis: Theory and Practice*. Cambridge Scholars Publishing.

Bahaziq, A. (2016). Cohesive Devices in Written Discourse: A Discourse Analysis of a Student's Essay Writing'. *English Language Teaching*; *Vol.9*, No.7; 2016. doi: 10.5539/elt. V9n7p112.

Banks, D. (2002). 'Systemic Functional Analysis as a Model for Text analysis.' ASP [online], 35- 36. URL: http://asp. revues. org/ 1584; DOI:10.4000/asp.1584

Beaugrande, R., Dressler, W.U. (1981). *Introduction to Text Linguistics*. London; New York; Longman.

Blutner, R. (1998). *Lexical Pragmatics in Journals of Semantics*. Volume15(2), pp 115-162.

Butt, D., Fahey, R., Feez, S., Spinks, S.&Yallop, C. (1995). *Using Functional Grammar.An Explorer's Guide*. Sydney: National Centre for English Language Teaching Research.Macquire University.

Brown, G., &Yule, G. (1983). *Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.

Carson, R. (2002). *Thoughts and Utterances. Pragmatics by Explicit Communication*. Blackwell Publishers Ltd, Blackwall Publishing Company.

Dik, S. (1978). *Functional Grammar.* North-Holland Linguistic Series, 37. Amsterdam: North Holland.

Eggins, S. (1997). *An International to Systematic Function.* London: Printer Publisher.

__________ (2004). *An Introduction to Systemic Functional Linguistics. 2nd ed.* London.Continuum International Publishing Group.

Fowler, R. (1991). *Language in the New: Discourse and Ideology in the Press*. London and New York: Routledge.

Gaichu, M.N. (2016). Uchanganuzi wa Sitiari Dhanifu Katika Methali za Kiswahili-Mtazamo wa Nadharia ya Uhusiano. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Gerot, L. & Wignell, P. (1995). *Making Sense of Functional Grammar*. New South Wales: Gerd Stabler.

Grice, H.P. (1975). Logic and Conversation. In Peter Cole & Jerry L. Morgan (eds.), *Syntax and Semantics 3: Speech Acts*,41-58. New York: Academic Press.

Habarkah, S. (2019). An Analysis of Textual Personal Reference in English Version of 'Open Letter to Baghdadi'. Strata One Thesis. State Islamic University: Jakarta.

Habwe, J.H. (1999). A Discourse Analysis of Swahili Political Speeches. Unpublished PhD Thesis, University of Nairobi.

____________ (2012).'Reference Cohesion Within the Complex Sentence in Kiswahili of Nairobi.' *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics, Vol.2* (2012), 79-88.

Habwe, J. & P. Karanja (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M.A.K., &Hasan, R. (1976). *Cohesion in English*. London: Longman.

___________________ (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.

_____________________ (1994). *An Introduction to Functional Grammar*. 3rd Ed. London: Edward Arnold

_______________________ (1997). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Arnold.

Halliday, M. &Mathiessen, C. (1999). *Construing Experience Through Meaning.* London: Edward Arnold.

________________________ (2004). *An Introduction to Functional Grammar (3rd. Ed.)*. London: Arnold.

Hameed, H.T. (2008)' Cohesion in Texts: A Discourse Analysis of News Article in a Magazine.' *AL- Faith Journal. No.37.*

Hasan, R. (1984). 'Coherence and Cohesive Harmony. Understanding Reading Comprehension: Cognition, Language and Structure of Prose, 181-219. Delaware: International Reading Association.'

Karanja, (1993). A Discourse Analysis of KBC TV Broadcast Discussion Programmes. M. A. Thesis. University of Nairobi: Unpublished.

Khofidoh, N. (2017). Anaphoric and Cataphoric Function on Personal References used in English Political News Articles. State Institute for Islamic Studies (IAIN) Salatiga.

Klimova, B. & Hubackova, S. (2014).' Grammatical Cohesion in Abstracts'. University of Kralove, Faculty of Infomatics and Management. *Procedia-Social and Behavioural Sciences* 116, 664-668.www.sciencedirect.com

Koech, S.K. (2013). A Study on Figurative Language Used in Selected Kipsigis Songs. A Lexical Pragmatic Analysis. M.A. Thesis. University of Nairobi: Unpublished.

Lyons, J. (1995). *Linguistic Semantic. An Introduction*. Cambridge University Press.

Malah, Z., Tan, H., Rashid, S.M. (2017).'Evaluating Lexical Cohesion in Nigerian Newspaper Genres: Focus on Editorials.' *International Journal of Applied Linguistics and English Literature*. Vol.6. No.1. URL:http//dx.doi.org/10.7575/aiac.ijalel. v.6n.1p.240.

Matei, A. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matifari, C.J. (2016). A Descriptive Study of Idiom in Lubukusu: A Relevance Theoretical Approach. M.A Thesis. University of Nairobi: Unpublished.

Mathews, P.H. (1997). *The Concise Oxford Dictionary of Linguistics*. Oxford University Press.

Mathiessen, C. (2013). *Introduction to Functional Grammar*. New York.Routledge.

Mulila, A.M. (2005). Muala na Mshikamano Katika Vipuli vya Figo. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi: Haijachapishwa.

Njue, J.G. (1989). Muala Katika Kiswahili: Umuhimu Wake Katika Uchanganuzi wa Ngano za Kiswahili. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Nthenya, M.S. (2009). Uamilifu wa Tonisho Katika Sentensi za Kikamba. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.

Nyarige, P. K. (2002). Thematic Organization and The Use of Reference Cohesion in Written Compositions of Secondary School Students. M.A. Thesis. Kenyatta University: Unpublished.

Ogato, M. M. (2018). Nafasi ya Mshikamano Katika Maudhui Katika Insha za Wanafunzi wa Kidato cha nne Katika Kaunti ya Murang'a. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.

Ojode, J.O. (2014). Uchanganuzi wa Sitiari Katika Nyimbo za Taarab: Mfano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally, Unguja.Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kisii: Haijachapishwa.

Okeyo, J.S. (2011). Matumizi ya Usonde Nafsi na Usonde Jamii: Mtazamo wa Uhusiano. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Okoth, B.Q. (2015). A Cognitive Approach to Cohesion in Dholuo Narratives. M.A. Thesis. University of Nairobi: Unpublished.

Saddimbah, C.R. (2011). Cohesive Devices in Dholuo Sermons: A Textual Analysis. M. A. Thesis. Kenyatta University: Unpublished.

Schiffrin, D., Tannen, D., & Hamilton, H.E. (Eds). (2008). *The Handbook of Discourse Analysis*. John Wiley & Sons.

Schubert, C. (2008). *Englische Textlinguistik*. Eine Einfuhrug. Berlin: Schmidt.

Shroeder, H. (2005). "Do we speak the same Language?" A Cognitive Pragmatic Explanation of Cultural Misunderstandings.In Across Borders: Benefiting from Cultural Differences. Paper Originally Presented at International Conferences on Africa, Globolization and Justice, at the Catholic

University of Eastern Africa (CUEA), Centre for Social Justice and Ethics Nairobi: 17th-19th May 2006.

Sperber, D.& Wilson, D. (1995). *Relevance: Communication and Cognition*. Oxford: Blackwell.

______________________ (2004). *"Relevance Theory in Horn and Wards (eds). The Book of Pragmatics"*. United Kingdom Blackwell Publishers.

Sugiharto, S., (2004). 'Reference, Anaphora, and Deixis: An Overview. '*Journal Bahasa &Sastra*, *Vol.4* No.2, 134-145.

Sukthanker na wengine. (2020).'Anaphora and Coreference Resolution. A review. '*Information Fusion*; *59, 139*-162.

Thiga, C.N. (1997). Cohesion and Compactness in Compositions Written by Kenyan Urban Primary School Children. M.A Thesis. Kenyatta University: Unpublished.

Thompson, G. (1996). *Introduction to Functional Grammar*. 2nd ed. New York: Oxford University Press.

Toews, N. (2016). Relevance Theory and Proverbs: Exploring Context Through Explicatures and Implicatures. M.A. Thesis. Trinity Western University: Unpublished.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wakirindi, P.M. (2010). A Functional Grammar to the Analysis of Gikuyu Emphatic Clauses. M.A. Thesis. Kenyatta University: Unpublished.

Wilson, D. (2003). *Relevance Theory and Lexical Pragmatics*.Italian Journal of Linguistics/Rivista Di Linguistica 15:273-291.

Wilson, D. & Spencer, D. (2002). *Truthfulness and Relevance*. Mind III: 583-632.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*.Oxford: Oxford University Press.

**VIAMBATISHO**

**KIAMBATISHO 1**

4 **HABARI ZA KAUNTI**

Jumatano, Juni 3, 2020 | TAIFA LEO

Matini 1

# Katiba haihitaji mageuzi, Karua akosoa Uhuru

NA WANDERI KAMAU

**NAIROBI**

KIONGOZI wa Narc-Kenya, Bi Martha Karua(*pichani*), amekosoa vikali pendekezo la Rais Uhuru Kenyatta, kwamba Kenya inahitaji mabadiliko ya kikatiba ili kukabili ghasia za kikabila ambazo hutokea kila baada ya uchaguzi mkuu nchini.

Kwenye hotuba yake mnamo Jumatatu, wakati wa sherehe za Sikukuu ya Madaraka, Rais Kenyatta alisema kuwa mabadiliko ya kikatiba ndio njia pekee ya kuondoa taharuki za kisiasa ambazo hukumba chaguzi hizo.

Hata hivyo, Bi Karua amekosoa pendekezo hilo, akishikilia kuwa ingawa hapingi marekebisho hayo, kile Wakenya wengi wanataka kuona ni utekelezaji ufaao wa katiba ya sasa.

Kwenye mahojiano mnamo Jumatatu, Bi Karua alisema kuwa ni kinaya kwamba wanasiasa wanakimbilia kushinikiza marekebisho hayo, wakati katiba ya sasa imekuwa ikikiukwa kila mara.



"Hisia zetu ni kwamba Katiba ya sasa haijatekelezwa kikamilifu, kwani kumekuwa na ulegevu mkubwa katika utekelezaji wake. Kwa hilo, sioni haja yoyote ya kushinikiza mageuzi hayo, wakati Katiba iliyopo haijakuwa ikizingatiwa," akasema.

Baadhi ya ripoti zimekuwa zikidai kwamba Rais Kenyatta analenga kuendelea kuhudumu serikalini baada ya uchaguzi mkuu mnamo 2022, kwa kuongeza nyadhifa za kisiasa.

Miongoni mwa nyadhifa zinazotajwa ni nafasi ya Waziri Mkuu na manaibu wake wawili.

Na ingawa amejitokeza wazi kukanusha kauli hiyo, Rais Kenyatta alinukuliwa mwaka uliopita akisema kuwa hangejali kuhudumu kwenye wadhifa wowote ikiwa Wakenya wataamua.

Hata hivyo, Bi Karua alipinga vikali kauli ya Rais Kenyatta, akishikilia kuwa tatizo kuu linalokumba Kenya si mfumo wa utawala, bali utaratibu wa usimamizi na uendeshaji wa chaguzi kuu na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

"Tatizo tulilo nalo kama Wakenya ni ukosefu wa imani kwenye chaguzi kuu na taasisi zinazoziendesha. Tunahitaji mdahalo wa kitaifa kuhusu hilo, kwani IEBC haijaimarisha uaminifu wake kwa Wakenya kwa muda mrefu," akasema.

Alieleza kuwa katika mfumo wowote wa kidemokrasia, lazima kuwe na mshindi na anayeshindwa, ambapo wanaokosa kuridhika na matokeo wanapaswa kwenda mahakamani kuwasilisha malalamishi yao.

Bi Karua amekuwa akikosoa juhudi zozote za mageuzi ya kikatiba, akishikilia kuwa badala yake, serikali inapaswa kuimarisha taasisi zilizopo chini ya Katiba ya sasa.

**UBOMOAJI:** Wafanyabiashara walia kudhulumiwa



**WAFANYABIASHARA** watwaa bidhaa zao baada ya vibanda vyao sokoni Kongowea, Mombasa kubomolewa jana asubuhi na serikali ya Kaunti ya Mombasa. Wanabiashara hao wanashutumu serikali hiyo kwa kupuuza agizo la mahakama.
*Picha/Wachira Mwangi*

**KIAMBATISHO 2**

4 HABARI ZA KA

Matini 2

MOMBASA 04/06/2020

# Shirika lasaidia watu wenye akili taahira

**WATU** wawili wenye akili taahira wanashughulikiwa na shirika moja la kutoa msaada baada ya kubainika kuambukizwa maradhi ya virusi vya corona katika mtaa wa Majengo, Mombasa.

Wawili hao ni miongoni mwa wagonjwa wengine 15 wenye akili punguani waliochukuliwa kutoka maeneo mbalimbali katika kaunti hiyo mwezi uliopita.

Akizungumza na *Taifa Leo*, Mwenyekiti wa shirika la *Women Empowerment Network* ambaye amekuwa akishughulikia na kupigania haki za wagonjwa wa akili katika kaunti hiyo, alisema walipokea matokeo hayo baada ya kaunti kuwapima watu hao 15.

"Maafisa wa afya katika kaunti walituelekeza tuwatenge wagonjwa hao wawili. Kwa bahati nzuri, tangu tuwachukue wagonjwa hao 15, wamekuwa wakikaa katika vyumba tofauti katika chuo cha ufundi cha Kenya Coast National Polytechnic," akasema Bi Abdalla.

*Na Diana Mutheu*

## KIAMBATISHO 3



4 HABARI ZA KAU

Matini 3
05/06/2020

THIKA

# Landilodi atimua wapangaji kwa kutolipa kodi

**FAMILIA** saba katika kijiji cha Kisii mjini Thika, kaunti ya Kiambu, wamefungiwa nyumba zao baada ya landilodi kudai hawajalipa kwa miezi miwili.

Kulingana na wapangaji hao mwenye nyumba alifika hapo Jumanne asubuhi kwa fujo na kulazimisha kila mpangaji kuondoka ili afunge nyumba yake.

Licha ya wapangaji hao kumsihi awahurumie, hawakuwa na budi kwani alikuwa ameandamana na watu waliolazimisha wapangaji kuondoka au mali zao zitupwe nje.

Diwani wa wadi hiyo, Bw Raphael Chege alisema mmiliki wa nyumba hiyo ameagizwa kufika katika makao makuu ya kaunti ya Kiambu kuelezea sababu zilizomfanya kuchukua hatua hiyo.

"Hatua iliyochukuliwa na landilodi huyo ni mbaya na atalazimika kueleza ni kwa nini alifanya hivyo," alisema Bw Chege.

*Na Lawrence Ongaro*

## KIAMBATISHO 4

4 **HABARI ZA K**

08/06/2020
Matini 4

LAMU

# Gavana aonya maafisa wake kuhusu ufisadi

Na KALUME KAZUNGU

GAVANA wa Kaunti ya Lamu, Bw Fahim Twaha, ameonya kuwa afisa yeyote wa umma atakayehusishwa na ufisadi atasimamishwa kazi.

Akizungumza wakati wa kuapisha maafisa sita wapya wa Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu (PSB), Bw Twaha aliwasisitizia haja ya kuzingatia maadili, uwazi na uwajibikaji wakati watakapokuwa wakitekeleza majukumu yao.

Alionya kwamba serikali yake haitamruhusu yeyote atakayejihusisha au kupatikana na kesi za ufisadi kuendelea kuhudumu katika bodi hiyo.

Gavana huyo pia aliwataka maafisa hao kutekeleza majukumu yao kulingana na katiba inavyosema hasa kuhusiana na mamlaka na sheria zinazoongoza utendakazi wa serikali za kaunti.

"Ninawapongeza nyote kwa kufaulu kuchaguliwa. Langu tu ni kuwaomba kuzingatia maadili na kutekeleza majukumu yenu kwa uwazi na uwajibikaji. Ukijihusisha na ufisadi wa aina yoyote hutakuwa na budi ila kutemwa nje. Wakazi wa Lamu wanawategemea nyinyi ili kuleta sura mpya katika utekelezaji wa majukumu yenu," akasema Bw Twaha.

Sita hao ni Mawiya Farid, Mwenye Ali, Sairus Mburu, Naima Ahmed, Rehana Gubo na Fadhil Mohamed.

Waliapishwa katika hafla maalum iliyoandaliwa kwenye makao makuu ya Kaunti ya Lamu mjini Mokowe iliyohudhuriwa pia na Naibu Gavana Abdulhakim Aboud.

Bw Aboud aliwasisitizia maafisa hao kutekeleza majukumu yao kwa kufuata matamanio ya wananchi wa Lamu.

"Hatutaki nyinyi mfuate matamanio yenu au ubinafsi katika kutekeleza majukumu yenu. Mtafaulu zaidi iwapo mtatekeleza wajibu wenu kwa kufuata matamanio ya wananchi wa Lamu," akasema Bw Aboud.

Wengine waliokuwepo wakati wa hafla ya kuwalisha kiapo sita hao ni Katibu wa Kaunti ya Lamu, John Mburu na mawaziri wa idara mbalimbvali za kaunti ya Lamu, wakiongozwa na Waziri wa Fedha wa eneo hilo, Ahmed Hemed na mwenzake wa Ardhi na Mipangilio ya Kaunti, Bi Fahima Araphat.

**KIAMBATISHO 5**

Matini 5 09/06/2020

Afisa wa makavazi asema wanataka kuupa ufuo huo sura mpya

# Serikali yatetea ubomoaji Pirates

**MOMBASA**

**NA DIANA MUTHEU**

SERIKALI imejitetea kuhusu ubomoaji vibanda katika ufuo wa Jomo Kenyatta almaarufu kama Pirates, Kaunti ya Mombasa.

Kwenye mahojiano na *Taifa Leo*, Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Makavazi ya Kenya (NMK) eneo la Pwani, Bw Athman Hussein alisema wanashirikiana na serikali ya kaunti pamoja na Wizara ya Utalii ili kuupa ufuo huo sura mpya, ifike hadhi ya kimataifa.

Wafanyabiashara wanaotegemea ufuo huo kiriziki walishtuka Jumamosi walipokuta vibanda vyao vimebomolewa Ijumaa usiku.

"Tumekuwa na mipango hii tangu tupewe mamlaka ya kusimamia ufuo huo. Eneo lenyewe limekuweko na vibanda vingi vibovu na hata hali ya usalama haijakuwa ya kuridhisha na tunataka kubadilisha hayo yote," akasema Bw Hussein.

Ufuo wa Jomo Kenyatta ni moja kati ya sehemu za umma zenye umaarufu sana katika kunti ya Mombasa.

Kabla ya nchi kukumbwa na janga la corona, watu wengi, ikiwemo wenyeji na watalii walipenda kuzuru eneo hili kujivinjari wakati wa sikukuu za Pasaka na Krismasi.

Bw Hussein alisema kuwa mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya kaunti ya Mombasa na Wizara ya Utalii.

Hata hivyo, hakutaja ni kiwango kipi cha fedha kitatumika wala marekebisho hayo yatachukua muda kiasi gani.

Inaaminika mpango ni kuuboresha ili ufikie hadhi ya bustani ya Mama Ngina ambayo pia ilifanyiwa ukarabati mwaka uliopita.

"Wakati huu ambapo hakuna biashara nyingi zinaendelea pale na hata watu hawaruhusiwi kwenda baharini, inatupa fursa nzuri kuanza marekebisho hayo. Tunasubiri serikali itoe fedha hizo ili kazi ianze," akasema.

Afisa huyo wa NMK alisema kuwa wanabiashara katika eneo hilo walipewa ilani kitambo, kabla ya ubomoaji kuanza.

"Wafanyabiashara walipewa ilani zaidi ya miaka mitatu iliyopita na majina yao yakaorodheshwa ili marekebisho yakikamilika, watarudi katika sehemu zao za kazi ambapo yatakuwa ni majengo mapya," akasema.

Wafanyabiashara wengi walilaumu serikali ya kaunti kwa kutumia fursa hiyo wakati watu wako nyumbani kwa sababu ya janga la corona, kuharibu majengo yao bila kuwajulisha.

"Imekuwa siku ndefu na ya kusikitisha kwetu sisi, kuona uharibifu unaofanywa na watu ambao wanafaa kulinda mali yetu," alisema Hamis Abdallah, mwogeleaji katika ufuo huo.

Kwa upande wake, Benard Kioko ambaye pia alikuwa na duka katika eneo hilo anataka serikali iwape sehemu ya kufanyia biashara zao.

"Uharibifu huo ulifanywa usiku wakati wa marufuku ya kutoka nje, ambapo Mkenya wa kawaida haruhusiwi nje, na hii inadhihirisha mengi kuhusu viongozi wetu," Bw Kioko alisema.

## KIAMBATISHO 6

10/06/2020 Matini 6

# Wazee waunga mkono azma ya Kalonzo kumrithi Uhuru

**MACHAKOS**

**NA STEPHEN MUTHINI**

WAZEE kutoka jamii ya Wakamba wamezidisha juhudi za kutaka Kiongozi wa Chama cha Wiper, Bw Kalonzo Musyoka amrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022.

Wazee hao walisema uamuzi wa Bw Musyoka kufanya kazi na Rais ulikuwa wa busara kwa sababu ulimweka katika nafasi nzuri ya kujitayarisha kuongoza nchi.

Akiongea na wanahabari wakiwa Mwala, mwenyekiti wa baraza la wazee wa koo za jamii ya Wakamba Boniface Kilonzo alihimiza jamii hiyo kuendelea kuunga mkono azma ya Bw Musyoka akisema nafasi yake ya kuongoza nchi imekaribia.

"Kama viongozi, tuna furaha kwamba mwana wetu Kalonzo Musyoka alifanya uamuzi wa busara kwa kuchagua kushirikiana na chama tawala cha Jubilee na Kanu. Hii ni ishara ya nia njema ya jamii yetu," wazee hao walisema kwenye taarifa wakimshukuru Bw Musyoka kwa hatua hiyo.

Wazee hao walisema kama baraza, wako na jukumu la kuelekeza watu katika masuala ya umoia huku wakilenga umoja wa kitaifa.

"Tunatambua kwamba Kenya inakabiliwa na changamoto ambayo haijawahi kutokea tunapopigana na virusi vya corona huku mageuzi ya kikatiba, umoja na ushirikishi kupitia BBI zikihitaji kuendelea.

"Inatuhitaji sisi sote kukomesha siasa zisizokuwa na maana na kuelekeza nguvu zetu kumuunga Rais," alisema Bw Kilonzo aliyesoma taarifa ya wazee hao.

Walisema wanasikitishwa na matamshi ya baadhi ya watu kutoka jamii hiyo na wakawashauri wakomeshe tabia hiyo mara moja.

Bw Kilonzo alisema maslahi ya kibinafsi na ya kisiasa hayawezi kufanya jamii nzima ikose kuwa serikalini.



**KINARA wa Wiper Kalonzo Musyoka (kulia) akiwa na Isaac Ruto wa CCM majuzi.** *Picha/Maktaba*

## KIAMBATISHO 7

KAUNTI

Matini 7

Ijumaa, Juni 12, 2020 | TAIFA LEO

12/06/2020

# Magereza yashona barakoa 500,000 kukinga wafungwa

NA OSCAR KAKAI

**KAPENGURIA**

IDARA ya magereza imeanza kushona barakoa 500,000 zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja na wafungwa kama njia ya kukabiliana na virusi vya corona.

Kamishna wa magereza nchini, Bw Wycliffe Ogallo akizuru gereza la Kapenguria jana alisema kuwa magereza mengi nchini yamejiandaa vyema kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.Bw Ogallo alisema kuwa ziara yake ililenga kuangalia jinsi magereza yamejitayarisha kupigana na janga hilo. Pia alisema kuwa iwapo kutakuwa na msongamano wowote, wafungwa wenye makosa madogo wataachiliwa.

"Utaratibu ambao umewekwa na wizara ya afya unafaa kufuatwa. Magereza yetu kwa sasa yana wafungwa 47,000 kote nchini," alisema.

Alisema kuwa serikali imepeana msaada kwa idara ya magereza kwa kukabiliana na virusi na kuipongeza wizara ya afya kwa kazi nzuri inayofanya. Aliongeza kusema kuwa wamewekwa mahali pa kuosha mikono na sabuni katika magereza yote na wafungwa wamehamasishwa kuhusu virusi vya corona.

Gereza la Kapenguria lina wafungwa 274 na kufikia sasa hakuna kisa chochote cha corona kimeripotiwa.



**POLISI wa Magereza abeba maboksi yaliyo na bidhaa mbalimbali za kujikinga na virusi vya corona, kupeleka kwenye Makao Makuu ya Magereza, Nairobi, Aprili.** *Picha/Evans Habil*

**KIAMBATISHO 8**

Matini 8

16/06/2020

## Msongamano na vurugu katika kivuko hicho ndicho kiini cha uhalifu

# Kanuni kali kudumishwa ferini hata baada ya virusi

Na MISHI GONGO

**MOMBASA**

SERIKALI inapanga kudumisha kanuni kali zinazotekelezwa katika kivukio cha feri Likoni, Kaunti ya Mombasa, zitadumishwa hata baada ya janga la corona kudhibitiwa kikamilifu.

Kulingana na mratibu wa usalama katika eneo la Pwani Bw John Elungata, msongamano na vurugu katika kivuko hicho vimekuwa vikisababisha uhalifu ikiwemo wanawake kunajisiwa, na abiria kuporwa.

Akizungumza na Taifa afisini mwake, Bw Elungata alisema hatua ya kuwaagiza abiria kuwekeana umbali wa mita moja imesaidia kupunguza uhalifu.

"Tutahakikisha kuwa maafisa wa usalama watasalia katika kivuko hicho kuhakikisha kuwa abiria wanatekeleza masharti yaliyopo," akasema.

Kila siku kivuko cha feri hutumiwa na takriban watu 300,000 na magari 6,000.

Bi Rehema Mzee, mkazi wa Likoni anayetumia kivuko hicho kila siku, alisema kwa sasa anafurahia huduma za shirika hilo kufuatia utulivu unaoshuhudiwa.

"Tulikuwa tunashuhudia wazee kwa watoto wakikanyagwa katika vurumai ambazo huzuka saa za jioni na alfajiri watu wanapokimbilia vibaruani lakini kwa sasa hali ni shwari," akasema.

Mkazi mwengine Bi Irene Mwangi ambaye ni muuzaji bidhaa katika eneo la Shonda, Likoni, alisema awali walipoteza mizigo yao kwa wabebaji ambao walitoweka nayo katikati ya halaiki kubwa ya watu.

"Wahudumu wengi wa vibanda hutoa bidhaa zao soko la Kongowea, tukifika katika kivuko hichi huwapa wabebaji ili kutusaidia. Baadhi yao hujiingiza katika makundi ya watu na kutoweka, lakini tangu kuwekwa sheria mpya hilo haliwezekani," akasema.

Manufaa mengine ambayo yanashuhudiwa Pwani kwa kanuni za kudhibiti corona ni uhifadhi wa fuo na bahari.

Katika mahojiano ya awali, wataalamu wa mazingira walisema tangu kuwekwa kwa kafyu mazingira yamekuwa safi.

Kabla kufungwa kwa fuo za bahari, maelfu ya wakazi walikongamana katika fuo za bahari katika eneo la Pwani kujivinjari. Hali hiyo ilisababisha uchafuzi kwa utupaji taka kiholela.

Aidha marufuku ya kukongamana yamesitisha disko matanga na disko vumbi katika Kaunti ya Kilifi ambaya yalikuwa yanasababisha mimba za mapema miongoni mwa vijana.

Kulingana na Kamishna wa polisi katika eneo hilo Magu Mutindika, jam visa vya mimba za mapema bado vinashuhudiwa japo vimepunguwa pakubwa.

Katika sekta ya hoteli na utalii, Bw AbdulAziz Ali alisema maduka ya jumla pia yanapaswa kuendeleza kanuni za usafi baada ya janga la corona.

**KIAMBATISHO 9**

4 **HABARI ZA KAUN**

Matini 9 18/06/2020

**KILIFI**

# Wazee wateta msitu wa Kaya kuharibiwa

**WAZEE** wa Kaya katika Kaunti Ndogo ya Rabai, Kaunti ya Kilifi, wamelalamikia uharibifu wa msitu wa Kaya Bomu unaotekelezwa na watu wanaochoma makaa.

Wakizungumza na wanahabari katika eneo la Rabai wakiongozwa na Bw Kwasho Koba, walisema tangu serikali ilipopiga marufuku wazee kuingia katika misitu kufutia mulipuko wa virusi vya corona, baadhi ya wakazi wa sehemu hiyo wameanza kuharibu msitu huo.

Wazee hao wanaitaka idara ya misitu nchini kuingilia kati na kusaidia kuuhifadhi msitu huo kwani wanahofia iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa dhidi ya kuulinda huenda ukamalizwa kabisa.

Kwa upande wake, Bw Said Shitanda ameitaka idara ya polisi katika kaunti hiyo kuimarisha usalama hadi katika maeneo ya mashinani ili kuzima wahalifu watekeleza mauaji ya wazee eneo hilo.

"Tunawasihi maafisa wetu wa polisi waimarishe ziara za mara kwa mara ili kukabiliana na mauaji ya wazee." alisema Bw Shitanda.

*Na Alex Amani*

**KIAMBATISHO 10**

KAUNTI

Matini 10
20/06/2020

### Apuuza dai la kutumia mageuzi ya katiba kuhudumu zaidi ya 2022

# Sina haja ya kubaki mamlakani - Uhuru

**NAIROBI**

**Na CHARLES WASONGA**

RAIS Uhuru Kenyatta amepuuzilia mbali madai kuwa anapania kutumia mabadiliko ya Katiba kuendelea kusalia mamlakani baada ya 2022.

Aidha, alikanusha uvumi unaosambazwa na mahasidi wake wa kisiasa kwamba anakimezea mate kiti cha Waziri Mkuu mwenye mamlaka, kinatakachobuniwa baada ya mageuzi hayo ya katiba kupitia kura ya maamuzi.

"Inasikitisha kuwa kuna watu wanaofasiri mageuzi ya Katiba kupitia kura ya maamuzi kuashiria kuwa ni njama ya kuongeza muhula wangu uongozini kama rais. Na wengine pia wamedai eti ninataka kuwa Waziri Mkuu. Madai haya hayana ukweli wowote," Rais Kenyatta akasema Alhamisi jioni.

Alikuwa akijibu maswali, kwa njia ya video, wakati wa mkutano na shirika la Atlantic Council lenye makao yake nchini Amerika.

Rais akaongeza: "Nawaambia, ikiwa kuna suala ambalo Wakenya wanafahamu fika ni mihula miwili ya urais. Wakenya wamefahamu kuwa marais wamekuwa wakihudumu kwa mihula miwili tangu 1992 utawala wa vyama vingi uliporejelewa nchini Kenya. Hakuna Rais ambaye amewahi kuvunja sheria hiyo na sina nia ya kuwa wa kwanza kufanya hivyo."



**RAIS Uhuru Kenyatta akiwa kwenye mkutano na viongozi wa Umoja wa Afrika kwa njia ya video katika Ikulu ya Nairobi juzi. Rais amepuuza wanaodai kuwa ana nia ya kusalia madarakani baada ya 2022 kupitia mageuzi ya katiba.** *Picha/PSCU*

Kiongozi wa taifa alisema lengo la Mpango wa Maridhiano (BBI), na mageuzi yanayopendekezwa kwayo, ni kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo havikabiliwa na baadhi ya changamoto zinazokumba kizazi cha sasa.

"Chini ya utawala wa vyama vingi, taifa hili limekuwa likishuhudia machafuko kila baada ya chaguzi. Kwa hivyo, ushirikiano wangu na Raila (Odinga) unalenga kujaribu kuona kama tutapata suluhu la matatizo kama hayo kupitia mpango wa BBI," Rais Kenyatta akaeleza.

Kuhusu iwapo maguezi ya Katiba yanalenga kubuni cheo cha Waziri Mkuu alisema: "Sina habari kama kama kutabuniwa wadhifa wa waziri mkuu katika katiba. Haya ni maoni ya baadhi ya watu. Kile ambacho raia wana haja nayo ni kupata thamani ya kura yao, ugavi sawa wa rasilimali na uwepo wa serikali inayowashirisha watu wote."

Naibu Rais William Ruto, na wanasiasa wandani wake, wamepinga pendekezo la mageuzi ya katiba kupitia kura ya maamuzi ili kubuniwe wadhifa wa Waziri Mkuu na manaibu wake wawili, wakisema zitawaongezea raia gharama zaidi.

Baadhi yao wamekuwa kuwa aidha, Rais Kenyatta anapania kusalia mamlakani baada ya muhula wake wa pili na wa mwisho kukamilika au anataka ateuliwa Waziri Mkuu baada ya 2022.

Lakini kwenye mahojiano hayo, yaliyoendeshwa na Katrina Manson, Rais Kenyata alisema hangezungumzia suala hilo la Waziri Mkuu "kwa sababu sio suala kuu katika mpango mzima wa BBI".

"Kile ninaweza kusema ni kuwa Afisi iliyoko sasa ni ile ya Rais. Rais wa Jamhuri ya Kenya. Na Katiba yetu imebainisha wazi kuwa Rais huhudumu kwa mihula miwili. Mihula miwili pekee. Na sasa niko katika muhula wangu wa pili," akasisitiza.

## KIAMBATISHO 11

22/06/2020 Mtaifa 11

NAKURU

# Wadau wataka kuelekezwa kuhusu Sh3b za utalii

NA SAMUEL BAYA

WAWEKEZAJI katika sekta ya utalii kaunti ya Nakuru sasa wanataka kujua jinsi watakavyonufaika na Sh3 billioni zilizotengwa na serikali kuifufua sekta hiyo.

Mwenyekiti wa muungano wa watalii katika kaunti hiyo, Bw David Mwangi na mwenyekiti wa muungano wa waelekezaji watalii David Mwangi walisema sekta hiyo ni miongoni mwa sekta zilizoathiriwa vibaya na ugonjwa wa corona.

"Ni vyema tukijua kama serikali itatusaidia vipi kupata fedha za kufufua mpango huu wa utalii. Tunafahamu kwamba serikali ilitenga kiasi cha Sh3billioni kwa ajili ya mpango huo," akasema Bw Mwangi.

Aidha alisema kwamba kuna haja ya serikali kupitia kwa wizara ya utalii kuwafahamisha wao kama washikadau ni kwa njia gani ambayo watatumia kufidia biashara zao ambazo ziliathiriwa vibaya na virusi vya corona.

"Kufikia sasa hatujafahamu kama fedha hizi zitatufikia kama mikopo aina ya grants au tutapatiwa kama mikopo ya biashara na mabenki. Hapo ndipo ambapo bado tuko gizani. Vile vile hatujafahamishwa ni shirika gani la serikali ambalo litakuwa likihusika na utoaji wa pesa hizo," akasema Bw Mwangi.

Akiongea kwa niaba ya waelekezi wa watalii, Bw John Mwangi naye alisisitiza kwamba kuna haja ya serikali kuwaeleza jinsi ambavyo wataweza kupata fedha zilizotengwa na serikali kwa ajili ya sekta hiyo.

"Tunachofahamu ni kuwa zipo fedha ambazo zilitengwa na serikali kufufua tena sekta hii baada ya corona kuisha. Tungeomba serikali itueleze ni vipi tutakavyoweza kuzipata kwa sababu bado tuko katika giza la haya yote," akasema.

## KIAMBATISHO 12



ISIOLO

Matini 12
25/06/2020

# Familia nzima karantini kwa kukiuka kanuni za afya

Na WAWERU WAIRIMU

WATU wanane kutoka familia moja wanaodaiwa kusafiri mjini Isiolo kutoka mtaa wa Eastleigh, jijini Nairobi, wamesukumwa karantini kwa lazima.

Wanane hao ambao walikuwa wakisafiria gari aina la Land Cruiser walilokuwa wamekodisha, walinaswa na polisi wanaosimamia kuzuizi cha barabara katika Uwanja wa Ndege wa Isiolo.

Vile vile, walikuwa wamebeba mizigo.

Polisi waliwaweka kwenye karantini mara moja kwa kukosa stakabadhi zifaazo za usafiri.

Dereva wa gari hilo alijitetea akisema, hawakutumia njia za mkato, kwani walipeana maelezo yao katika kizuizi cha polisi kilicho katika eneo la Blue Post, Kaunti ya Kiambu.

Waziri wa Afya katika kaunti hiyo, Bw Wario Galma, alisema wanane hao wanajumuisha mwanamke, wanawe wawili wa kiume na wasichana watano.

Alisema watakaa kwenye karantini kwa siku 14 ndipo waruhusiwe kuondoka.

"Familia hiyo ilikuwa ikielekea mjini Isiolo na tumeiweka kwenye karantini katika Kituo cha Matibabu cha Isiolo," akasema Bw Gama, kwenye mahojiano na 'Taifa Leo.'

Aliwaomba wakazi kutoa habari kwa idara husika wanapowaona wageni wanaofika katika maeneo yao bila kupimwa ikiwa wameambukizwa virusi hivyo. Kamishna wa Kaunti hiyo, Bw Herman Shambi, alionya kuwa watu wanaoingia humo kutoka maeneo yaliyoorodheshwa kuwa na maambukizi makubwa ya virusi watawekwa kwenye karantini kabla ya kuruhusiwa kutangamana na wananchi.

Alisema kinyume na awali, sasa watakuwa wakiwekwa kwenye karantini kwa lazima ili kudhibiti maambukizi ya virusi.

**KIAMBATISHO 13**

Nyataya

Matini 13 26/06/2020

# Wakulima wa chai waomba mbolea

GITONGA MARETE Na DERICK LUVEGA

MERU

WAKULIMA wa majani chai, sasa wanataka serikali iwape mbolea ya bei nafuu baada ya Mamlaka ya Ustawishaji wa Chai (KTDA) kusimamisha uagizaji kutoka nje wakisema hawawezi kumudu bei ya bidhaa hiyo.

Wakulima hao wanasema kwamba iwapo hawatapata mbolea ya bei nafuu kiwango cha majanichai kitapungua mwaka huu.

"Serikali inafaa kuingilia kati sasa kwa sababu iwapo tutakosa kutumia mbolea, uzalishaji utapungua kwa asilimia 50," alisema Bw Nturibi Gikunda, mkulima kutoka Imenti ya Kati, Kaunti ya Meru.

"Baadhi yetu tulikosa kutumia mbolea miaka iliyopita kwa sababu mbalimbali lakini tukagundua kuwa bila kuitumia, mazao hupungua," alisema.

Kwa miaka mingi, KTDA imekuwa ikiagiza mbolea kutoka nje ya nchi na kuwauzia wakulima kwa bei ya Sh2,000 badala ya bei ya kawaida ya Sh3,000 kwa gunia la kilo 50.

Kwa sababu ya matatizo yaliyosabishwa na janga la corona, KTDA ilisema kwamba haitaweza kununua mbolea kutoka Urusi na kuacha wakulima wapatao 600,000 wa mashamba madogomadogo kwenye shida.

Shirika hilo lilisema kwamba litarejeshea wakulima Sh1.3 bilioni walizokuwa wametoa kununua bidhaa hiyo katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Mwenyekiti wa kitaifa wa chama cha wakulima wa majanichai wa mashamba madogo (Kestega), Bw John Nteere alizitaka serikali za kaunti zitenge pesa kusaidia wakulima wa majanichai.

"Wizara inafanya mabadiliko ambayo yatafanya KTDA kupoteza baadhi ya mapato iliyokuwa ikipata kama wakala ili yafaidi viwanda.

Hatuelewi jinsi uagizaji wa mbolea ulivyoathiriwa ilhali bidhaa nyingine zinanunuliwa kutoka nje ya nchi. Pia hakuna haraka ya kurudisha pesa na wangesubiri," alisema Bw Nteere.

Kwingineko, kundi la madiwani kutoka Magharibi, Nyanza na Rift Valley Kaskazini wanamtaka Rais Uhuru Kenyatta akabiliane na mabwanyenye wanaoingiza sukari nchini kimagendo.

Wakihutubia wanahabari eneo la Kaburengu, Kaunti ya Kakamega, madiwani zaidi ya 15 kutoka kaunti za Nandi, Uasin Gishu, Trans Nzoia, Vihiga, Busia, Bungoma na Kakamega walitishia kuvamia vituo vya forodha vya Busia na Malaba, wanavyodai kuwa vimegeuzwa ngome za ufisadi.

Wakiongozwa na Naibu Spika wa Bunge la Kaunti ya Kakamega, Bw Leonard Kasaya, walidai sukari hiyo inaingizwa katika eneo lao na kuwaathiri wakazi, ambao wengi ni wakulima wa miwa.

"Uingizaji huu wa sukari kimagendo huenda ukashukisha bei ya sukari inayotengezwa humu nchini. Jambo hili litawaathiri wakulima wetu, ambao huingia gharama kubwa kukuza miwa," akasema Bw Kasaya, ambaye pia ni diwani wa Wadi ya Shirugu.

Naibu spika huyo alisema karibu wakulima milioni sita wa miwa wataathiriwa na uingizaji huo haramu wa sukari kutoka nje ya nchi.

## KIAMBATISHO 14



4 HABARI ZA KA

Matini 14

TRANS NZOIA 27/06/2021

# Wakazi waandamana baada ya kukosa umeme kwa mwezi

**WAKAZI** wa eneo la Premium viungani mwa mji wa Kitale waliandamana wakilalamikia tatizo la kukosa umeme kwa muda wa mwezi mmoja na nusu.

Wakiwa na mabango na matawi, walisema wameteseka sana kwa kukosa umeme kwa muda huo wote.

Wakiongozwa na Bw Chirchir Bor, walitaka kampuni ya Kenya Power imhamishe msimamizi wake eneo hilo, wakidai kuwa amekuwa na kiburi wala hasikilizi malalamishi ya wakazi wa Trans-Nzoia.

"Juhudi zetu za kupata usaidizi kwenye afisi kuu mjini kitale zimekuwa zikigonga mwamba huku biashara zikiathirika na usalama kudorora eneo hili. Tunaomba serikali ya kitaifa kupitia waziri wa Kawi kuingilia kati," akasema bw Bor.

Mwenzake Bi Ann Juma alisema hali ya masomo kwa wanafunzi imeathirika mno kwa kuwa wengi hawawezi kusoma nyakati za usiku kutokana na giza.

*Na Osborn Manyengo*

**KIAMBATISHO 15**

KISII 28/06/2020

Matini 15

# Shebesh alaani usiri kuhusu ukeketaji

**WAZIRI** Msaidizi wa Utumishi wa Umma, Vijana na Jinsia, Bi Racheal Shebesh amelaumu jamii Abagusii kwa kukosa kuripoti visa vya ukeketaji.

Kulingana naye, tabia hiyo pamoja na ukosefu wa ushirikiano kati ya wahudumu wa afya na wazazi ndizo sababu kuu zinazochangia ongezeko la desturi hiyo iliyopitwa na wakati.

Waziri huyo aliyekuwa ziarani katika Kaunti za Nyamira na Kisii kwa siku mbili alidokeza kwamba, kaunti hizo mbili zinaongoza katika ukeketaji wa watoto wa kike, kati ya kaunti 22 zinazoendeleza ukatili huo.

Kulingana na Bi Shebesh, wazazi wengi maeneo hayo wamekuwa wakiendesha ukeketaji kisiri wakati shule zimefungwa kwa ushirikiano na madaktari wanaomiliki kliniki za kibinafsi au hata madaktari wanaohudumu katika hospitali za serikali ambao huitwa nyumbani waliko watoto kwa lengo la kujipatia hela.

Bi Shebesh alipuzilia mbali dhana miongoni mwa jamii ya Abagusii kwamba, mtoto wa kike asipokeketwa, atageuka kuwa kiruka njia atakapoolewa eti atakuwa na hamu ya kufanya ngono isiyoweza kudhibitiwa kwa urahisi.

"Hakuna kitu kama hicho. Hamu ya kufanya ngono huletwa na homoni za mwili na tafadhali tukome kuwabandika wasichana wetu majina ya kuwadhihaki wanapoasi mila hii. Ikiwa ilituchukua wiki moja kuzingatia maagizo ya corona kama vile kukoma kupigana busu na kusalimiana kwa mikono, mbona tusiuasi ukeketaji huu jameni ambao hauna umuhimu wowote?" akauliza Shebesh.

Aliwaonya machifu kwamba watafutwa kazi iwapo kisa chochote kitatekelezwa kwenye kata zao na kisiripotiwe.

Pia alisisitiza machifu watakaojaribu kufunika uovu huo kwa kutatua migogoro itakayoibuliwa na ukeketaji kwa njia za kienyeji hawatasazwa.

*Na WYCLIFFE NYABER*

## KIAMBATISHO 16

Alhamisi, Julai 2, 2020 | TAIFA LEO

Matini 16

BUNGOMA

# Wazee Wabukusu wakaidi ushauri wa kusitisha tohara

**WAZEE** wanaopasha vijana tohara kutoka jamii ya Wabukusu, wanajiandaa kwa shughuli hizo licha ya kushauriwa na baadhi ya viongozi wa kijamii kuzisitisha kwa sababu ya janga la corona.

Wazee hao tayari wamefanya ibada ya kutakasa visu kwa maandalizi ya kutahiri vijana mnamo Agosti, licha ya juhudi za kuahirishwa kwa zoezi hilo kwa sababu ya sheria kali zilizowekwa kuzuia maambukizi ya maradhi ya Covid-19.

Mangariba hao ambao walikutana nyumbani kwa Bw Leonard Walusuna katika eneo la Liyabo, walisema walilazimika kufanya mila hizo ili kuwafurahisha mababu walioaga zamani.

Ikiwa shughuli hiyo haitafanywa mwaka huu, itabidi vijana wanaotaka kutahiriwa wasubiri hadi 2022.

Walisema hata kama zoezi hilo linaweza kuahirishwa, huenda wazazi wengine watajitokeza kutaka watoto wao watahiriwe lakini bila shamrashamra inayotangulia tohara inayojulikana kama Khuminya, kwa sababu ya sheria zilizowekwa na Wizara ya Afya.

*Na Gerald Bwisa*

## KIAMBATISHO 17

# Waomba Rais afungue sasa maeneo ya ibada

04/07/2020 Matini 17

**THARAKA-NITHI**

**KENNEDY KIMANTHI NA WACHIRA MWANGI**

VIONGOZI wa kidini wamemwomba Rais Uhuru Kenyatta aamuru kufunguliwa kwa maeneo ya ibada atakapolihutubia taifa kuhusu hali ya janga la Covid-19 nchini.

Akiongea na wanahabari mjini Chuka Alhamisi, mwenyekiti wa Baraza la Madhehebu Nchini (IRCK) tawi la kaunti ya Tharaka-Nithi, Deonisia Murungi alisema wameweka mikakati ya kuwakinga waumini dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema viongozi wa kidini katika eneo hilo wamekubaliana kwamba marufuku ya ibada ya wazi itakapoondolewa, watatii masharti yote yaliyowekwa na Wizara ya Afya.

"Ndiposa tunamwomba Rais wetu aturuhusi kujumuika pamoja kwa ibada kwa sababu tumefahamu kanuni za kuzuia kuenea kwa virusi vya corona," akasema Bw Murungi.

Alieleza kuwa maeneo ya ibada yatakapofunguliwa ni idadi ndogo ya waumini wataruhusiwa kuhudhuria ibada kwa wakati mmoja, ili kudumisha kanuni ya kutokaribiana.

"Vile vile, vifaa vyote makanisani vikiwemo viti vitanyunyiziwa dawa za kuangamiza viini na vieuzi kabla na baada ya kila ibada," Bw Murungi akaeleza.

Hata hivyo, katibu wa baraza hilo Silas Micheni alisema japo wanatarajia kwamba maeneo ya ibada yatafunguliwa, wako tayari kutii agizo lingine ambalo serikali itatoa ikiwa ni kuongezwa kwa muda wa marufuku.


Alisema vita dhidi ya janga la corona linapasa kuwa wajibu wa kila mmoja wala sio serikali pekee. "Tuko tayari kuzingatia agizo la Rais kwa sababu tunaamini anapata ushauri kutoka kwa wataalamu wenye uelewa mpana," akasema Bw Micheni.

Viongozi hao wa kidini ambao waliungama kuwa wanatambua hatari ya janga la Covid-19 walisema watawaonya waumini wao dhidi ya kusalimiana kwa mikono na kukumbatiana. "Vile vile, tutawahimiza kunawa mikono kabla ya kuingia makanisani, kutumia vieuzi na kuvalia barakoa ndani na nje ya maeneo ya ibada," akaeleza Bw Murungi.

Viongozi hao wa kidini waliipongeza serikali ya kaunti ya Tharaka-Nithi chini ya uongozi wa Gavana Muthomi Njuki kwa kuimarisha masharti ya kuzuia maambukizi kwa kuweka mitambo ya kunawa mikono kwenye malango ya afisi zake. Muungano wa Mapadri kutoka Mombasa (MPF) pia umetoa wito kwa serikali iwaruhusu waumini warejee makanisani kwa ibada kama zamani.

Mapadri hao walisisitiza watazingatia masharti yote yaliyowekwa na wizara ya Afya ili kuzuia kuenea kwa virusi vya corona makanisani.

Aidha walidai kuwa haki ya kukongamana na kuandaa ibada imenakiliwa kwenye katiba mpya.



**DEREVA wa trela apimwa ikiwa ameambukizwa COVID19 na afisa wa afya katika kituo cha NTSA Miritini kabla ya Waziri wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), Bw Adan Mohamed kuzindua kampeni ya uhamasishaji kuhusu corona jana katika barabara kuu ya Mombasa kuelekea Busia.** *Picha/ Laban Walloga*

**KIAMBATISHO 18**

UNTI

Matini 18
05/07/2020

Wataalamu wameanza kuhamasisha wakazi kuhusu mpango huo

# Wasomi Magharibi wapigia debe BBI

NA DERICK LUVEGA

VIHIGA

KUNDI la wataalamu kutoka eneo la Magharibi nchini wanaounga handisheki wameanza vikao vya kuhamasisha wakazi kuhusu Mpango wa Maridhiano wa BBI, kabla ya kuchapishwa rasmi kwa nakala ya mwisho.

Mkutano wa kwanza wa kundi hilo ukiongozwa Bw Joseph Simekha, ulifanyika katika eneo la Ebunangwe, kaunti ya Vihiga.

Viongozi hao wanataka mchakato huo uungwe mkono na wataalamu wote pamoja na wenyeji, huku wakisema hafla zingine kama hizo zinatarajiwa kufanyika katika kaunti zingine, eneo la Magharibi nchini, katika siku zijazo.

"Jukumu letu kubwa ni kuwaarifu wananchi jinsi BBI inavyoweza kuwakuza kiuchumi, kisiasa na kijamii," akasema Bw Simekha.

Mpango huo wa BBI ambao unatafuta kuleta mabadiliko ya kikatiba ulianzishwa na Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa chama cha ODM, Raila Odinga mnamo Machi 2018.

Zoezi hilo lililofanywa na kundi hili la wataalamu ni sawa na mchakato ambao ulifanywa na Gavana wa Kakamega, Wycliffe Oparanya na Waziri wa Ugatuzi, Eugene Wamalwa mwezi uliopita, na kusababisha mzozo wa kisiasa katika eneo hilo, ambalo lina wapiga kura wengi.

Bw Simekha, ambaye ni mshirikishi wa kikundi hicho, aliongoza idadi kubwa ya wataalamu hao kutoka sekta tofauti kwa kujitolea kuhamasisha watu katika eneo hilo, waunge mkono mpango wa BBI ambao unaweza kusababisha kuweko kwa kura ya maoni.

Alisema wana nia ya kuwaelezea wakazi jinsi mchakato huo utakavyochangia katika ukuaji wa uchumi, kukuza ugatuzi na kuhakikisha serikali iinachunguzwa vizuri jinsi inafanya kazi zake.

"Tutajaribu kubadilisha mawazo ya wananchi kuhusu siasa za kuleta mgawanyiko, ili kuwawezesha kutambua umuhimu wa mchakato huu ambao unakusudiwa kuleta umoja na ujumuishaji wa kila mmoja nchini," akasema Bw Simekha.

Afisa huyo alisema kuwa mawazo ya watu wengi katika mkoa huo kuhusu kuhusu BBI, yamepotoshwa. Alisema kuwa wengi hudhani ni propaganda.

Bw Simekha alibaini kuwa mpango huo unastahili kukuza dhamira ya mgao na ujumuishaji wa kila mmoja.

"BBI itashughulikia maswala ya kijamii na kiuchumi na pia itahakikisha umoja katika usimamizi wa maswala ya umma," akasema.

Bw Simekha alisema wanakusudia kuwafikia wataalamu wote na wenyeji wengine na kuwafanya waelewe mchakato huo.

"Hatuwaachii tu Bw Oparanya na Bw Wamalwa kazi yote," akasema.

Viongozi wa eneo la Magharibi pia wameonekana wakifaya mikutano mbali mbali katika kile kinachofasiriwa kuwa harakati za kujipanga kisiasa.

## KIAMBATISHO 19

Wasema magari yaegeshwa kiholela bila kujali hatari iliyopo

Matini 19 06/07/2020

# MCAs wataka steji za kati mwa jiji zitolewe

**NAIROBI**

**NA COLLINS OMULO**

MADIWANI wa Kaunti ya Nairobi sasa wanataka uongozi wa Nairobi Metropolitan Services (NMS), kuondoa maeneo ya maegesho na uchukuzi wa abiria katikati mwa jiji la Nairobi.

Madiwani hao wanadai kwamba waendeshaji wa magari ya umma wamegeuza barabara nyingi mijini na hata maeneo ya kutembea kama maegesho na sehemu za kuwabeba abiria bila kujali hatari iliyopo.

Kwenye mswada uliowasilishwa na diwani wa Woodley/Kenyatta Golf Course, Bw Mwangi Njihia, madiwani hao wanasisitiza kwamba uegeshaji magari kiholela kwenye barabara nyingi ndiyo umechangia ajali nyingi mjini haswa kugongwa kwa watu wanaotembea kando ya barabara.

Bw Njihia alitaja eneo linalopakana na Chuo Kikuu cha Nazerene jijini ambapo madereva wa magari ya uchukuzi wameligeuza pahala pa kuyaegesha magari yao na kuwabeba abiria bila kupokea idhini kutoka kwa kaunti.

"Magari ya PSV yanafaa yaruhusiwe kwa dakika chache tu mjini kuwabeba abiria na kuwashukisha wengine kisha yaelekee steji zao," akasema Bw Njihia.

Diwani huyo anayehudumu muhula wake wa kwanza amehoji kwamba kuna maeneo ya kuegesha magari yanayohudumu kwenye barabara mbalimbali lakini madereva wake na hata wahudumu wa bodaboda hawajakuwa wakizingatia hayo na kukataa kimakusudi kuyatumia.

Hii ndiyo maana mwanasiasa huyo amemtaka Meja Jenerali Mohammed Badi kupitia afisi yake, ahakikishe magari yanaegeshwa tu katika maeneo yao.

Hata hivyo, alisema maeneo ya maegesho yalitengewa magari yanayohudumu katika barabara mbalimbali mara ya mwisho mnamo mwaka wa 2000 na kuna haja ya maegesho hayo kupanuliwa kwa sababu idadi ya magari ya uchukuzi imeongezeka maradufu miaka kadhaa baadaye.

"NMS inafaa kubuni sera maalum ya kutenga maegesho mapya au kuyapanua yaliyomo pamoja na vituo vya mabasi nchini," akaongeza

Serikali ya Kaunti ya Nairobi kwa miaka mingi imeshindwa kuzima tabia ya madereva wa magari ya uchukuzi wa umma kuyaegesha kiholela kwenye barabara za katikati mwa mji.

Mara nyingi tabia hii husababisha msongamano wa magari na

Gavana Mike Sonko mara nyingi amewaonya maafisa wa kaunti akidai wana tabia ya kupokea hongo kutoka kwa madereva hao kisha kuwaruhusu wayaegeshe magari yao maeneo yasiyofaa.

Mapema mwaka jana maafisa wa kaunti walitwaa magari 100 yaliyoegeshwa pasipofaa kwenye barabara za Tom Mboya, Moi Avenue, Latema, Munyu na karibu na Gill House.



**MAGARI ya uchukuzi wa umma katika barabara ya Accra, Nairobi katika picha hii ya Machi mwaka huu. Madiwani wataka magari hayo yaondolewe katikati mwa jiji.** *Picha/ Dennis Onsongo*

**KIAMBATISHO 20**

4 **HABARI ZA KAU**

Matini 20
07/07/2020

**BARINGO**

# Majangili wajeruhi wafugaji wawili na kuiba mifugo 200

**WAFUGAJI** wawili walijeruhiwa kwa risasi kijijini Atirir katika Kaunti ndogo ya Tiaty baada ya kushambuliwa na wahalifu wenye silaha wanaoshukiwa kutoka kaunti jirani ya Turkana, ambao pia waliiba mifugo zaidi ya 200.

Shambulio hilo la Jumamosi lilitokea wakati majambazi zaidi ya 100 wenye silaha walipovamia kijiji hicho, na kuwashambulia wachungaji kabla ya kuwaibia mifugo na kuelekea katika vijiji vya Kamuge na Lokori katika Kaunti ya Turkana.

Hali ya taharuki imetanda katika eneo hilo huku shambulio hilo jipya likiibua uhasama kati ya jamii mbili zinazopigana za Turkana na Pokot.

Mwakilishi wa wadi ya Tirioko, Bw Sam Lourien alisema kuwa watu katika eneo hilo wametoroka nyumba zao kwa kuhofia mashambulio zaidi.

*Na Florah Koech*

## KIAMBATISHO 21

08/07/2020 Matini 21

# Wakulima wataka ukaguzi wa fedha kwa mashirika

NA GITONGA MARETE

**MERU**

**WAKUZAJI** kahawa kutoka Kaunti za Embu na Meru wametoa wito kwa Wizara ya Kilimo kufanya ukaguzi wa vitabu vya uhasibu katika vyama vya ushirika kama njia ya kutokomeza ufisadi uliokithiri katika sekta hiyo.

Wakulima hao wanadai kwamba baadhi ya maafisa wa vyama hivyo hushirikiana na wauzaji wa kahawa kuwafilisi pesa zao.

Aidha wakulima hao wamependekeza vyama vya ushirika ambavyo haiwezi kujisimamia kiuchumi, viunganishwe ili kuwaepushia wakulima gharama ya kuviendesha.

James Ireri ambaye ni mkulima wa kahawa Embu alisema baadhi ya mameneja wa vyama hivyo wamekuwa kikwazo na hupinga pendekezo la kuvifanyia ukaguzi wa hesabu rekodi zao.

"Wengi wa maafisa hawajapokea mafunzo ilhali wao ndio husimamia pesa za wakulima. Hawana ofisi na sioni haja ya wao kuendelea kuwabebesha wakulima mizigo ya kugharimia shughuli zao," akasema Bw Ireri.

Kinachomtia hofu zaidi Bw Ireri ni kwamba maafisa hao hukopa fedha kutoka benki bila kuwashauri wakulima.

## KIAMBATISHO 22

Matini 22 10/07/2020

# Walimu, wanafunzi watoa kauli tofauti kuhusu KCPE

Na MISHI GONGO

**MOMBASA**

WANAFUNZI na walimu wanaofunza da Darasa la Nane na Kidato cha Nne waliostahili kufanya mtihani wa kitaifa mwaka huu wameeleza hisia mseto baada ya serikali kufutilia mbali mitihani hiyo hadi mwaka ujao.

Huku baadhi wakisema hatua hiyo itawarudisha nyuma kimasomo, wengine walisema watapata nafasi kujiandaa vyema kwa mtihani.

"Nilikuwa nikijiandaa nikitarajia kuwa nitafanya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane mwishoni mwa mwaka huu, lakini sasa nahisi kama nilipoteza wakati," akasema Swabrina Omar mtahiniwa wa darasa la nane katika shule ya msingi ya Bomu, eneo bunge la Changamwe, Kaunti ya Mombasa.

Tangu shule zifungwe Machi kwa sababu ya janga la Corona, wadau katika sekta ya elimu wamekuwa wakijadiliana kuhusu kufunguliwa kwa shule hizo kwa ajili ya mitihani ya kitaifa.

Uamuzi ulitangazwa Jumanne na Waziri wa Elimu, Prof George Magoha kuwa mitihani ya kitaifa haitafanywa mwaka huu kwa kuwa maambukizi ya virusi vya corona yanaongezeka.

Mwanafunzi mwingine, Fatuma Mohammed kutoka Shule ya Upili ya Mama Ngina, Mombasa, alisema anahofia hatua ya kusukuma mbele mtihani hadi mwaka ujao huenda ikafanya wengine wao kulegea kimasomo.

"Kuna uwezekano mkubwa kwetu kutofanya vizuri kufuatia hatua hii," akasema.

Hata hivyo, mwanafunzi mwingine, Bilal Ali alisema angalau sasa wanafunzi watapata muda wa kutosha kujitayarisha.

"Kuna watahiniwa ambao hawana uwezo wa kufuatilia masomo mtandaoni. Tumekuwa nje ya shule tangu Machi," akasema.


Mwalimu anayesimamia wanafunzi wa darasa la sita hadi nane katika Shule ya Msingi ya M.M Shah na M.V Shah, Bw Bonface Ekirapa alisema muda walioongezewa utawasaidia kuwaandaa wanafunzi wao vilivyo.

Mwalimu mkuu katika shule ya Kisauni Bw Joshua Kuria alisema watatumia muda ulioongezwa kuwaandaa wanafunzi wao.

Wanafunzi wengine waliohojiwa katika kaunti tofauti pia walikuwa na hisia mseto.

Katika Kaunti ya Siaya, Mary Akoth alisema: "Serikali ingelegeza masharti ili watahiniwa wafanye mitihani yao. Hilo lingetupatia matumaini."

Ili kutolea maoni habari hii, nenda kwa taifaleo.nation.co.ke



WAZIRI wa Elimu Prof George Magoha akiwa darasani kwenye picha hii ya awali. Waziri alitangaza kuahirishwa kwa mitihani ya kitaifa hadi mwaka ujao kutokana na Corona.

**KIAMBATISHO 23**

# BBI si njama kufaidi watakaookosa viti

Matini 23
12/07/2020

**HOMA BAY**

Na GEORGE ODIWUOR

VIONGOZI watatu wa chama cha ODM wamekanusha madai kuwa mageuzi ya kikatiba yanayotarajiwa kutekelezwa chini ya ripoti ya Mpango wa Maridhiano (BBI), yanalenga kubuni nafasi za kisiasa kwa viongozi wanaoshindwa kwenye uchaguzi.

Watatu hao ni Kiongozi wa Wachache kwenye Seneti, Seneta James Orengo, Seneta Moses Kajwang' (Homa Bay) na mbunge Otiende Amollo (Rarienda).

Badala yake, viongozi waliwahakikishia Wakenya kuwa ripoti hiyo inajumuisha mabadiliko kuhusu masuala yanayowahusu Wakenya kama uwazi kwenye mchakato wa chaguzi.

Bw Orengo aliwaambia Wakenya kujitayarisha kwa mageuzi mazuri ya kikatiba yatakayowafaa.

Seneta alidai kuwa baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakipinga utekelezaji wa mpango huo.

Baadhi ya viongozi wanaoegemea upande wa Naibu Rais William Ruto wamekuwa wakiupinga mpango huo, unaoungwa mkono na Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa ODM, Bw Raila Odinga.

Mpango huo umezua migawanyiko miongoni mwa viongozi, baadhi wakiutaja kuwa mbinu ya wanasiasa wanaoshindwa kwenye uchaguzi kuingia serikalini.

Bw Orengo aliwalaumu baadhi ya viongozi wanaopinga mageuzi ya kikatiba kwa kueneza uwongo kuihusu ripoti ili kuwapotosha Wakenya.

"Wanasiasa wanaopinga ripoti wanapaswa kukoma kueneza uvumi kuhusu yale yaliyopo ndani yake," akasema.

Akizungumza Ijumaa wakati wa mazishi ya Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda vya Kutengeneza Kemikali Kenya (KCWU), Bw Were Ogutu, eneobunge la Karachuonyo, Bw Orengo alisema kuwa utekelezaji wa ripoti utajikita kwenye katiba bila kuzingatia matakwa ya mtu yeyote binafsi.

"Hakuna yeyoye anayepaswa kuwadanganya kuwa mageuzi yatakayotekelezwa kwenye katiba yanalenga kubuni nafasi kwa baadhi ya viongozi kama wanavyodai wanasiasa wanaopinga ripoti," akasema.

Alisema kuwa mapendekezo yaliyo kwenye ripoti yatawekwa kwenye Katiba kupitia kura ya maamuzi na mchakato utakaoendeshwa na Bunge la Kitaifa.

"Rais Kenyatta na Bw Odinga watakabidhiwa rasmi ripoti katika siku kadhaa zijazo. Baadaye itawasilishwa kwa Wakenya ili waitathmini na kutoa mapendekezo yao. Baada ya hapo itageuzwa kuwa katiba, japo kwa kuzingatia mapendekezo yatakayotolewa," akasema.

"Viongozi wanaoendesha kampeni kuipinga ripoti wanapswa kukoma. Tunataka Kenya kuwa na amani hata baada ya uchaguzi. Hili linaweza tu kufanikishwa kupitia mageuzi ya kikatiba yaliyojumuishwa kwenye ripoti. Mpango huo ni kama gari la moshi ambalo haliwezi kusimamishwa na yeyote," akasema Bw Kajwang.

Kwa upande wake, Bw Amollo alisema kuwa ripoti itahakikisha uwepo wa uongozi mzuri nchini.

Baadhi ya wanasiasa wanaomuunga mkono Dkt Ruto wamekuwa wakisema kuwa ripoti ni njama fiche inayolenga kuhakikisha kuwa viongozi watakaoondoka serikalini watarejea kwa mlango wa nyuma baada ya uchaguzi wa 2022.



**Senata wa Siaya James Orengo akihojiwa katika afisi yake bungeni mwaka jana.**
*Picha/Maktaba*

## KIAMBATISHO 24

NYERI 13/07/2020

Matini 24

# Mama, mwanae wafa lori lilipogongana na matatu eneo la Kiganjo

**MAMA** na mwanawe mwenye umri wa miaka miwili jana walifariki kwenye ajali mbaya ya barabarani eneo la Kiganjo kwenye barabara ya Nyeri-Nanyuki.

Ajali hiyo ilitokea baada ya lori kugonga matatu saa nne asubuhi huku mwendeshaji wa lori hilo akilaumiwa kwa kuliendesha vibaya na kusababisha mauti hayo.

Watu kadhaa pia walijeruhiwa wakati wa kisa hicho na wakapelekwa kupokea matibabu katika hospitali ya rufaa ya Kaunti ya Nyeri.

Kamanda wa Polisi wa Nyeri ya Kati, Bw Paul Kuria, alieleza Taifa Leo kwamba matatu hiyo ilikuwa ikielekea upande wa Chaka wakati ambapo lori hilo lilitokea upande wa pili na kuigonga kwenye mzunguko karibu na Chuo cha polisi cha Kiganjo.

"Mtoto aliaga dunia eneo la ajali lakini mamake akafariki akipokea matibabu katika hospitali ya rufaa ya Nyeri. Tunaendeleza uchunguzi na hata kupokea ripoti kutoka kwa manusura hospitalini," akasema Bw Kuria.

*Na Nicholas Komu*

## KIAMBATISHO 25



UNTI

Matini 25

### Zaelezea hofu ya shule zaidi ya 1,000 kukosa kufunguliwa tena kutokana na athari za corona

# Shule za kibinafsi zalilia serikali

**MOMBASA**

MISHI GONGO na GITONGA MARETE

ZAIDI ya shule 1,000 za kibinafsi nchini huenda zikakosa kufunguliwa mwaka ujao, chama cha shule za kibinafsi nchini (KPSA), kimesema.

Naibu mwenyekiti wa chama hicho, Bw Isaiah Mbaabu, alisema kuna shule za kibinafsi 11,000 nchini, asilimia 10 ya shule hizo zimeathiriwa na corona, ikizingatiwa ziko katika majengo ya kukodisha.

Shule hizo zimeajiri zaidi ya wafanyakazi 200,000 ambao tayari wameachwa bila ajira, huku zaidi ya watoto 300,000 wanaotarajiwa kurudi shuleni mwaka 2021, wakiwa hawana pa kwenda.

"Walimu wengi wameacha ualimu na kuingilia biashara nyingine kujipatia riziki. Tumeshindwa kuwalipa mishahara kwa zaidi ya miezi mitatu," akasema Bw Mbaambu.

Jana, wawakilishi wa shule za kibinafsi jijini Mombasa, walilalamika kutengwa katika misaada inayotolewa na serikali ili kuwalinda wasiojiweza katika jamii.

Wawakilishi hao walisema licha ya wao kuwa miongoni mwa wanaotoa huduma muhimu nchini, serikali haijashughulika kuwakinga kutumbukia katika dimbwi la uchochole.

Wakizungumza na wanahabari katika afisi za shirika la Haki Africa, mwenyekiti wa shule za kibinafsi mjini Mombasa, Bw Omar Mboli alisema si sawa watu wa sekta zingine kufadhiliwa na serikali huku wao wakitelekezwa.

"Tunasikitika kuona serikali imetoa ufadhili kwa wasanii, wadau wa sekta ya hoteli, makahaba na kadhalika, ilhali sisi hatujatambulika licha ya kutoa huduma muhimu nchini," akasema.

Alisema tangu kufungwa kwa shule kufuatia kuzuka kwa ugonjwa wa COVID 19 nchini, walimu wengi wanaohudumu katika shule za kibinafsi wanashindwa kujikimu kimaisha.

Mwenyekiti huyo alisema walimu wa shule za kibinafsi wamesajiliwa katika bodi ya ualimu sawia na wale wa shule za umma. Hivyo wote wanafaa kuangaliwa na serikali.

Bw Mboli alisema tayari wamepoteza walimu watatu mjini Mombasa waliojiua kufuatia hali ngumu ya maisha.

"Juzi mwalimu mmoja alifungiwa nje akiwa na mtoto wa miezi sita kwa kukosa kulipa kodi ya nyumba. Walimu waliojitoa uhai ni kufuatia kushindwa kukimu familia zao," akasema.

Alisema tangu kufungwa kwa shule ili kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona, wamiliki wa shule za kibinafsi wameshindwa kuwalipa mishahara walimu na wafanyakazi wengine katika shule hizo.

Mwenyekiti wa shule za kibinafsi katika eneo bunge la Mvita, Bw Shadrak Attik, alisema walimu wanapitia hali ngumu ya kiuchumi na wanahitaji msaada wa haraka kutoka kwa serikali.

"Tunahitaji msaada wa haraka,tunashukuru baadhi ya walimu waliajiriwa katika kazi za mtaani,lakini bado kuna wengine hawajabahatika," akasema.

Aliwasuta viongozi wa serikali kwa kuwakumbuka nyakati za kusaka kura pekee.




Mwenyekiti wa shule za kibinafsi eneobunge la Mvita, Bw Shadrack Atik (kati) akiongea na wanahabari jana katika afisi za shirika la Haki Africa mjini Mombasa. Aliandamana na mwenyekiti wa walimu wakuu shule za kibinafsi, Bw Omar Buli (kulia) na mkurugenzi wa Muslim Schools eneo la Makupa, Bi Firdousa Woche (kushoto). *Picha/ Mishi Gongo*

**KIAMBATISHO 26**

24/07/2020 Matini 26

## Hatimaye baba apokea msaada baada ya corona kumletea dhiki



**BENJAMIN Kilonzo na mwanawe ambao wamekuwa wakilala kichakani katika Kaunti ya Machakos baada ya kufukuzwa kwenye nyumba waliyokuwa wakiishi kwa kushindwa kulipa kodi.** *Picha/Hisani*

# Walikimbilia kichakani baada ya kukosa kodi

Na MWANDISHI WETU

**MACHAKOS**

MWANAMUME na mwanawe, ambao wamekuwa wakilala kichakani katika kaunti ya Machakos, baada ya kutimuliwa kwa nyumba waliyokuwa wakiishi waliposhindwa kulipa kodi, walipokea msaada jana kutoka kwa wahisani.

Katika mahojiano na *Taifa Leo,* Bw Benjamin Kilonzo, alisema mambo yalimwendea mrama kufuatia janga la corona na akashindwa kumudu kulipa kodi ya nyumba.

"Nilikuwa nikifanya vibarua na kuuza kuni katika mikahawa na vibanda vya kuuzia chakula mjini Machakos, lakini vilipofungwa kwa sababu ya janga la corona, nilikosa mbinu ya kujipatia mapato," alisema mwanamume huyo ambaye amedhoofika kiafya.

Alieleza kwamba baada ya kukosa kodi ya nyumba, landilodi alimfukuza na akawa hana pa kwenda.

Baada ya kukosa ajira na kufukuzwa nyumba aliyokuwa akiishi, alijaribu kumpeleka mwanae kwao Kangundo lakini jamaa zake walimrudisha mjini Machakos.

"Nilimtuma mwanangu nyumbani Kangundo akaishi na ndugu zangu lakini walikataa kumpokea na akarudi kuungana nami tena," alisema.

Tangu wakati huo, wawili hao wamekuwa wakiishi kichakani katika mtaa wa Kathaayoni viungani mwa mji wa Machakos, ambapo ameunda makao kwa kutumia karatasi za plastiki na magunia.

Bw Kilonzo na mwanawe wa kidato cha pili wamekuwa wakilala kwenye godoro lililochanika wakivumilia baridi kali usiku.

Kwa miezi mitatu, hawajawahi kubadilisha nguo na huwa wanategemea chakula kutoka kwa wasamaria wema.

Jana wasamaria wema waliwapa makao na pesa za matumizi baada ya masaibu yao kuangaziwa na vyombo vya habari.

Padri Lazarus Musyoka aliwapa nyumba ya kuishi, naye pasta Maurice Oloo akawapa Sh15,000 waanze maisha yao upya.

Wahisani wengine pia waliwasaidia kwa vifaa mbali mbali vya matumizi..

"Mke wangu alitoroka na kuniachia mtoto huyo akiwa na miaka miwili. Nimefanya vibarua kumlea na kumsomesha hadi shule ya upili lakini corona imevuruga maisha yetu," alieleza.

**KIAMBATISHO 27**

KAUNTI · 25/07/2020 Matini 27

## Gavana asema visa vya unyakuzi wa ardhi vimeongezeka kaunti

# Mvurya aalika DCI kusaka wanyakuzi

**KWALE**

**NA FADHILI FREDRICK**

SERIKALI ya kaunti ya Kwale, inashirikiana na afisi ya Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI), kupambana na ongezeko la visa vya unyakuzi wa ardhi katika kaunti hiyo.

Gavana Salim Mvurya alisema utawala wake utaisaidia DCI kuwanasa wahusika katika uovu huo ili waadhibiwe kwa mujibu wa sheria.

"Serikali yangu imekuwa mstari wa mbele kulinda rasilmali ya ardhi dhidi ya watu wenye nia ya kuitwaa kinyume cha sheria. Kwa hivyo, tutawasaidia maafisa wa DCI kuhakikisha kuwa wanyakuzi wa ardhi wanaadhibiwa," akasema Bw Mvurya.

"Ardhi ni hitaji muhimu katika mpango wa uzalishaji chakula, vita dhidi ya umaskini na shughuli za utunzaji mazingira," alisema.

Gavana Mvurya alisema afisi yake ina habari kwamba kuna tajiri mmoja ambaye ameghushi stakabadhi na kunyakua sehemu ya msitu wa Kaya Tiwi.

Aliongeza kuwa kamati zimeundwa kinyume cha sheria katika ranchi za Mwereni na Lunga Lunga kwa lengo la kuuza sehemu za ardhi hizo kwa wastawishaji wa kibinafsi.

"Ningependa kukariri kwamba hatutaruhusu vitendo kama hivyo kuhujumu juhudi ambazo tumeweka kulinda rasilmali kwa manufaa ya umma," Gavana Mvurya akasema.

Mkuu huyo wa kaunti alisema hayo wakati ambapo zaidi ya familia 2,000 zinazoishi katika mpango wa makazi kwa jina *"Sheep and Goats Settlement Scheme"* kaunti ndogo ya Matuga, zinakabiliwa na tishio la kufurushwa baada ya watu wenye ushawishi kunyakua sehemu kubwa ya ardhi hiyo.

Wenyeji wanadai kuwa serikali iliahidi kuwagawia ekari 80, 000 za ardhi lakini sasa wanashangaa kuwa wageni wanapewa vipande vikubwa vya ardhi. Mkazi, Bw Ali Njiwa, alisema ameishi hapo tangu mwaka wa 1992 aakidai kuwa serikali ya Kanu ilipteketeza nyumba zao, na sasa anashangaa kuwa watu wengine wamefika hapo wakidai ndio wamiliki halisi.

"Walikuja na stakabadhi wakidai tuondoke kwamba ardhi hii ni yao. Sasa tumeshindwa la kufanya kwa sababu tuliahidiwa ardhi lakini sasa nyumba zetu zimeteketezwa. Sisi ndio maskwota halisi sio wale wanaokaa katika afisi kubwa," akasema.

Bw Omar Mwamaisha, mkazi mwingine alisema wanaishi kama maskwota kwani hawawezi kujenga nyumba za kudumu.

"Haitakuwa haki kama sisi ambao tumeishi hapa kwa miaka mingi hatutapewa hatimiliki na badala yake wageni ndio wanapewa," akasema.

## KIAMBATISHO 28

BARINGO 28/07/20
Matini 28

# Maji ya ziwa yatatiza usafiri katika barabara kuu

**NA FLORAH KOECH**

ONGEZEKO la kiwango cha maji katika Ziwa Baringo linahatarisha usafiri kwenye barabara ya Marigat-Loruk-Chemolingot, Kaunti ya Baringo baada ya maji kufurika hadi kwa barabara kuu inayounganisha zaidi ya kaunti tano jirani.

Barabara hiyo inaunganisha Baringo na kaunti jirani kama Turkana, Laikipia, Samburu, Isiolo, West Pokot na Elgeyo Marakwet.

Hali hii pia imehamisha watu zaidi ya 300 na wafanyabiashara katika kituo cha kibiashara cha Loruk karibu na Ziwa hilo.

Kulingana na wenyeji, kiwango cha maji kimeongezeka pakubwa katika kipindi cha mwezi mmoja na huku ikiathiri nyumba kadhaa zilizoko kando ya ziwa hilo.

Haron Cheburet, mwenyeji wa Loruk aliibua wasiwasi wa watumizi wa barabara wamo hatarini kusombwa au kushambuliwa na viboko na mamba.

"Viwango vya maji katika ziwa vimekuwa vikiongezeka hapo awali wakati wa mvua lakini haijawahi kufikia kiwango cha kumeza barabara ya lami. Mamia ya wenyeji huko Loruk pia wamehamishwa kutoka nyumba zao, jambo ambalo halijawahi kushuhudiwa katika eneo hili," akasema Bw Cheburet.

"Maji yanaendelea kuongezeka kila siku na hivi karibuni madereva watalazimika kutafuta njia mbadala kwa sababu barabara iko kwenye maji mengi," akaongeza.

Kufurika kwa maji ya ziwa katika barabara hiyo kuu ya takriban kilomita 65 pia kunatishia kufungwa kabisa kaunti ndogo ya Tiaty kupata huduma za kijamii katika miji ya Marigat na Kabarnet.

Barabara hiyo ni muhimu pia kwa usalama kwani maafisa wa usalama huitegemea wanapoenda kukabiliana na wizi wa mifugo.

**KIAMBATISHO 29**

KISII 29/07/2020

Matini 29

# Ongwae aitikia ombi la bodaboda

NA WYCLIFFE NYABERI

WAHUDUMU wa bodaboda katika Kaunti ya Kisii, wamepata afueni ya kutolipa ushuru kwa kipindi kingine cha miezi miwili kutoka kwa serikali ya kaunti.

Wiki moja baada ya Taifa Leo kuangazia kilio cha bodaboda hao, Gavana James Ongwae ametikia ombi lao pamoja na wafanyabiashara wengine wadogo ambao hawatalipa ada za kaunti hadi Oktoba.

Gavana aliwataka maafisa wa serikali hiyo kutowahangaisha bodaboda wanapohudumu kwani Wakenya wengi, hasa vijana wanategemea sekta hiyo kujichumia riziki yao. Hatua hii imepokelewa vyema na wahudumu hao ambao wamemshukuru Bw Onwae kwa kuwajali.

"Kwa hakika tuna furaha kwa kupata afueni nyingine. Gavana wetu ni mtu wa kusikiza furaha ya mnyonge na tunampa mkono kwa hilo," akasema Bw Amos Kaisa, mmoja wa wanabodaboda.

Imebainika kuna baadhi ya walimu ambao wanajichumia riziki kutoka kwa sekta hiyo baada ya shule kufungwa.

Wiki iliyopita, wahudumu hao walimwomba Gavana Ongwae kuwaongezea afueni kwa mara nyingine, jambo ambalo sasa amelitimiza.



**Gavana wa Kisii James Ongwae akipokea vifaa vya madaktari kujikinga na maambukizi ya Corona, juzi.** *Picha/Ruth Mbula*

**KIAMBATISHO 30**

# Simanzi gwiji wa ushairi akifariki

30/07/2020

Matini 30

NAIROBI

JUMA NAMLOLA na CHRIS ADUNGO

WAPENZI wa Kiswahili wamepata pigo baada ya mshairi mkongwe Abdalla Mwasimba kuaga dunia hapo jana akiwa na umri wa miaka 83.

Jamaa na marafiki waliofika katika makaburi ya Waislamu ya Kariokor, Nairobi, walimmiminia sifa Mzee Mwasimba, ambaye ni Mkenya wa kwanza kuwahi kughani mashairi redioni.

Mtindo wake wa kughani ulivutia wengi, akiwemo mshairi Nuhu Zubeir Bakari almaarufu Al-Ustadh Pasua.

"Nimempoteza mwalimu aliyeniachia kikoba cha ughani wa mashairi. Alinichochea kuanza kuchangia mashairi magazetini nikiwa mwanafunzi wa darasa la sita. Ilikuwa tija kumsikiliza akighani tungo zangu redioni na imekuwa fahari kufanya naye kazi katika shirika moja," akasema Bakari.

Mwasimba amekuwa akikagua na kusahihisha mashairi yanayochapishwa katika magazeti ya ***Taifa Leo*** na ***Taifa Jumapili.*** Aliugua kisukari na presha kwa muda mrefu.

Mwanawe mdogo wa kiume, Bw Mwasimba Abdallah, alisema babake alizidiwa na maradhi hayo Jumanne usiku na akakata roho mwendo wa saa kumi alfajiri.

Mtangazaji mkongwe Badi Muhsin alimsifia Mwasimba kuwa mwalimu wa wengi katika ushairi na tasnia ya uanahabari.

"Alikuwa mtu wa watu. Hakukosa ucheshi kila alipouliza maswali au kunasihi kupitia ushairi. Aliwahi kuniuliza: Iwapo mpera huzaa mapera, mwembe huzaa maembe, mgomba huzaa nini?"

Mashairi yake, ***Faida ya Pombe Nini, Mzungu Kutuita Bwana*** na ***Kuvaa Hirizi*** yaliwapa vijana changamoto ya kuachana na ulevi na kujitahidi kazini bila ya kutegemea mitishamba.

Kutokana na weledi wake katika ushairi, Mwasimba alitunukiwa tuzo kadhaa na Kituo cha Kiswahili cha WASTA kinachomilikiwa na Guru Ustadh Wallah Bin Wallah mjini Ngong.

"Tumeondokewa na nguzo ya Ushairi wa Kiswahili na kigogo ambaye mashairi yake hayakuwa yakitungwa kwa kalamu. Alikirimiwa kipaji adhimu na uwezo wa kutunga papo kwa hapo."

"Mwasimba alikuwa mnyenyekevu, mwenye roho safi na mwepesi wa kuitikia wito. Alihudhuria hafla zote za kutolewa kwa *Tuzo za WASTA* na akatufundisha umuhimu wa kuthamini Kiswahili," akasema Guru Ustadh Wallah Bin Wallah.

Tuzo kubwa zaidi ambayo Mwasimba aliwahi kupata ni kutambuliwa na Rais Uhuru Kenyatta mnamo 2015.

Alipewa tuzo ya *Head of State Commendation* (HSC) kwa mchango wake katika makuzi ya Kiswahili. Aliwahi pia kuongoza kikundi cha wanafunzi kutoka Nairobi, kuimba shairi wakati wa sherehe za ufunguzi wa Michezo ya Bara la Afrika mnamo 1987 katika uwanja wa MISC Kasarani.

Mwingine aliyewaongoza wakereketwa wa Kiswahili kumuomboleza Mwasimba ni Afisa Mkuu Mtendaji wa *Kenya Yearbook Editorial Board*, Bw Edward Mwasi.

"Tumepoteza gwiji, malenga na mshairi hodari. Nilifanya kazi na Mwasimba katika gazeti la ***Taifa Leo*** nilikosimamia usanii wa michoro. Alikuwa mcheshi na Kiswahili kilimtiririka kwa urahisi kabisa. Alichangia sana makuzi ya lugha hii Afrika Mashariki. Kwa heri shujaa," akasema Mwasi.

Mwanahabari wa Radio Maisha, Hassan Kauleni mwana wa Ali, alisema: "Kwake Mola ndiko tutokako na kwake ndiko turejeako. Kila nafsi itaonja mauti. Lala salama mzee wetu."

Mwasimba alizaliwa mnamo 1937 katika eneo la Msambweni, Kaunti ya Kwale. Alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msambweni na akaachia masomo katika darasa la tano. Mnamo 1955, alielekea Tanganyika kujifunza ulehemu (*welding*) katika Shule ya Ifunda, Mkoani Iringa.

Aliporejea Kenya mnamo 1956, alipata kibarua cha kuchomelea vyuma katika mojawapo ya karakana za kutengeneza vitanda na madirisha jijini Mombasa. Alihamia Nairobi mwishoni mwa 1957.

Umahiri wake wa kutunga na kuimba mashairi uliwaridhisha vinara wa Kenya Broadcasting Service (kabla ya kuitwa VOK) kiasi kwamba walimpa jukumu la kuyaghani mashairi katika kipindi kilichoongozwa na Hassan Mazoa, Daniel Katuga, Mahfudh Bawazir, John Nzau na baadaye Khadija Ali. Alihudumu huko kati ya 1958 na 2003 kisha akapata nafasi ya kuendesha kipindi ***'Dunia Ina Mambo'*** katika runinga ya QTV .

Malumbano ya hoja nzito zenye busara kuhusu masuala ya ndoa na dini kati ya Pala Mlanzi Hassan kutoka Rufiji na Shabaan Bin Robert kutoka Tanga, Tanganyika yalimvutia sana tangu utotoni.

Kwa hofu ya kutoruhusu chochote kumfutu katika mijadala yao, ilimlazimu kila siku kusoma magazeti ya ***'Mamboleo'*** (Tanganyika) na ***'Baraza'*** (Kenya). Mashairi ya wawili hao yalichapishwa katika magazeti hayo.

Akiongozwa na tamaa ya kuvifikia viwango vyao, Mwasimba alimtungia msichana mmoja wa darasa la tatu shairi la mapenzi ambalo liliwasisimua walimu na wanafunzi wote shuleni Msambweni mnamo 1947. Hapo ndipo kipaji chake cha kutunga mashairi kilianza kudhihirika.

Wakati akiyaghani mashairi KBC, pia aliaminiwa kuendesha vipindi ***'Ubingwa wa Lugha', 'Kuzungumza ni Kuelewana'*** na ***'Baraza la Wazee'***. Kwa kuwa uigizaji ni kipaji kilichojikuza ndani ya Mwasimba tangu akiwa tineja, alianza kutunga na kurekodi michezo ya kuigiza ya ***'Usipoziba Ufa', 'Mchezo wa Wiki', 'Ushikwapo Shikamana'*** na ***'Kikulacho Ki Nguoni Mwako'.***



**BAADHI ya waombolezaji watia dua kando ya kaburi la mshairi maarufu Abdallah Mwasimba katika makaburi ya Kariokor, Nairobi.** *Picha/Juma Namlola.*

## 'Kazi Mtaani' kuifaa shule kwa madarasa mapya

**SHULE** ya upili katika Kaunti ya Makueni, sasa imekita matumaini yake kwa vijana walio kwenye Mpango wa Kazi Mtaani kujenga madarasa kwa wanafunzi wake zaidi ya 1,000 watakaporejea shuleni mwakani.

Shule ya Upili ya Mikuyuni, ina jumla ya wanafunzi 962, hilo likiifanya kuwa shule ya mseto na kutwa yenye idadi kubwa zaidi ya wanafunzi katika kaunti hiyo. Usimamizi wake unasema unatarajia wanafunzi wengine zaidi ya 500 kujiunga nayo Januari mwaka ujao, wakati shule zitakapofunguliwa upya.

Shule imeshuhudia ongezeko la idadi kubwa ya wanafunzi katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

*Na Pius Maundu*